

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report of

**DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL, NAROK NORTH
CONSTITUENCY, HELD AT NAROK COUNTY COUNCIL HALL**

ON

17TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL NAROK NORTH CONSTITENCY HELD AT NAROK
COUNTY COUNCIL HALL ON 17TH OCTOBER 2002**

Present:

Programme Officer	-	Mr. George Nakholi
Asst. Programme Officer	-	Maurice Kepoi Karia
District Coordinator	-	Ben Molel

Mr. Nakholi: Asante, kwa sababu ilikuwa ni nia ya WaKenya kuhakikisha kwamba hii Katiba yetu inaanzia kwa msingi wa imani, ya kwamba waKenya wanaoamini Mungu. Na kwamba ni watu huru watu wa taifa hili, kwa hivyo bila shaka tumenakili hiyo na tutahkilisha kumewakilisha kwenye Tume.

George Nakholi: Utangulizi mara kwa mara, kila Constituion la ulimwengu inaanza na hii preamble. Ijapokuwa ile ya Constituion ilioko sasa haina kwa sababu ilifanyiwa huko Uingereza, haikufanyiwa na wa Kenya vile tunafanya saa hii. Asante sana, kama hakuna jambo lolote kutoka kwa wananchi wa Narok, sasa Bwana Karia atatuelezea upande wa act. Kuna mambo mengi sana juu ya, ambao tutazungumzia juu ya Constituion hii, kuna mambo mengi. Lakini umeona mambo ya ardhi ni ya muhimu sana kwa jamii ya Masai. Kutoka huko, tulikuwa Namanga, mpaka kuja Kajiado Central, na Kajiado North na kutoka huko tumekuwa huko na Transmara, tumeona kweli ni haki mambo ya ardhi ni muhimu sana kwa jamii ya Masai na other pastoral communities. Kwa hivyo, tumeona ya kwamba, vile tumefanya mahali popote, pia tuende kwa mambo ya ardhi, ili ichukue muda ule unao tosha. Na mukiwa na maswali na maoni mtoe kabisa kwa sababu hii ni kama hot cake kwa jamii ya wa Masai. Kwa hiyo, nitapatia Bwana Karia tena aendelee na hiyo jambo la ardhi, na tusikize kwa makini tukiwa na jambo tutoe tuchangishe. Asante sana. Bawana Olelare.

Maurice Karia Olerare: Asante sana Bwana Nakholi. Wananchi ningependa kuwaeleza ya kwamba hii sura inayo zungumzia ardhi ni sura ya kumi na moja katika nakala zenu, kutoka kipengele ya 232, hapo ndiyo mtapata sura inayo zungumzia juu ya ardhi. Ni tumaini langu kwamba ni swala ambalo litachukua muda wetu sana, kwa sababu hasa shida ama maoni mliotoa wananchi yalikuwa yanahu su ardhi. Ukurasa 28, page 28, katika nakala hizo za Kingereza.

Basi wananchi ningependa kusema ya kwamba ardhi ni rasilmali muhimu sana kwa watu wote wa Kenya. Ardhi ni rasilmani muhimu sana kwa ukuzaji wa uchumi wa nchi hii kwa sababu ya kwamba wa-Kenya wengi wanategemea ardhi kwa shughuli zao za kiuchumi. Tunasema kwamba utu wa mgongo wa nchi yetu ni kilimo na kilimo hasa inaweza tu kuifanyika kukiwa na ardhi pale. Na kwamba ni rasilmali muhimu sana, kwa sababu hakuna shughuli yoyote ya kiuchumi unaweza kuendeleza kama hakuna ardhi. Kwa hivyo mambo ya ardhi yamepewa umbele sana katika maoni ya wananchi wakati ma-Commissioners

walikuwa wanaenda katika sehemu tofauti za nchi. Ijapokuwa shida za wananchi kuhusu ardhi ni tofauti tofauti, lakini swala la ardhi liliweza kutokea katika kila kituo katika Jamhuri. Na wananchi wamesema kwamba kuna shida nyingi sana kuhusu ardhi, na ukijaribu kuangalia jamii zinazo ishi kati ya Kajiado, Transmara na Narok, shida za ardhi ambazo wako nazoz hivi sasa zonawenza kueleweka vizuri sana tukirejelea historia ya nchi hii. Kwa sababu kuna treaties, ama mikataba ilio wekwa baina ya viongozi wa wakati huo ama machifu wa wakati huo, na wakoloni Waingereza ambao wali vamia nchi yetu katika miaka za 1904, na 1911. Kwa hivyo, kulikuwa na mikataba ama treaties, ambazo ukijaribu kuangalia hasa shida zilizo Masaini hasa juu ya ardhi, zinatokana hasa na mikataba hiyo.

Wananchi katika jamhuri waliweza kutoa sababu tofauti tofauti kuhusu shida wanazo juu ya ardhi Ningependlea tu kuwapeleka kwa mukhtasari hii hizo shida ambazo wananchi walizungumzia juu ya ardhi na hapo ndipo nitarudi niwaeleze ishara gani ama ni policy gani Katiba hii imetua kuhusu ardhi. Wananchi wamesema ya kwamba, kwa wingi walisema ya kwamba hata miaka 40 baada ya kupata uhuru wananchi wengi wangali hawana ardhi, wangali ni squatters, kwa hivyo ni shida moja ambayo iliweza kutokea hasa katika vituo vingi vya Kenya. Wananchi pia wamesema ya kwamba ijapokuwa kuna wa Kenya hawana ardhi, pia kuna watu wachache ambao wameshikilia ardhi kubwa sana, na kwamba hiyo ni shida ya kutokuwa na usawa na kwamba hii ndiyo sababu ya shida nyinyi zinazotokea kama mizozo.

Wananchi pia wamesema kwamba kupata takabali ya kumiliki shamba, kupata title deed, ilikuwa liko na garama na inachukua pia muda mrefu sana ili uweza kupata takabali ya kumiliki shamba. Wananchi wakasema kwamba iko na garama, ni lazima utumie pesa nyingi sana ili uweze kupata stakabadhi ya kumiliki shamba. Na pia ile process inachukua muda mrefu sana na ni shida ambao wananchi pia wamezungumzia. Wananchi pia wamesema ya kwamba kuna sheria nyingi sana ambazo zina husu ardhi, katika sheria tulizo nazoz hivi sasa, kuna sheria nyingi sana ambazo zinahusu ardhi, na kwamba sheria hizo haziambatani. Basi wananchi walishawishi Tume ya kurekebisha Katiba, iweze kuja na muongozo ama sheria moja au chache ambazo zinahusu ardhi na ambazo wananchi wanaweza kufuata. Saa hii kuna sheria 19, zinazo husu ardhi na kwamba sheria hizi ni za kikoloni kwa sababu zilikuwa zinawasaidia wao tu. Zilikiwa zinasaidia wakoloni kuweza kunyakua ardhi ya wa Kenya ni sheria zilizoweza wakoloni kuweza the white settlers, kuweza kupanya katika sehemu za Masaini. Kwa hivyo sheria hizi ndizo zilisababisha wananchi waambie Tume hii ya Kurekebisha Katiba iweze kuja na sheria fulani, chache, na sera ama policies za ardhi ambazo wanaweza kuelewa. Kwa sababu, hizi sheria, sheria moja inakupa haki ya kumiliki ardhi, na ukienda sheria nyingine inakupokonya hiyo haki ya kumiliki ardhi.

Wananchi pia wamesema kwamba stakabadhi hizi za mililki mashamba zinapatikana kwa mbali. Either unapaswa kwenda Nairobi katika Lands ili uweze kupata sstakabadhi ya kumiliki shamba, ama uende katika mkoa ambao mara kwa mara ni mbali sana. Ningependa kutoa mfano wa Marsabit, Mwananchi wa Marsabit, ambaye mkoa wake ni Embu, basi atalazimika kwenda kilometer zaidi ya 650 ili aweze kupata msstakabadhi ya kumiliki shamba. Kwa hivyo wananchi walisema ni lazima Tume ya kurekebisha Katiba iweze kubuni njia ya ku hakikisha kwamba sstakabadhi za kumiliki mashamba zinapatikana karibu nao. Na wananchi tutawaeliza itawezekana namna gani kuweza kupata sstakabadhi hizo za kumiliki mashamba kwa eneo la karibu. Na

wakati tutakapo enda kwa usambazaji, kwa madaraka ama devolution, mtakuta ya kwamba kutakuwa na serikali hata katika ngazi ya vijiji. Na serikali hiyo ya vijiji, itakuwa ikizingatia mambo kama hayo, mambo ya kusuluhisha mizozo ya ardhi katika kijiji hicho, na hata kutoa sstakabadhi za kumiliki mashamba.

Wananchi pia wamesemo kwamba kuna mizozo ya mipaka baina ya jamii tofauti, ambapo hii mizozo imesababisha umwagaji wa damu, watu wepoteza maisha yao, na kwamba mali za dhamani nyingi zimeweza kuharibiwa kwa sababu ya mizozo ya mipaka. Kwa hivyo, hilo ni swala ambalo Tume Ya kurekebisha Katiba iliweza kushugulikia jamba hilo. Na tulipoenda Transmara jana kulikuwa na maoni nyingi sana kuhusu mizozo ya mipaka, na walishawishi ya kwamba ni vizuri Katiba iweke sera fulani, ama kuweka sheria katika Katiba ya kuonyesha shida hizi za mipaka zinaweza kusuluhishwa namna gani ili shida hizo zotatuliwe mara moja. Wananchi wamelalamikia uharibifu wa ardhi. Wananchi wamesema kuna uharibifu mwangi sana, hasa ukiangalia kuna uharibifu ambao unasababishwa na hali ya nature, ama hali ya Mungu, kama vile mvua ikikosekana katika sehemu fulani basi lazima nchi hio iwe kame. Lakini pia kuna shida zingine za uharibifu wa ardhi ambazo zime sababishwa na wanandamu wenyewe, watu wamekusudia kuharibu ardhi, hasa kwa sababu ya ukataji miti. Kuna mifano kama Mau Forest ambayo iko na miti ambayo ni ya kiasili, indigenous trees, na pia ina wanyama wa aina tofauti, na kume kuwa na uharibifu, kumekuwa na ukataji miti. Katika sehemu ya Nairobi mnajua kuna Karura forest, na hizo pia zomeweswa kukatwa na binadamu, kwa hivyo tunaweza kusema ya kwamba, hizo ni sababu za kibinadamu za kuharibu ardhi.

Pia kuna upeanaji, kutoa kwa trust land, ardhi ambazo zinamilikiwa na County Councils, wananchi wamesema kwamba ardhi hizo zimebadilishwa na mabaraza ya miji na zikiwa nikama sio za wananchi tena, bali zimekuwa juu ya County Councils kuweza kupeana ardhi hizo za trust lands, na wananchi wamelalamikia jambo hilo. Wakati katika sehemu ya Kajiado, kuna sehemu Elodariak, and Mosro, sehemu ambazo ni chini ya Trust lands, na zimeanza kupeanwa na County Councils bila idhini ya jamii zilizo katika sehemu hiyo. Upande wa Narok pia, lazima mnajua kuna sehemu kama hizo ambazo zinaweza kupeanwa na wanachi wamezungumzia sana kwa kirefu na kwa uchungu juu ya kupeana ardhi bila idhini yao.

Shida ya land grabbing, shida ya unyakuaji ya mashamba, imekuwa pia ni tishio kubwa sana katika nchi hii na shida ya kuponyakuaji kwa mashamba imekua inaonekana hasa katika sehemu za miji, shida ambao ilianza kwa miaka ya 80, 1980s, ndio shida hasa unyakuaji ya mashamba imeweza kuonekana. Wananchi wamesema mali nyingi ya uma imeweza kunyakuliwa, wananchi wamesema ya kwamba, choo zimenyakuliwa, wananchi wamesema hata wanyakuaji hawa wameweza kunyakua sehemu za makaburi hata sehemu za kando kando ya barabara, ama road reserve zinaweza kunyakuliwa na watu hawa, sehemu za kuchezea fields ama playground zimenyakuliwa, na hata compounds za shule zimeweza pia kunyakuliwa. Hivyo basi kulikuwa na sera ya serikali, kuliwa na policy order ya kusema kwamba shule zote ya uma ni sharti ziwekwe upuwa ili kuzuia watu hawa wasiweze kupenya katika sehemu ambazo watoto wetu wanasomea, na wakaweza kunyakua sehemu hizo.

Pia kuna shida nyingine kuhusu ardhi, na inatokana na land policy. Kuna sera ya ardhi kinasema ya kwamba, kuna policy ya lands inaitwa willing seller, willing buyer. Kwamba wewe kama unahitaji kuza ardhi yako, na kama kuna mnunuzi ambaye

angependa kununua ardhi hiyo basi ni sawa na ni haki. Na hasa katika sehemu hizi za Narok hata sehemu sa Kajiado hasa Kajiado North, kuna hii shida saa ya hiyo policy ya willing seller na willing buyer. Kwasababu sera hii inaumiza jamii ambazo hazijui sheria zilizoko juu ya ardhi. Kwa hivyo inasemekana policy kama hii, sio ya haki. Kwa sababu wale wanaonunua mashamba ni watu ambaao wako na nguvu ya kiuchumi, na ni watu ambaao wako na elimu na wanajua haki, wanajua sheria zilizoko kuhusu ardhi, na wale ambaao wanauza ardhi ni watu ambaao hawana elimu, na ni watu hawajui haki zao kuhusu ardhi, kwa hivyo hio inachukuliwa kama ni unyakuaji wa hali ya juu, na wananchi wamesungumzia kwa uchungu sana juu ya jambo hili, na wali omba Tume ya kurekebisha Katiba iweze pia kumulikia sera ama policy kama hizo.

Shida zote ambazo zinatokana na ardhi, limesemwa ya kwamba ni kwa sababu haina sera kuhusu ardhi. Kwa wakati huu, na kwa Katiba hii ambayo tuko nayo kwa sasa ni kwamba the government does not have a land policy, na kama serikali haina sera kuhusu ardhi, basi ni lazima kuwe na shida nyingi sana kuhusu ardhi. Na dhamira ya Katiba hii, ukiangalia kutoka kipengele 232, imefafanua sera mpya kuhusu ardhi. Kwa hivyo sera ya ardhi sasa iko katika Constituion mpya, sera ya ardhi iko katika Katiba mpya ambayo wananchi wameandika na kwamba kuna mambo fulani juu ya sera ya ardhi ambaao Katiba hii imezungumzia. Ningependa kusema sera 4, ambazo ni za muhimu sana ambayo Tume ya kurekebisha Katiba iliweza kuwasikia na kwamba Katiba itahakikisha wamba kuna usawa kwa umilikaji wa ardhi, ili kila MKenya angalao aweze kupata ardhi ya kuweza kujimudu kiuchumi, kwa hivyo sera hiyo ilizungumiziwa kwa kirefu na Tume ya kurekebisha Katiba.

Jambo lingine ni uhakikisho ama security of lands rights for all land owners, kwamba kama wewe unamiliki ardhi fulani na uko na stakabadhi ya kumiliki shamba, ni sharti ya hii Katiba ilinde ardhi yako, na hata mali ambayo uko nazo ni sharti kwa hii Katiba ihakikishe ya kwamba hiyo uko na security ama uko na ulinzi kwa mali ambayo umepata pata kwa njia ya halali. Kwa hivyo Katiba hii inadhamiria kuhakikisha ya kwamba mali ambayo uko nayo, na ardhi ambayo uko nayo, na kama uko na stakabadhi ya kumiliki shamba, Katiba hii imeapa kuhakikisha italind mali ya mwananchi huyo.

Pia sera nyingine ni kuhusu utumiaji vizuri wa ardhi, ama sustainable and productive management of land. Kuna sera katika Katiba mpya kusema ya kwamba, hata kama wewe ndiyo mwenyewe na unamiliki shamba fulani, unamiliki ardhi fulani, ni sharti uitumie katika njia inayo faa, haupasi kuharibu ardhi hiyo kwa sababu ardhi hiyo itatumwa kwa vizazi na vizazi, kwa hivyo sera mpya kuhusu ardhi inahakikisha ya kwamba lazima kila mtu katika sehemu ambaao unayo miliki huwezi kutumia hiyo ardhi kwa njia unayo faa. Unapaswa kutunzwa, unapaswa kutokata ikiwezekana, unahitajika upande miti, na kuhakikisha ya kwamba, kuna mumonyoko wa udongo, ili ardhi hiyo iweze kufaa vizazi, na vizazi ambavyo vitakuja baada yako.

Pia kuna sera nyingine ya transparent and cost-effective management and administration of land. Hivyo basi kutakua na njia ya wazi ya kuweza kama unge tako kuuza ardhi, ama ungetaka kununua ardhi, ni lazime iwe inafanywa katika hali ya uwazi, kwa sababu imeonekana ya kwamba shida nyingi ambazo wa Masai wako nayo ni kwamba wanauza ardhi bila idhini ya jamii, wana uza ardhi bila mtu yejote, ama bila kuhusisha ofisi yoyote ya serikali, na inakua ni masikizano baina yake na yule mtu anae nunua ardhi. Kwa hivyo wanaenda wanaandikiana makubaliano ambazo haziwezi kukutetea katika sheria iwapo kutakuwa na

shidi kuhusu kuuza kwa ardhi yako. Kwa hivyo, kuna sera mpya ya kuhakikisha ya kwamba, ikiwa unataka kuuza ardhi yako itakuwa ni lazima ujiwashilishe katika ofisi ifatayo, ama uende katika jamii uwaeleze sababu zote zako za kutaka kuuza ardhi, waone kama sababu hizo ni za muhimu, na jamii ikiona ni kwamba kuna umuhimu wako wa kuuza ardhi, basi watahakikisha ya kwamba, itafanywe kwa njia ya haki ili kusije kukawa na shida badaye wakati mtakuja kukosana na yule ambaye ulimuuzia ardhi, kwa sababu itakua inahusisha watu zaidi ya wawili. Kwa hivyo jambo hilo la transparency in land administration ni jambo pia ambalo limezungumziwa na ni sera mpya katika Katiba hii.

Jambo lingine ningependa muone kuna kipengele cha 232, article 232 ambacho inazngumzia juu ya land ownership, na kuna tofauti kubwa sana kati ya Katiba tulio nayo hivi sasa na Katiba mpya kuhusu umilikaji wa ardhi. Katiba tunayo hivi sasa inasema ya kwamba umilikaji wa sjuu zaidi, ama milikaji wa mwisho wa ardhi ni serikali. Kwa hivyo hata wewe mwanachi ukiketi hapa na uko na sstakabadhi za kumiliki shamba, Katiba tulio nayo hivi sasa yasema ya kwamba ardhi hiyo milikaji wa mwisho ni serikali. Kwa hivyo hata ukiwa na sstakabadhi ya kumiliki shamba, bado ardhi hiyo ni ya serikali. Sehemu ambayo wewe unamiliki, ni kutoka tu mahali ambapo unaishi hadi foot 6. Lakini sehemu zozote ziko chini ya foot 6, hiyo ni ardhi ya serikali. Basi tofauti kati ya sera hiyo kuhusu umilikaji wa ardhi na Katiba mpya ya wananchi, inasema ya kwamba, ardhi yote katika jamhuri ya Kenya inamiliwi, au ni ya wananchi wa Kenya kwa ujumla, sio ya serikali, ni ya wanachi wa Kenya, either wakikaa kama jumuia, kama communities kwa sababu kuna watu wanamiliki sstakabadhi ya schemes. Kwa hivyo either ni wananchi wanaishi katika jumuia hizo ama ni ya wananchi kwa binafsi. Tunajua kwamba kuna wananchi wengine amba wako na sstakabadhi za kumiliki shamba na kuna wengine wanaishi kama katika communities ama hizo schemes kwa hivyo Katiba hii mpya inasema ya kwamba serikali haina ardhi, ardhi yote ni ya uma, ardhi yote ni ya wananchi, wakimiliki hizo shamba katika jumui, ama katika vikundi ama wakimiliki hii kama kibinafsi. Kwa hivyo hiyo ni tofauti kubwa kati ya Katiba ya sasa na Katiba mpya.

Jambo lingine, kuna sera kuhusu ardhi ni kusema ya kwamba watu wasio WaKenya non-citizens hawawezi kumiliki ardhi katika jamhuri ya Kenya. Watu wasio WaKenya hawawezi kumiliki ardhi, bali wanaweza ku-lease, wanaweza kukomboa hiyo ardhi kwa muda wa miaka 99. Mnakumbuka wananchi ya kwamba kuna makampuni fulani katika nchi hii ya Kenya na hasa katika sehemu hizo za Narok na sehemu za Kajiado, an sehemu za Transmara, kuna kampuni zingine ambazo zikona lease na miaka 999, karibu karne mzima. Kwa hivyo Tume hii ilionelea na bado inahitaji kupata maona kwa wananchi, kwa sababu Tume hii ilionelea kwamba hiyo ya watu wanaomiliki mashamba kwa miaka 999, hizo miaka zitaapunguzwa ziwe 99, iwe muda amba mtu asie MKenya wakuweza kukodesha ardhi ni miaka 99 peke yake. Na mngependa kujua na jee, makampuni, hayo au mashjirika hayo ya kigeni ambayo yako na lease ya miaka 999, mnawenza kuuliza ya kwamba mambo yao yatakuwa ni namna gani? Basi ningependa kuwaambia mfungue katika nakala zenu ukurasa wa 47, kinazngumuzia juu, ukiangalia kipengela cha 18-1, kinazngumzia juu ya kumuiliki ardhi, na inasema kwamba, natumaini wananchi mko hapo, 47, ownership of land, hicho kipengele cha mwisho, kipengele cha 18-1. Kinasema ya kwamba, baada ya kipengele kwa Katiba hii, maslahi yoyote yanao husu ardhi ambayo ni kubwa zaidi ya kipindi cha kukodesha cha miaka 99, inayoshikiliwa na mtu asiyekuwa raia, itabadilishwa kuwa kipindi cha kukodisha cha miaka 99 isipokuwa ifutiliwe mbali.

Katiba hii inasema ya kwamba watu hao ambao walikuwa wamekomboa ardhi kwa miaka 999, baada ya utekelezaji wa Katiba hii, basi miaka hizo zitapunguzwa kutoka 999 hadi 99 na hawa watu hawatalipwa sudia, hawatakuwa na compensation yoyote, hata ikiwezekana, ardhi hizo zitarudishwa kwa wananchi. Wananchi, kuhusu hizo miaka za lease, itakuwa ni juu yenu kujua kama hata 99 zinafaa ama kuna mapendekezo yoyote mnaweza kusema either mngependelea miaka hizo 99 zipunguzwe ama mungependa ziongezwe, itakuwa ni juu yenu wananchi kutoa maoni yenu boda ya mimi kumaliza kipindi kuhusu ardhi.

Sasa pia ningependa kuwapeleka katika kipengele 234, moja ambayo inahusu juu ya sehemu vile ardhi sasa imegawanywa. Katika Katiba tulionayo hivi sasa ni kwamba, ardhi imegawanywa mara tatu. Kuna ardhi ya serikali, government land, kuna trust land, ambazo hizi ni ardhi zinazo milikiwa na County Council, na private lands ama ardhi za binafsi. Lakini kwa Katiba mpya sasa, kuna migawanyiko mitatu, lakini kuna tofauti kwa sababu sasa hakuna government land, bali tuko na public land au ardhi ya uma. Kuna community land, ama ardhi ya jamii, na pia kuna private vile ilivyoko hapo awali, private land ama ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi, mtu ambaye ako na title deed, hiyo ndiyo private land ama ardhi ya binafsi. Kwa hivyo kuna umilikaji wa ardhi lakini imekuwa imegawanywa mara tatu, kuna ardhi ya uma, kuna ardhi ya jamii, na kuna ardhi ya binafsi.

Ningependa pia muone kipengele cha 234-2, ambacho kinaeleza juu ya ardhi ambayo itaitwa ni ardhi ya uma. Tunasema kwamba ardhi yoyote ambayo hivi sasa inamiliwi na wizara yoyote, ardhi yote inayomilikiwa na Ministry, kama ni Ministry of Lands ama ni Ministry of Agriculture, ardhi hiyo yote inamiliwi na wizara yoyote ya serikali ama department yoyote ya serikali, ama agency yoyote ya serikali, basi tunasema ardhi hizo zitakuwa sio za serikali tena, bali zitakuwa za uma. Pia ardhi zote ambazo baada ya kutekelezwa kwa hii Katiba, wenyewe watakuwa wametafutwa, kuna ardhi zingine ambazo ni vigumu kupata mwenyewe, na iwapo baada ya kutekelezwa kwa hii Katiba, zitanguliwe, ya kwamba ardhi hizo hazina wenyewe ama hakuna mtu atakaeku kutetea kusema ni yake, basi tunasema hizo ardhi zitakuwa pia ni za uma.

Pia mabarabara zote na sehemu za kando kando yake ama road reserves, tunasema pia hiyo ni mali ya uma. Na mito zoto, mito na ziwa zote kuu, ama lakes, pia tunasema hayo yoteyaitakuwa ni mali ya uma. Pia bahari na sehemu za kando kando wa bahari na hata sehemu za chini za bahari tumesema kwamba sehemu hizo za bahari, kama bahari ya Hindi tafadhalini, itakuwa ni sehemu ama itakuwa ni mali ya uma.

Mngependa kujua basi mali ya uma ni nani atakayekuwa akimiliki ardhi hiyo ya uma, ni nani atakaye kuwa na title deeds ya ardhi hiyo ambayo tumesema itakuwa ----

District Coordinator Ben Molel: (inaudible) District Coordinator Narok. Na siku hii ya leo ni siku muhimu sana kwetu sisi watu wa Narok, ni siku ambayo tutasikia na kusoma Draft ya Constituion , na nafikiri mmeefika hapa kwa sababu tuko na hamu sana kusikia na pengine contents ya Katiba yetu mpya. Na nifikiri sijui kama sisi wote tunaewa Kiswahili au nichanganye niongee KiMasai wengine wasikie? Kwa hivyo inaonekana tutatumia lugha ya Kiswahili, na ninatuma sisi yote tunaelewa lugha

hio. Kwa wale wenzangu ambao hawajui lugha ya Kiswahili (ianaudible) kuna wengine ambao hawajui, na tungependa masilahi yenu pia ichukuliwa. Tunataka muelewe tuwe pamoja, na hivyo ndiyo muhimu kabisa kusema, tutaongea Kiswahili tu. Ikiwa na swali ambalo hujasikia vizuri na unataka isemwe kwa ile lugha ambayo unaelewa, lugha ya mama, tuko hapa kwa ajili yenu.

(in *KiMasai*)-----

Ndiyo basi ningependa kusema hata hawa wenzangu wajue ya kwamba kunao watu ambao hata pengine tukisome tukiongea Kiswahili throughout, hawatajua kabisa, hapo atapotea njiani, na hatutaki mtu moja apotee. Tunataka kila mtu awe na sisi, tukisoma Draft. Na tumekuja hapa kuangalia tu mambo ya Draft, hatuna agenda ingine. Ukiwa na swali lolote, uhakikisha inahusu Draft. Na ukiwa na jambo la kusema, tafadhali usitoke nje ya Draft hii. Nikienda kumalizia tukiwa nafasi hii, ningependa tu ku-introduce our officers kutoka headquarters (CKRC) ambao ndiyo watatuendesha, na kutupeleka through the Draft. Inaonekana tunaweza kukaa hapa mpaka jioni kabisa, lakini tukae na tupate draft yenyewe lile jambo tumekuja kilifanya.

Kwa hivyo hapa karibu nami, niko na Bwana George, ambaye pia ametoka ofisi headquarters, na hapo ni Maurice, ambaye naye pia ametoka huko. Maurice Ole laria, ametoka Kajiado. Ninatumaini watatupeleka na ninawapatia programme watuendeshe tuende through the Draft.

George Nakholi: Kabla sijapatia nafasi mwenzangu bwana Raria, nataka kuchukua nafasi hii kuwakaribisha kwa niaba ya Constituion Review Commission, hapa Narok County Coucil hall, na nimeseme ya kwamba tutakuwa pamoja kwa siku nzima ili tuangalie yale mambo mlikuwa mumepeana kwa maoni, ambayo yaliangaliwa na Commission, na sasa ni wakati tumerudi, na hayo mambo mlikuwa mumeopana, au maoni mlikiwa mmepeana, tuyachambue na kuangalia kitu gani kilikosekana. Na kama kuna jambo lolote ambalo mlikosa au mmeona haliko kwa hio Draft Constituion , tafadhali utakuja mbele baada ya sisi ku zungumza, na kusema kama una jambo lolote ambalo unataka ufanولي au liongezwe.

Pia unaweza, baada ya leo, kama una muhimu unaona unataka kuongeza, unaweza kuandika na umpatia District Coordinator, ambaye utalileta kwa Commission offices kabla tarehe 22, kwa sababu wakati huo ndio Commissioners watakan tena waangalie haya mambo mengine kutoka kwa constituencies hizi 210, zote za hapa Kenya, Narok North ikiwa pamoja na hizi constituencies. Kwa hivyo, mabibi na mabwana tunawakaribisha sana hapa, tuangalia mswada huu, tuangalia mambo gani ambayo yako, halafu tunaweza kuongeza yale mnayo. Mnaweza kusema hapa tutakuwa tuna-record kilakitu hapa, kuna chombo cha kunasa hayo mambo, na pia tutakuwa tunaandika, na ukikosa uandike upatie District Coordinator alete. Pia, mkiangalia kwa gazeti la jana, mtaona kwamba kuna watu watatu kutoka Narok District, ambao ni delegates, wataenda huko Nairobi, wataanza mkutano tarehe 28 mwezi huu. Sasa hao watatu nataka kujua kama wako hapa, itakuwa bahati sana. Labda kama wako hapa wasimame tu, tuwaone. (Inaudible), District Coordinator ananiambia. Sasa walikuwa wawe watatu, na mmoja wawo lazima awe mama. Kuna bahati naona mama akisimama, na nikushukuru sana watu wa Narok kwa kufanya vile inatakikana na Constituion .

Kwa hivyo hao wenyewe wako hapa wasikize kabisa kwa makini yale mambo watu wa Narok North watatoa. Juzi tulikuwa Narok South, na jana tulikuwa huko Kilgoris, na leo tuko hapa. Tulikuwa tumemaliza Kajiado hapo zamani. Kwa hivyo nataka mtoe maoni hawa wasikize, wakienda huko tarehe 28, nafikiri hata inatakana tarehe 24 waende Bomas of Kenya, lakini mkutano wakina nani watakuwa wanaingiza mambo ya watu wao vile watasikiza leo. Kwa hivyo sina mengi, nasema tu tuwe na mkutano wa amani, tu malize mambo yetu, halafu tupeleke report huko ofisi yetu. Sasa nitapatia mwenzangu Bwana Raria aanze na sikizeni kabisa vile anazungumza. Bwana Raria.

Maurice Kepoi Raria: Asante sana Bwana Nakholi, na pia ningependa kushukuru wananchi wa Narok ambao wamekuja katika hii hall. na ningependa tu kurudia kwa lugha ya KiMasai yale mambo ambao kusudi wale wenzetu hawalewi hiyo lugha wapate pia kusaidika.

In KiMasai--

Basi bila kupoteza wakati, ningependa kuwanza kuwapeleka moja kwa moja hadi kwenya Katiba ili tuone mambo muhimu sana. Kwa kusema kweli hatuwezi kumaliza mambo yote yalio katika Katiba hiyo, kwa sababu tukijaribu kufanya hivyo itatuchukua mda mrefu sana. Tukijaribu kujadiliana kutoka kipengele cha kwanza hadi cha mwisho hata nafikiri siku mbili haitatutosha. Kwa hivyo tutajaribu kuzungumzia yale maneno ambao yana tuhusu kwa sana. Hasa mambo ya ardhi ni jambo ambalo linatatiza hasa weatu wa eneo ya Masaini sehemu ya kajiado sehemu ya Narok, sehemu ya Transmara, tumesikia vilio sana kuhusu ardhi. Na kwamba Wamasai wamesema ya kwamba iwapo mambo ya ardhi hayata nukuliwa vizuri katika Katiba, basi wao hawatakuwa wamepata uhuru kwa sababu kwa wa-Masai Katiba ni juu ya ardhi. Kwa hivyo tutatia mkazo mambo ya ardhi pia pamoja na usambazaji ya utawala, ama devolution, kuleta utawala kutoka chuu, hadi kwa mashinani, kwa mikono ya wananchi, kwa hivyo hayo ni baadhi ya mambo ambayo tutatilia mkaso sana kwa sababu hapa kwa report, ama kwa maoni ambayo wananchi wa sehemu hii walitoa walipatia umuhimu sehemu hizo mbili.

Translation in Kimasai:

Ningependa hata kuanza kuwambia juu ya Katiba kwa sababu kuna wananchi wengine ambao hata sasa bado hawaja elewa Katiba ni kitu gani. Hii ni kwa sababu Katiba tulionayo hivi sasa Katiba ambayo ilitengenezwa kwa nchi ya Lancaster kule Uingereza, hata Katiba hiyo ilipo patikana wananchi hawakuhusishwa na hata baada ya kutunga, ama baada ya kutunga Katiba hiyo, wananchi hawakupewa nafasi yakuweza kusoma. Nina hakika wengi wengi watakubaliana na mimi kwamba ni watu wachache tu wamewahi kusoma Katiba tulionayo hivi sasa. Hii ni kwa sababu imekuwa hata mambo ya muhimu kama Katiba, haijawekwa kwa wananchi, kwa hivyo wananchi wamekuwa katika gizani, hawaelewii haki zao, na ndiyo sasa dhamira ya Katiba mpya ni kuhakikisha ya kwamba wananchi wanaelimika, wananchi wanajua Katiba yao, na ndio sababu hata hivi sasa kila mwananchi aliye katika ukumbi huu ako na makala ama ako na copy yake ya Katiba, na pia hivi karibuni mtapata pia nakala katika lugha ya Kiswali, na hata kuna matokeo ya kwamba Katiba ya wakati huu, Katiba mpya ambayo tunadhaminia

kuwa nayo, itaweza pia kubadilishwa katika lugha za mama ili wananchi wote wa Kenya wapate kujua kwa lugha wanao elewa zaidi, waweze kujua haki yao katika Katiba.

Basi Katiba tumesema kwamba ni mkataba wa masikizano, na sema Katiba ni mkataba wa mazikizano, kwa sababu wananchi wa sehemu ambao watu wanoishi katika sehemu wanao ita nchi yao, ni lazima waketi na watunge sheria ambazo zitawasaidia katika maisha yao wa kila siku. Kwa hivyo hiyo kutokana na hayo masikizano, ndio wananchi wanatoa Katiba ambayo itawasaidia katika mambo yao ya kila siku, ndio sababu ninahita ni mkataba tu wa masikizano.

Katiba pia ikiwa ni mkataba wa masikizano, ni lazima na ni sharti Katiba iweze kufutia vizazi na vizazi vijavyo ikitumia lugha ya wakati ule. Tunasema ni kwamba ni lazima Katiba ya nchi, Katiba ya wananchi ni lazima imulike mambo muhimu katika jamii hiyo na iweze kuvutia vizazi na vizazi, isiwe Katiba inavutia tu vizazi vyta wakati ule, bali Katiba inahitajika itumike kwa miaka na miaka. Basi tunasema, ni lazima Katiba itumie lugha ambayo inatumiwa na watu katika wakati huo. Tukijaribu kuangalia Katiba tulionayo hivi sasa na Katiba mpya tofauti kubwa sana ni kwamba, Katiba ya sasa imetumia lugha ambayo ni rahisi, na wananchi wao wenyewe walisema ya kwamba hatutaki Katiba ambayo imeandikwa kwa lugha ya hali ya juu sana ya kisheria, kwa sababu Katiba sio ya wana sheria, bali inapaswa kuwa ni ya wananchi. Kwa hivyo ukiangalia Katiba ya sasa imetumia lugha rahisi sana kwa kiingereza na hata kwa Kiswahili. Lugha ile Katiba imetumia, ni lugha ambayo hata nyinyi wananchi lugha ambayo mnasoma kila siku katika magazeti, ni lugha ambayo mnasoma katika Bibilia, kwa hivyo tunaseme ile lugha imetumiwa katika Katiba hii ni lugha ya wananchi.

Jambo lingine ningependa kuwaambia ni kwamba nimesema hapo awali kwamba Katiba haiwezi kunakili shida zote ambazo mlimtoa. Kuna shida nyingi ambazo wananchi walilalamikia, na waliitisha Tume ya Katiba iweze kurekebisha mambo hayo. Tunasema ya kwamba' Katiba yetu haingeweza kunakili shida hizo zote, bali imejaribu kumulika mambo ambazo muhimu ya kimsingi katika jamii. Wananchi kwa kusema kweli, hata watalam wa Katiba wamesema ya kwamba, Katiba yetu mpya ni kati ya Katiba ambazo ziko na kurasa nying sana duniani kwa wakati huu, kwa sababu imemulikia mambo mengine ambayo hayako katika Katiba zingine. Hata Katiba kongwe kama ile ya Americani, sio kubwa kama Katiba yetu mpya kwa sababu hapa tuko na kurasa ama tuko na chapters inayo husu mazingira, environment and natural resources, na Katiba ya Americani ambayo ni kongwe haijaguzia mambo kama hayo. Kwa hivyo wataalam wa Katiba wamesema kwamba Katiba mpya, ambao wananchi wa Kenya wanadhaminia kuijandikia, imeguzia mambo mengi sana ya ki msingi ya maisha.

Jambo lingine ni kwamba ningependa kuwaambia kifupi historia ya Katiba yetu. Ukiutaribu kuangalia tangu wakati wa Lancaster hadi sasa, tunaweza kusema Katiba ya sasa iko na miaka 39, na Katiba hii imebadilishwa mara 30. Nikijaribu kuifananisha na Katiba ya nchi ya Americani ambaye ni kati ya Katiba kongwe sana duniani, Katiba ya Americani iko na miaka 200. Na Katiba hiyo ya America, imebadilishwa mara 20 peke yake. Wananchi ningependa muona tofauti hiyo kati ya Katiba yetu changa ambayo iko na miaka 39, imebadilishwa mara 30, na Katiba ya America ambaye iko na miaka 200 na imewahi tu kubadilishwa mara 20 peke yake. Hivyo basi, inaonekana kwamba ni kama kwamba, kila mwaka Katiba yetu ya Lancaster

hubadilishwa kila mwaka. Basi yaelekea kusema kwamba ubadilishji wa Katiba kwa mara kwa mara, ni duihirisho ya kwamba hata msingi ya kuandika ile Katiba haikuwa ni msingi ya thabiti. Ikiwa kila mara Katiba inabadilishwa, basi inaonekana ya kwamba, inadhihirisha ya kwamba basi hiyo Katiba hata mara ya kwanza haikuwa ina msingi katika wananchi, iko na kasoro.

Ndio sababu wananchi wa Kenya walipata msisifuko wakasema ni vyema sana wakati huu tupate Katiba ambayo inajumuisha wananchi wote, na ni Katiba ambayo itakaa kwa vizazi hata bila kubadilishwa. Kwa sababu Katiba iliyo bora ni ile inayo aangaza mambo muhimu ya kimsingi katika jamii. Na ukiangalia Katiba kukonao hivi sasa, kuna maneno mengi ambayo imezungumzia, lakini ningependa tu kuwaeleza kwa ufupi, mambo muhimu ambavyo Katiba hii imezungumzia. Ningependa tu kuwapatia vipengele muhimu sana, ambayo hii Katiba imizingatia. Kati ya mambo hayo Katiba imezungumzia juu ya umoja wa kitaifa, imezungumzia juu ya kutambua utamaduni wetu, Katiba hii imizingatia sana mambo ya democracia na wajibukaji. Katiba pia imezungumzia juu ya kuheshimu watu wote, akinamama, wazee, watu walemavu, watoto, na watu wakongwe. Katiba hii inazingatia kuheshimu kila mmoja.

Jambo lingine ambalo Katiba hii imetilia mkazo sana ni mambo ya ufisadi ambayo imeaminika ya kwamba kwa kusema kweli ufisadi umekuwa ni jambo ambalo limevunja utu wa mgongo wa nchi yetu, kwa hivyo Katiba hii pia imezungumzia mambo kuhusu ufisadi. Pia mambo ya kujumuisha wote katika watu wote, katika maendeleo ya taifa, mambo ya kujumuisha watu wote, imesungumziwa katika Katiba hii. Katiba hii pia imejumuisha mambo wa uongozi bora ugawaji sawa wa rasilmali. Wananchi wamesema ya kwamba Kenya iko na rasilmali za kutosha, lakini shida ilioko ni kwamba hakua usawa wa ugawaji wa rasilmali, kwa sababu rasilmai nydingi iko kwa mikono ya watu wachache, na rasilmali kidogo ndiyo iko katika mikono ya wananchi wengi. Kwa hivyo wananchi wamelalamikia mambo hilo na Katiba hii pia imengatia kwa kirefu.

Jambo lingine ni juu ya haki za kimsingi, kuna haki ambazo mwanchi anapaswa kujua, na wakati tutaenda kuangalia tukiendelea tutaona haki za akina mama, tutaona haki za watoto, tutaona haki za wati walio fungwa, tutaona haki za watu walemavu na haki za watu tofauti wanoishi katika jamii, kwa hivyo Katiba hii imejaribu kugusia haki za watu wote katika jamii. Kwa hivyo, kwa ufupi, hayo ndio mambo ambao Katiba hii, nimewapatia tumu mukhtasari kwa mambo yale ambayo Katiba hii imezungumzia kwa sababu bado tungali tutazungumzia kila kipengele kwa kirefu.

Ningependa tu kuwambia mfungo hizo katika hizo nakala zenu ningependa kuwaonyesha, ningependa tuanzie kwa utangulizi ama preamble, kwa hivyo wananchi ningewaomba muende pale, ili tujue hasa, ningewaomba mfungue ukurusa hiyo ili muone, uko na swali? Wananchi nimewaomba tu tafadhali mfungue makala zenu ili tuone utangulizi, ama preamble. Wakati Makomishona walipokuwa wakizunguka katika nchi hii kuchukua maoni, wakati Makomishona walipokuwa wakienda kuchukua maoni ya wananchi, wananchi walisema kwamba ni vizuri Katiba yetu iwe na uangulizi. Na utangulizi wa Katiba yetu, imezungumzia mambo tofauti ni fupi, lakini umezungumzia mambo muhimu sana katika jamii, mambo ambayo ndiyo yanafanya jamii kuwa ni moja. Mkiangalia utangulizi unaeleza WaKenya ni kina nani? Ukiangalia inaanza kusema sisi ni wanachi WaKenya, ukiangalia Katiba tulionao hivi sasa haizungumzii juu ya WaKenya kusema ni kina nani? Imeanza tu kusema

kwamba Kenya ni nchi huru. Lakini Katiba hii inadhaminia kuanza kwa msingi kabisa kuonyesha wa Kenya ni kina nani. Kwa hivyo nasema wananchi wa Kenya tukifahamu tofauti zetu za kikabila, kitamaduni, na kidini, na tukidhaminia kuishi kwa amani na umoja kama taifa moja huru lisilogamka. Hivyo basi mwongozo huu, ama utangulizi huu wasema ya kwamba sisi ni watu wa Kenya, na kwamba tunatambua kwamba kuna tofauti katika jamii ya Kenya, tuko na makabila tofauti katika nchi ya Kenya, hata namini hapa Narok, na nina amini hata ndani ya hii hall, kuna wananchi wa makabila mbali mbali. Pia WaKenya wako na tofauti za hisia za kidini, kuna, tunajua, tukona wa

Wakristo, tukona Waislamu, na watu wa dini zingine mbali mbali. Kwa hivyo, utangulizi huu unatambua kwamba sisi ni WaKenya naam. Lakini tunatambua pia kwamba tuko na hizo tofauti. Na pia utamaduni zetu in tofauti kabisa.

Lakini licha la hizo tofauti utangulizi huu unasema ya kwamba tunadhaminia kuishi katika hali ya umoja, tunadhaminia kuishi katika hali ya umoja, katika taifa hili moja la Kenya ambalo haliwezi kugawika. Utangulizi huo huo unaeleza juu ya wa Kenya, na kueleza tofauti zao, na nia ya watu wa Kenya kutambua ya kuamba ijapokuwa tuko na hizo tofauti, sisi bado tutaishi katika taifa moja, isilogawika. Pia mambo mengine ambayo utangulizi huu umemulikia ni kwamba Katiba hii itadhaminia kuweko na usawa katika watu wote katika jamii. Kuwe na usawa kati ya akina mama na wazee kulinda watu wote katika jamii katika hali ya usawa na zaidi ya yote wananchi. /// Katiba hii mkiangalia huu utangulizie intambua Mwenyezi Mungu kwa sababu wananchi walisema wananchi wa Kenya ni watu ambao wanaamini Mungu, na ni vizuri s ana utangulizi uweze kuweka kipengele katika utangulizi, ya kuonyesha ya kwamba, watu wa Kenya wanaamini Mungu, na ni sharti iweko katika utangulizi. Basi mkiona pale chini, baada utangulizi kuna sentensi moja inayosema Mungu ibaraiki Kenya. Ni kwa sababu wananchi wa tabaka mbali mbali katika jamhuri walisema kwamba sisi ni watu tunaoabudu Mungu na ni sharti tumuweke mbele kwa sababu yeye ndiye hasa chanzo cha kuweko kwa nchi hii, na chanzo cha kuweko kwa maisha yetu, kwa hivyo utangulizi huo mumeona ya kwamba tume wahi kumpatia Mungu ucheo wa mbele. Kwa hivyo wananchi kwa ufupi, nilikuwa ninataka kuwapatia huo mukhtasari na huo msingi wa Katiba, kusudi tukiendelea kuongea juu ya mambo mengine, ama vipengele muhimu muwe angalao mnajua msingi wa Katiba yetu.

Kama kuna mtu ako na swali hapo, mimi ningefurahia, mimi pamoja na wenzangu hapa, tungefurahia kujibu na kama hakuna swali kuhusu utangulizi, ama kuhusu mukhtasari huo wa Katiba, basi ningependelea kwenda kuzungumzia mambo ya ya ardhi.

Kwa hivyo kama-----

Speaker: Inyoroshwe kabisa! Kwa sababu ya hiyo basi sasa tunashindwa. Unashindwa hii ni Narok, hii ni Nakuru, inaendaje? Hizi corner, corner hizi, tunataka zinyoroshwe. Inatakikana mweke kwa hiyo review hicho kitu kinyoroshwe.

Kitu kingine ni grabbing of land. Wale watu ambao wamenyakua mashamba ya Wamaasai, imekuwa ni wakubwa hapa. Mtu analetwa kutoka kwao anakuja kuwasimamia na kuwachunga Wamaasai, halafu yeye anakuja ku-grab. Sana, sana officers wa serikali ndio wana-grab. Unakuta mahali tumetenga, tumetanga mahali ya kupanda miti, wanaweka nyumba ya gorofa, wana-grab. Na D.C. ndiye anasimamia kwa sababu ndiye Chairman wa Town fulani, ndiye Chairman wa kupeana plot.

Tunataka plots ziwe zinasimamiwa na watu wenyewe na chairman awe ni mmoja wa Wamaasai ambaye tumemchagua sisi wenyewe. Kwa sababu tunashida sana, tumetatizika hapa zaidi.

Kitu kingine ni forests. Mambo ya forests mlisema zingine zinasimamiwa na County Councils na zingine zinasimamiwa na serikali. Tunataka hizi forests zirudi kwa wenyewe, kwa sababu hata County Councils siku hizi hatuwaamini. Wengine wanunuliwa tu, na kwingine watu wengine wanaingia tu halafu unakuta D.C. pia ndio member kwa mambo ya forests. Anawezaje kuwakataza watu na labda analeta ndugu yake kutoka pale. Hatutaki hiyo pia, tunataka forests zirudi kwa wenyewe. Wamaasai wenyewe wachunge hizo forests zao.

Kuna kitu kimeongewa hapa na ni kitu cha ajabu sana. Haya mashamba ya Naivasha, Wamaasai kutoka area hii yote wanapita Naivasha, hakuna mtu mwagine pale. Lakini Wazungu wameenda kufunga, na wakubwa wengine Waafrika, ambao wamekuwa wazungu weusi, wamefunga njia hakuna sasa njia mahali watu wanaweza kupita wakiapeleka ng'ombe wao kunywa maji. Na hakuna mtu, na wanasema kuna mtu. Na serikali haijatupatia maji ya kunywa. Tunaomba kuwa pia hizo njia zifunguliwe ili ng'ombe wa Kimaasai waende kulishwa Naivasha kwa vile hapo ndipo pahali kuna maji katika area hii yote, vile mzee mmoja aliongea hapa, Councillor. Kwa hivyo kwa hiyo tunataka kuweka mkazo kuwa njia za maji zifunguliwe. Asante sana.

Kepoi Raria: Kumiliki shamba kwa niaba ya uma, kwamba the national land commission will hold the title to public land in trust for use by the people of Kenya. Basi tunasema kuwa umilikaji ama national land commission ambayo itabuniwa ndiyo itaweza kuwa na stabakathi za umuliki kwa mashamba ambayo tumesema yatakua yainaitwa ardhi ya uma. Na community land ama ardhi ya jamii mtapata katika kipengele cha mia mbili thelatini na nne, tatu, inasema kwamba ardhi zote ambazo sasa ziko chini ya County Council hizo trust lands basi hizo trust lands, wananchi ningependa kuwaelezea hazitakuwa tena chini ya County Council, bali zitarudishiwa jamii.

Ranches zote ama ardhi zinazomilikiwa na jumia, ranches pia zitarudishiwa jamii. Na ardhi zozote zinazotumiwa na jamii ambazo hivi sasa ni gazetted land, ardhi hizo ambazo zinatumwi na jamii kwa malisho ya mifugo yao, ama kwa sababu ni chemi chemi za maji, hizo sehemu pia zitarudishiwa jamii. Kwa mfano, kuna sehemu ambazo ni gazetted katika sehemu ya Kajiado, Namanga hills ambayo hiko katika mpaka ya Kenya na Tanzania, milima hizo za Namanga ni gazetted lakini wananchi huwa wanapeleka mifugo yao kule wakati wa kiangazi kwa sababu ya malisho. Na basi wananchi wa sehemu hiyo walilalamikia wakasema ni vizuri ardhi hiyo iweze kumilikiwa na jamii kwa sababu walikua wakitumia kutoka jadi kwa sababu ya kulisha mifugo yao na hata kupata maji. Kwa hivyo ardhi hizo ambazo ziko gazetted na zinatumwi na community, ardhi ambazo ziko katika sehemu ambazo jamii zinaishi. Basi hizo adthi ama sehemu ambazo kuna chemi chemi za maji zilizo pale basi zitarudi katika jamii.

Mngependa pia kujua ni nani atamiliki sehemu hizo? Ni nani atamiliki ardhi ya jamii? Na tumsema ya kwamba ukiangalia katika

kipengele cha 235 –2A, juu ya tenure ama umilikaji, inasema ya kwamba baada ya jamii iliomiliki mali hizo, kukijulikana jamii ambayo ni hasa wamilikaji wa halali wa sehemu hiyo, baada ya kutambulikana basi hiyo jamii ndio inaweza kumiliki arthi hiyo ambayo ni ya jamii. Pia tunasema ya kwamba, baada ya kutambulikana wenyeji wa asili wa sehemu hizo ambazo ni gazetted, baada ya wenyeji wa asili kutambulikana basi Serikali itaweza kuhakikisha ya kwamba sehemu hizo ama sehemu zingine kama za streams. Serikali basi itaweza kuenda mbele na kuhakikisha kuwa sehemu hizo zitagawanyiwa wananchi, zitafanyiwa demarcation na wananchi ama jaami ambao ndio wenyewe wa asili wa sehemu hiyo, Serikali itahakikisha ya kuwa sehemu itapewa wananchi na wapewe stakabadhi za kumiliki shamba.

Jambo lingine kuhusu ardhi ya jamii ni kwamba, Katiba hii itaadhimia kutoa sheria kali sana kuhakikisha kwamba ardhi ambayo inamilikiwa na jamii ama community land, kama vile schemes Katiba hii itatoa sheria kali kuhakikisha ya kwamba hakutakuwa na watu watakao tumia sheria yejote ama kuja pamoja na kuuza sehemu ya arthi ya jamii hiyo bila kueleza members na hii ni shida hasa jamii wamelalamikia juu ya schemes, wanasema kwamba katika scheme wale officials wamekuwa wakienda wakifanya makitaba na makampuni fulani ama na watu fulani binafsi kutoka nje na kuenda kuuza arthi hii ya jamii bila kuwasilisha ama bila idhini ya members wa scheme hiyo. Na kwamba wananchi wamesema ni lazima kuwe na sheria kali sana kama kuna community land ambayo stakabathi ya kumiliki shamba inashilikiwa kwa jumla, na ili watu wachache wasiweze kutumia ujanja wao ama kutumia mali yao kuweza kuuza ama kupeana arthi ya jamii.

Tumezungumzia pia juu ya ardhi ya binafsi na hii mnaelewa vizuri kwa sababu ni hile ardhi ambayo wewe uko na tittle deed na uko na stakabathi ya kumiliki shamba, tumezema private land ama ardhi ya binafsi ni ile ambayo unashikilia tittle deed na Katiba hii imeathimia kuhakikisha ya kwamba bado tu wewe ndiye utashikilia tittle deed yako ni ardhi yako na ni haki yako, iwapo umepata arthi hiyo kwa njia ya halali. Katiba hii insema ya kwamba mali yote ambayo umepata kwa njia ya halali ama ardhi ambayo unamiliki hivi sasa kwa njia ya halali, Katiba hii inaadhimia kukulinda wewe mwananchi kama mali hizo umeyapata kwa njia ya halali. Lakini pia Katiba hii inasema kwamba kuna watu wengine ama kuna mashirika mengine katika sehemu ambazo jamii zingine zinaishi ambao wamepata ama wamemiliki arthi, na wako na stakabathi ya kumiliki mashamba na hawakumiliki arthi hizo kwa njia ya halali. Katiba hii inasema za kwamba ikiwa kuna ardhi yoyote ya jamii, ambayo imemilikiwa kwa njia ambayo jamii hiyo inaona si ya haki, kwa sababu wao hawa kuhusishwa kwa uuzaaji wa ardhi hiyo, ama kwa upeanaji wa ardhi hiyo Katiba hii inaadhimia ya kuwa ardhi hizo ambazo zimepeanwa kwa njia isiofaa kulingana na jamii ambazo wanaishi katika sehemu hiyo. Basi Katiba haitalinda tittle deeds kama hizo. Kwa sababu Katiba hii imesema kwa wazi ya kwamba ni lazima kuwe na umilikaji wa haki na itakuwa ni jua ya hii Katiba ya mwananchi kulinda mwananchi ambaye amepata mali yote kwa njia ya halali, lakini kama kuna mali yoyote ambayo umepata kwa njia isiofaa, kama basi lazima kuwe na hatua kali ya Katiba hii itaenda kutekeleza juu ya umilikaji huo.

Hapo chini utakuta Legislation ama sheria ambazo Bunge zitapitisha, baada ya miaka miwili na baada ya Katiba hii kutekelezwa, Bunge litatakiwa kati ya miaka miwili kuja na sheria za kuweza kushughulikia shida zote ambazo zinahusu ardhi. Kwa sababu kuna mambo ambazo wananchi wamezungumzia juu yao, hasa kuna mambo ya illegal land allocations ama ardhi

ambazo zimetolewa kwa njia ambazo isiofaa. Na pia kuna historical claims, kwa mfano Wamasai wamelalamikia sana juu ya ardhi zao ambazo zimechukuliwa na wakoloni na hata baada ya uhuru, ardhi hizo hazikurudishiwa wenyewe, ni watu wengine waliweza kunyakua hizo ardhi. Basi Bunge limepewa muda wa miaka tu, miwili na waweze kuja na suluhisho la kudumu kuhakikisha hizo historical land claims, ardhi ambayo ilinyakuliwa kwa njia isiofaa, ardhi za jamii ambayo ilinyakuliwa kwa njia ambayo haikuhusihama ambayo haikuwa na ithini ya uwingi wa jamii, ni lazima Bunge likuje na suluhisho la kudumu juu ya hiyo na iwapo kuna ardhi yoyote ambayo ilipeanwa kwa njia isiofaa, basi ni sharti Bunge kuja na sheria ambazo zitashugulikia malalamishi hayo ya illegal allocation na pia historical land claims.

Kwa hivyo, wananchi ningependa kusimama hapo kwa sababu na jua mngependa kuchangia sana na tunawakaribisha muwe huru mtoe maono yenu nasi tutaenda ku nakili na kupeleka katika Commission.

George Nakholi: Basi asante sana Bwana Raria kwa hayo ambayo umeyasema. Ninajua mtakuwa na mambo mengi ya kuchangisha na mna karibishwa kwa sababu huu ndio wakati, mchangishe vile mnaweza tutawapitia uhuru wote kwa sababu tunataka hii ingie katika Constitution. Kwa hivyo tutaanza na mzee, mtakuja upande huu useme jina lako halafu uluuze swali kwa sababu tunarekodi.

Shadrack Olerotike: Na isipotoka Nairobi mimi naitwa Councillor Shadrack Olerotike. Mambo ambayo nitazungumzia ni hii agenda ya tribal clashes. Kwa sababu katika Masaini ardhi ndio kitu ya muhimu sana na ndio tunashida sana. Ningeanza hivi; kwanza sheria ilioko kwa wakati huu. Wakati wa land adjudication process, kuna pahali ambaio inafika inakua mbaya, wakati wa arbitration board, mtu mmoja ndio anafanya kesi, land adjudication Officer. Hiyo iondolewe itafutiwe kamati, maana mtu mmoja anaweza kuhongwa anaweza kupendelea. Sehemu ya pili ni kesi ya Minister ambaye ndio inakuja baada ya hiyo na Minister hawezikufanya kesi zote za Kenya. Inafanywa na DC, hapo imetukanwa na corruption inaingia mapendeleo hapo. Ziondolewe section hizo ambazo mtu mmoja ndio anafanya kesi iwe community elder's ambayo wanaelewa sehemu ambaye hiyo shamba hiko maana madaraka hayo yametumiwa vibaya.

Vile vile, tukija nimesikiza sana hii sheria ya trust land act, hii two hundred eighty eight mashamba yale ambayo yalikuwa yanamilikiwa na mabaraza ya wilaya, mimi ningeonelea hivi kama Mau forest kwa mfano ama mengine, yarudi kwa wananchi sio kwa land commission, mimi napinga land commission. Land commission ni mbaya hata kuliko Serikali. Hiyo irudishiwe kwa wenyewe itengenezewa kitu kinaitwa trust, trust ya hiyo community. Kama ni ya Taita, trust ya Wataita. Kama ni Kakamega, trust ya Waluhyia. Kama ni Masaai, trust ya Wamaasai. Kwa sababu hii land commission ilikuwanga hapa mbele ya ukoloni, natakuuliza hii swali wakati wazungu waliporudi ni mashamba gani walirudishiwa Wamasai? Hakuna. Mambo ya hii lease 999, years nakubaliana iwe reduced iwe hata 33. Kwa sababu leo hii katika Magadi, mnajua kampuni ya magadi soda baraza la Kajiado hailipati hata ndururu na ni 999 years. Hiyo ivunjwe iwe 33 years, kwa hiyo foreign company na kila kitu.

Haya nikiwa hapo, kuna agreement ambayo inahusu sisi Wamasai hile ya Laikipia, ya 1904 itakwisha 2004 nasikia sasa watu

wanakimbia juu chini Kenya wakitaka kunuanua wasinunue ni yetu, na ikiisha hiyo maana ya agreement iliku ya miaka mia moja, na itaisha the year 2004. Parliament.....(interjection inaudible) usiongee kwa niaba yangu. Naomba hiyo kama typical example, Laikipia ilikuwa ya Wamaasai mashamba yote yameenda Narok, Eldoret, Nakuru wapi mpaka(inaudible) hii hapa. Tunataka hile ikilisha isiende kwa land commission, irudi kwa original owners ambayo ni WamAsasi. Kwa hivyo, ningependa kusema maneno ya mashamba yaitolewe kwa county council, isiende kwa land commission irudi kwa wenyeve straightaway. Mambo haya ya tittle deed nimefahamishwa wakati nilikua nasikiza ya kwamba hata kama una tittle deed ni futi sita tu ndio yako, chini sio yako kama shamba ni yangu iwe yangu mpaka ndani ya bahari. Sijui kama mnaelewa vile ninasema? Nimesikia ya kwamba.

(Interjection) **Rario:** Wacha kwanza, ningependa kuwaeleza vizuri sana juu ya sehemu ambayo unapaswa kumiliki. Ikiwa unamiliki sehemu yejote ya ardhi, nilikua nimesema kwa Katiba ilioko sasa hivi wewe mwananchi unapaswa tu, kumiliki mahali unapoishi hadi futi sita, na hiyo ardhi nyingine inakuwa ni ya Serikali. Lakini tunasema kwa Katiba mpya, mwananchi unapaswa kumiliki ardhi hiyo, hadi jina zilizo huko chini ardhi hiyo yote itakuwa yako hata ikiwa na madini itakuwa yako. Lakini Serikali ningependa ku-clarify hii, ya kwamba Serikali wako na haki ya kupata hile ardhi lakini lazima kama kuna minerals inasemekana ni ya Serikali, ni lazima basi Serikali iongee na mwenyeve na kuwe na fidhiya ya kutosha. Lakini ardhi yote ambaa unaishii na hata sehemu ya juu itakuwa ni ya mwananchi.

Shadrack Olerotike: Hile ilikuwa inafuatilia ni hii nimeelewa sawa sawa ardhi hiyo yangu na kama kuna madini au mafuta Serikali iongee na mwenye hiyo ardthi. Sio kunyakua maana wakati huu Serikali ina uwezo ya wanatumia kitu inaitwa land acquitation act. Kwanza hiyo land acquituation act ya Serikali kusema tunataka hapa wachukue iondoke. Kuna mashamba katika Narok ambayo title deeds zimetolewa kwa njia isio ya haki. Watu wanakaa kwa meza wanachora wanaenda kwa commissioner of lands wanatumia pesa, tittle deed inatoka. Mashamba hayo yako katika Narok, labda mwenzangu ametaja. Mfano kuna ngareta isipokua singetaka kutaja kwa sababu kuna kesi hiko kortini, okay kuna ngareta na kuna olkiongo, katika Mara iangaliwe hapo ijulikane maana kuna registration of land sheria ilifuatwa? Kama bado haijafuatwa iwe revoked na Ngarauwene na Mauwa forest ambaa inaingiliwa, title deed inatolewa bila wenyeve kujua hakuna nini, unatoa title halafu unaenda kutafuta shamba na sheria ya sasa inasema unapewa shamba on the ground halafu unaenda kuleta title siku hizi title inakuja mbele ya shamba hata unabeba karatasi na haujui shamba yako hiko wapi.

Kwa hivyo katika Narok, napeana tu examples(inaudible) kwa hivyo katika Narok, kuna many examples those are just a few out of many and I hope I'm protected by the law? Thank you, basi ningependa vile vile kusema mambo haya ya kurudisha mambo ya ardhi Parliament baada ya two years, Parliament ni mbali sana kwanini isitolewe district councils? Kila district, iwe na County Council inasema Council of elders ambaa wanaangalia mambo ya mashamba ya hiyo jamii, mito na kila kitu. Kwa sababu Bunge hiko mbali na kuna kitui inaitwa manipulation na chochote cha weza kutokea basi kwa hivyo katika mambo ya ardhi ili nisichukue nafasi ya wengine mimi naonelea Serikali isi own any land ipatie communities. Kitu tu tunataka kwa Serikali ni advice technical advice, policy ndio tunataka kwamba kwa mto hauwezi kufanya hii kama ni mlima uchunge

lakini iwe ni ya hiyo jamii kama tumesikia hapa kuna pahali inaitwa Namanga kama hiyo example ili wananchi waone ardthi hii ni yao.

Yangu ya mwisho, haya maneno ya willing buyer, willing seller yaondolewe kabisa maana ardhi si yangu, ni ya jamii yangu ni ya mlango yangu, ni ya ukoo yangu kwa hivyo mambo ya willing buyer, willing seller iwe out. Vile vile kila wakati tunasikia mtu ako na uhuru wa kuishi kila pahali katika Kenya kuna watu wamemaliza mashamba yawo si hiyo ni njia ya wale ambao wanao na Masaai. Hile interpretation yangu inakuwanga hivi, mtu akisema katika Kenya unaweza kuishi popote, kuna watu wamejaa kwao wanakuja kwetu, sasa mimi hata nikienda kwao nitapata nini? Hiyo ni njia ya wale waliobakisha yao. Kwa hivyo, hii maneno, ndio unaweza kununua au ku-lease lakini ku-ow, watu wa ow kwao. Kwa sababu Mungu alitoa watu makabila arubaini na mbili. You can leasesland yes, you can fanya biashara lakini, you come and own land kwa watu wengine ati kwa sababu ni Kenya, hiyo maneno inangaliwe sana maana wakati mwingine kwa land control tukisema kwa nini hii inasemekani hii ni Kenya na willing buyer willing seller hiyo sheria ndio inaumiza sisi.

Na katika Kenya, kuna watu ambao wana territory zao. Hauwezi kuona kabilia zingine kwa sehemu hizo zao, lakini Masaais are victims of both circumstances, avoidable and un avoidable circumstances. Sisi ndio tunaumia sana kwa hivyo maneno ya land ichukuliwe na Serikali sana Laikipia tunadai sheria hile nimesema. Maana sitaki kurudi, ifuatwe land isiwe kwa land commission, land commission is a colonial idea. Maana sasa kama shamba ni yako na inakua kama ni yetu kama hi mau forest, tofauti gani baina ya ministry ya natural resources na land commission? Na land commission more worse because it is more of modern Kenya, ambayo njia mingi sana ya kunyakua. Kwa hivyo, kwa haya machache ili nisichukue nafasi ya wengine, weka maanani hii agreement ya 1904 ikiisha irudi kwa Masaai.

Speaker: Asante sana Councillor Shadrack Oleretiken kwa maoni yako na kwa sababu vile umechangia ni hoja ambazo ni muhimu sana. Kile tu ninngependa kubainisha vizuri kwa wananchi ni juu ya hilo pendekezo katika Katiba kwamba mkenya anaweza kuishi sehemu yoyote ya Kenya. Inasema ya kwamba Mkenya anaweza kununua ardhi, haki ya kununua ardhi, kwa sababu hata nyinyi mmekubaliana na mimi mmekubali kuuzia watu wa jamii zingine ardhi. Kwa hivyo Katiba hii inasema ya kuwa mtu anaweza kununua ardhi ama anaweza ku-lease lakini sio tu kuenda kwa sehemu ya watu wengine halafu unajitolea boma halafu unasema Katiba inasema naweza kuiishi kila sehemu ya ardhi unajenga nyumba na unasema hii ni sehemu yangu, hiyo haiwezekani. Lakini unaweza kununua katika sehemu yoyote ya Kenya ardhi au mali.

George Nakholi: Asante sana, Councillor kwa hayo maoni tumeyachukuwa na nafikiri imechangia vizuri sana asante wacha tusikie mama.

Pauline Nane: Kwa jina ni naitwa Pauline Nane Tinyargo na ningependelea vizuri kuongea kwa Kimasaii halafu wenzetu wale wako pale wasikize vile Councillor amesema, kwa sababu mimi nimeshukuru sana na ni shukrani sana vile Councillor amesema na ninataka wasikize vizuri.

(Masaai dialect)

Speaker: (Masaai dialect)

Alfred: (Masaai dialect)

Speaker2: (Masaai dialect)

Paul Olesopia: Yangu ni machache nitaongea kidogo kiswahili halafu niseme kwa Kimasaai. Kwa majina naitwa Paul Olesopia ni mmoja wa wanakati wa Narok North Constitution Review, ni na machache nataka kusema wengi wameongea kuhusu mambo ya ardhi na hapa pia mimi ninamchangwa kuhusu pia mambo ya ardhi. Jambo la kwanza ni natakuongea juu ya protection or depedance or even deceased persons na wale pengine labda wanategemea wengine ama watu amba pengine wameaga kwa hile jamii. Kama jinsi muelevavyo kwamba mara nyingi sasa kuna ogonjwa wa ukimwi kuna jamii unakuta pengine baba ameaga dunia mama pia na wale watoto wanaachwa bila kuwa na mtu wa kutegemea. Na hiyo katika section yenu miimi naoona kuwa chambers of lands, 235 sub section A4. Nimeona mmegusia hapo lakini nina addition fulani niweke hapo, kwamba wanafaa kuangaliwa. Kuwe na community control board ambayo from community.(Excuse me) kwamba kuwe na katika jamii katika community, wale amba watakuwa wakishughulikia hao watoto kuona maslahi yao na kuona hile ardhi yao imekua protected mpaka wakati ambayo watakapo kua watu wazima na kusimamia hile shamba yao na kupata hile mali yao jinsi ipasavyo.

Jambo lingine ambalo ninataka kuongea hapo, ni kwamba katika land issue nimepitia sana nikaona people with disability are not considered. Walemvu, na walemvu ni watu amba ni binadamu na wana haki zao. They are human beings na wana right ya ku-own land na property zote hata ku-inherit lazima wao pia wapewe kitu kama hicho. So, hapo wawe protected katika law hii sasa inakuja mpya, kwamba hata wao wakati mashamba yanapatwa wahesabiwe. Pia, inafaa kuangaliwa there are those people amba ni blind even them wana right ya kupata hile shamba na wanahaki ya kuangaliwa na hile shamba yake na jamii iangaliwe vizuri na sheria ambayo hiko.

Na pia nataka kusema kwamba there are this minority people, especially women. Katika jamii yetu ya Masaai wamekuwa discriminated katika mambo ya land issues. Wanafaa pia kupata protection ya land iwepo kusimamia wamama na wapate haki yao kuangalia kama kuwa mzee ameweka dunia asiwe kwamba terminated, na wale wengine ya hile jamii kwamba na weza kukosa hile ardhi mali yake ibaki pale kama vile mwenzetu mmoja alisema hapa kwamba hii sheria ihusishe yule mzee na mama katika ownership ya hile land. Kwa hivyo protection ya law iwekwe kwamba isimamia hao.

Jambo lingine ni nataka kusema ni kwamba, mambo haya ya willing buyer, willing seller imeleta shida kweli. Mara mingi wazee ndio wanauzwa shamba kwa mabar bila mama na watoto kuhuishwa. Haangali kama kuna wengine amba wamelamaa ndani ya

hile jamii pia wanategemea wapate hile shamba, na pia wataoa watasaidia hapo na kwa hivyo watakuta hile shamba yao imeenda. So, in the law, now I mean hii sheria ambayo inakuja, hii mpya kuwe na sheria kali ya kusimamia hao watu na kuwa-protect wote kwa jumla na jamii wahuishwa katika kila jambo majina yao yote yawe yana-appear katika tittle deed ili mzee asiwe na namana ya kuenda ku divide hile shamba bila wengine kuhuishwa. Kwa hivyo yangu ni hayo tu ni nataka kusema kwa ufupi ili nisije kula wakati wa wengine, nashaukuru sana. Thanks a lot.

Kepoi Raria: Asante sana Olesopia na na umeongea juu ya haki ya watu walemaru na ningependelea ukiangalia kipengele kutoka namba thelatini na tisa, katika haki za kimsingi utakuta kwamba watu amba ni walemaru wamepewa umuhimu katika Katiba hiina ningependa kwa wakati wako ujaribu kusoma na utaelewa kwamba pia wamehesabiwa. Asante.

Speaker: Sasa tutaanza pale tuchukue watu kama saba hivi. Mama ataanza namba 1,2,3,4 hapo namba 5,6,7 na mzee huyu 8 tukimaliza hawo halafu ndio tukuje kama tutakuwa na mambo meingine tukuje kwa wengine na mfanye haraka haraka ili tuweza kwenda kwa mambo mengine.

Kepoi Raria: Pengine jambo ambalo ningependa kuguzia kuhusu umilikaji wa shamba kwa sababu umetetea kina mama ili wawe pia wanaweza kumiliki shamba, ni kwamba pia jamii yetu ina paswa pia kuzingatia mtoto wa kike. Hii ni kwa sababu wazee wa Kimasaai wanaamini ya kwamba mtoto wa kike hapaswi kumiliki shamba kwa sababu ataolewa na ataenda kumiliki shamba kule. Lakini ningependa kuwaambia kwamba ya maisha imebadilika wasichana hawaolewi tena, kwa hivyo usifikiri kwamba atapata shamba lingine la kumiliki kwa hivyo lazima pia mhesabu watoto wa kike kama watoto wa kiume.

Jane Jeton: Basi asanti ma-Commissioner wetu, asante tena wananchi wale wamekuja. Kwa majina naitwa Jane Jeton kutoka Elabelibeli kwa ward ya Councillor yule ambaye kila mtu anamjua hapa. Mimi nimekuja kutilia mkazo kwa Katiba mpya kwa sababu ukweli kutoka siku hile tuliongozwa na Katiba ya zamani nimeonelea heri hata na mimi nije niweke mkazo Katiba ambayo sasa ni mpya na ina uongozi mzuri wa utawala. Nimeshukuru pia kwa Wamasaa kujitolea kwa sababu wameona kweli wamekua wakiteswa nikiwa Mmasaa mmoja kwa sababu nimeolewa nchi hii. Kile kitu tungependa kusema tubakishe kuowana tu, kwa makabila lakini sio kuenda kubakisha kuendelea kukulana kwa ardhi hi. Ardhi hii tubakishie watoto wetu kama watu wamezaana nchi yao sana, waendelee kununua mashamba wauzanie huko chini unachimba nyumba huko chini unakaa, kwa sababu tumeambiwa sasa Katiba hii itatupatia ardhi hii yako mpaka huko chini. Kwa hivyo kama kwenu mmezaana sana endelea kuuzia mwagine huko chini achimbe nyumba muishi kwenu. Lakini sio kuja kununua umasaini, umasaaini tumekataa tunataka tuwe na ardhi yetu ikiwa kubwa iwe ni yetu na ya watoto wetu.

Ningependa kushukuru Mheshimiwa Ole Ntimama ambaye amesimamisha area hii yote, ununuaji wa shamba ama kumiliki mashamba hiyo yote ilikuwa upande wa mau. Shukrani iende kwa huyo Minister, kwa sababu wako na shamba ya mali ilipotea,

mashamba ya mau ilipogawa kule sisi hata wale wamezaa watoto wa Masaai hata hatukupata. Na Wamasaa wenyewe ndio walikuwa wanagawa hiyo mshamba lakini wanaleta mtoto wa Kinuthia wanampatia shamba sisi tunakuwa wachungaji? Nikaenda pale nikawambia si mpatia hawa vijana wa Olechesoni shamba mimi nimekosa akapewe mwanamke alikua anaitwa Pauline Kipendela.....(Masaai dialect). Tumesema sasa hatuwapatii ardhi ya Masai tutatawala sisi wenyewe na watoto wetu tumbakishia khabila wengine kuwaoa tu na tukiendelea tutaendelea kuzaa tuwache hapa kwa wazi(inaudible). Kwa hivyo nimeshukuru kwa kila kitu.

Lile jambo lingine ningependa kutilia mkazo ni mambo ya wajane kwa sababu mimi ni mjane. Wajane tunapinga kabisa jamani, mzee akikufa hata haupatiwi nafasiya kumzika unasindikishwa na mambo umemroga, umemfanya nini mpaka masikio unachanganyikiwa na kweli unawenza kuishi na mtu miaka thelatini uje umroge ya nini? Na amekuwachia watoto size hii jamani wajane Kenya tunalia kabisa hamkeni Katiba mtuokoe tunakufa kabisa, na tuko na right kama mzee alikufa haikuandikwa kwa kitabu(Inaudible) na mzee wako siku moja mwekwe kaburi moja. Mungu anajua kwanini ametangulia na wewe umewachiwa wale watoto msichukue kimakosa, mjane anangaika hapa Kenya hile mpaka unalia machozi mpaka macho inageuka kama ya simba sijui ni kwanini tunateswa namna hiyo? Tunateswa kabisa jamani Katiba angalieni hiyo mambo ya wajane na watoto wawo kabisa kabisa.

Mambo mengine area ya Masaaini, wekeni mwanamke akuwe wa kawaida tu kama mtu yule mwengine, hapana sema.(Masaai dialect) kwa nini hawo ma Councillor wako hapa wanaume tupu hakuna wanawake mnataka kuniambia sasa hii kiti hiko na wanawake wawili hawangeongoza Council? Wangeongoza, nitawapatia nafasi hii tu kwa sababu Councillor Eile atasimama nilikuwa nimeamua kumpinga lakini tunampenda. Tunampenda kabisa wacha hawa wengine wanakuja hapa nyuma nyuma hapo wenze hatujui tunampenda, lakini wa Nominate wanawake hata wawo waingie pale ndio tugawane. Asante.

Kepoi Raria: Asante sana mama(Masaai dialect)

Speaker: Huyu alikua namba 1 na 2, tuende tumalize hawa wengine ukitaka kuzungumza hakuna yule atakataliwa.

John Oketch: Hamjambo Bwana Commissioner na wananchi wa Narok. Mimi kwa majina ni naitwa John Okech nafanya na shirika ya CPDA (Christian Partner Development Agency) kazi yetu ni civic education katika Narok. Tunafanya kazi mzuri kwa sababu bila civic education masomo ya kiraia hawa watu hawangejua Constitution ama Katiba ni nini sini ukweli? Kwa hivyo tumefanya na kazi yetu ni ya gender consultant tuna deal na kina mama na pia kina baba na watoto kila watu. Katika Narok tumekua tukienda round tukipatiana civic education kuna mambo matatu ambayo tunapambana nayo: ya kwanza ni land trust board, wanasema kwamba wanawake land trust board haitakikani wakue elected members na pia members hawatakiwani wawe ni watu Wamasaa wenyewe isiwe ni watu wakutoka nje. Shabir amesema inatakinana watu wa kumi katika land trust board hiyo na watatu wakiwa ni wanawake ili kwa sababu katika Masaai wanasema wazee wakienda kuuza shamba,

huwahawafiki nyumbani. Ama wanaauza tu, wanaauza halafu wanaenda hivyo, kwa hivyo inasemakana mama pia anatakinana awe pale na ajua maneno. Haya.

Ya tatu ninasema distribution of resources, Wamasaii wamethuluiwa zaidi, wanasema kwa mfano, kama Masaai Mara wanasema hiyo mali yote ya kutoka tourists wakikuja inaenda wapi? Inaenda nje hafadaidishwi chochote, Katiba inasema barabara imekuwa mbovu kabisa. Kwa mfano ninasema sehemu kama mau, mahali wanapanda barley wanapanda waruu wanasema wanshida nyangi sana kwa sababu hizo pesa wakati transportation ikija wanaenda wachukue wapeleke kwa soko barabara inkuwa ngumu sana. Kwa sababu wanasema Serikali iangalie hiyo maneno.

Halafu, mambo mengine wanasema kwamba, wanasema wanawake pia tumewafunza ili wasimame katika council, wasiwe tu wanaongaja wazee wanasimama, kwa sababu wanalia wanauwezo pia ya kufanya hayo maneno. Kwa hivyo hiyo ndio mambo tulipenda ndio tukasema tuzungumze na pia tueleze commission wapewe nafasi sawa na wanaume wapambanie maneno mengine. Asante.

Speaker: Asante sana kwa hayo maoni bwana Oketch.

Joseph Olekuaet: Kwa majina naitwa Councillor Joseph Olekuaet kutoka Narok County Council. Basi kwa hivyo nachukuwa nafasi hii kuwashukuru kwa kufika kwenu leo hapa. Yangu ni matatu kuhusu maneno ya ardhi. Ya kwanza kuhusu uuzaji wa ardhi, na kitu hiki mimi ninakielewa kwa sababu nimekaa upande wa Kajiado pahali panaitwa Rongai. Na wakati nilipoanza kuenda Rongai nilikuta ni kubaya na sahii wale walitembea huko, wanajua vile kuko na ni Wamasaii tu ndio walikuwa wanakaa hiko sahii haitajua utafikiri hata ni Nairobi hata ni kubwa kuliko Nairobi. Uuzaji wa ardhi ni kitu kibaya zaidi, na tuseme katika Narok hii, ni vile imesemwa na wenzangu hapa kama Mheshima Rotkey anasema kwamba tuwe na control board ya makamati ya district. Mimi nasema hiyo maneno tupeleke katika village council. Watu wa kijiji hicho(Masaai dialect)

Kwa hivyo haya naomba turudishe hiyo katika village council waangalie huyu mtu ana shida gani(Masaai dialect) ako na shida kweli? Hiyo ni moja.

Kuhusu mambo ya. Lease, ati tunasikia hii proposal tunaona hapa inasema ya kwamba 99 years kwanza mimi niko na miaka arubaini na mbili saa hii nikisimama hapa. Sasa kama mimi na nina-lease ardhi watoto wangu wataona hiyo ardhi yangu kweli? (Masaai dialect) tunaomba ya kwamba leasing irudishwe katika miaka thelatini na tatu mwisho katika Kenya hii.

Ya tatu ninasema ya kwamba hii haki ambayo watu wamenyanganywa hatuwezi kusema ardhi wamenyanganywa Wakikuyu irudi kwa Wamasaii, wapatiwe Wakikuyu. Hatuwezi kusema ardhi wamenyanganywa Wakelenjin na wakoloni wapatiwe

Wamasaai, wapatiwe Wakalenjin. Lakini hile ardhi ambayo sisi tumenyanganywa hata kama ni kilomita mia saba, sisi tutaenda pale kwa sbabu tuna-claim ardhi yetu. Basi nitaongeza kwa hii Katiba maneno mawili ambayo ni mchango yangu nitachangia hii Katiba, nitaongeza ya kwamba katika haya magonjwa yote ambayo tunayo, ni ugonjwa ya kutojua kusoma na kuandika, ninaomba hii Katiba iweke kwa uzito ya kwamba sisi Wamasaai tukipiga wanyama si tunashikwa? Ni kitu ambacho ni kibaya tuseme watoto wale ambayo ni Wakenya wote waende shule na inakua ni hati kwa mzazi ambaye hajapeleka mtoto shule. Tunaomba hata hile Serikali itachaguliwa chini ya hii Katiba wawe na pesa ya kusomesha watoto hawa kwa sababu sio kila mta anaweza kusomesha watoto.

Ya mwisho, nikusema sisi tunatakuwa kama wa Marekani ama wengine, wazee wetu wanazeeka na wahajafanikiwa kupata watu wa kulinda hao. Tuwe na sehemu ambayo mzee kama hana watoto wa kulunda yeye, apelekwe huyo mzee na kwenda kuchunga na Serikali na itolewe pesa ya kwenda kuchungwa wale wakongwe amba hawana maboma zao. Kwa hivyo ni hayo tu nimeongeza.

Kepoi Raria: Asante Bwana Olekueat umeongea juu ya elimu, na ukisoma katika haki ya kimsingi utakuta kuna haki ya kimsingi katika Bill of Rights, na inasema ya kwamba kutakuwa na masomo ya shule ya mzingi ambaye itakua ni ya bure itakua free and compulsory. Itakuwa ni ya bure na ni ya lazima kwa kila mtoto. Na Bill of rights, hamsini na nane ukurasa wa tisa mkiangalia. Na hii inasema kwamba, katika haki za watoto inasema kwamba, mzazi ambaye hatachukua jukumu lake la kumsomesha mtoto, hiyo itakua ni hatia katika sheria. Asante.

Speaker: Number nne.

Robert Nyangawu: Mimi ni naitwa Robert Nyang'au na wakati mwingi ninafanya kazi kwa CJPC na yangu ninataka kuyazungumza ni yale ambayo nimeyasoma kwa constitution draft ambayo mmetoa. Namba 299 inahusu boundary zetu za nchi yetu. Kwa hivyo namba 299 ningependa mkitoka hapa chora map yenyewe ili sisi tuweze kuiona. Nyingine, ni pahali ambapo tumezungumzia miaka ambayo land inakuwa lease, mta anakuja wame-sign land lease anaenda kwa miaka tiasini na tisa. Ukweli ni kwamba kuna zile ambawo zilikuwa zimewekwa na mpaka wakati huu miaka yake haijkwisha na wengine wetu tutakuwa tumeondoka ulimwenguni huu bila kuona that agreement, hasa zile ambayo zinahusu watu wa Narok, zile ambazo zinahusu Brook bond Kenya Limited kule Kericho. Zile ambazo zinahusu sehemu za Pwani ambazo hata watoto wetu hawawezi kurithi. Kuna lingine ambalo mmesema kwa hiyo draft, mambo ya village government, district government. Yangu ambayo inanisumbua sana ni kwamba, how will it be implemented? Kuna pesa ambazo zimepengwa ambazo zitaweza kutumika au vile tunang'ang' ana wakati kama huu ya kwamba Katiba tuitumie Katiba mpya, how long will take for the village government kufanya kazi?

Inging ni article namba 160 ambawo mnasema, Rais awe anamaliza 2 terms, sasa kwa sababu wakenya wamekuwa wengi, hata Members of Parliament waende term mbili. Hakuna haja wao wanaenda continuous hata wengine walienda 1970 hata sasa wako. Ni wakati gani watatoka? Kwa hivyo hata wao wanatakiwa wapewe miaka ya kudumu kwa Paliament kama ni term

mbili ya 5 years each na wawe wanaenda nyumbani kwa sababu wakenya ni wengi. Kuna mengine ambayo hata baada ya kusioma, sisi tulishangaa kwamba au mimi mwenyewe tulipokutana ya kwamba Members baada ya uchaguzi.

Interjection: Rario: Ningewaomba tafadthali kwa sababu sahii tunongea juu ya ardhi kwanza tumalize juu ya ardhi, halafu tuende mambo mengine asante.

Robert Nyangawu: Pengine Bwana Commissioner kwa sababu nilikua naondoka na ni hiyo tu nilikua nimebakisha, wacha tu nimalize niondoke. Kwa sababu ya Nomination, hii nomination tumeona hapa late Kariuki ameenda Bunge, Barng'etuny na watu wengine ambawo hawastahili kwenda kwa hiyo nyumba. Kwa sababu hiyo, inatakiwa itusaidie sisi ili watu ambawo wanakua nominated kwenda kwa hiyo nyumba wawe watu wanaenda positively, kuchangia maendeleo ya nchi hii, hata nomination ikwishe hata hakuna haja ya kuchukua watu wengi. Nimemaliza.

Kepoi Rario: Wananchi hebu tusikazane, kwanza jambo la ningependa kuwaambia kila mtu ako na haki ya kutoa hoja zake. Lakini tungewaomba sana tujaribu kuguzia yale mambo moja kwa moja tukimaliza ardhi tuende nyingine.

Speaker: Haya nambari 5 alikua nani? 6 namba 5 alikua nani ameingia na utamfuata.

Olesungulia: Basi asante sana Bwana Commissioner.....(Masaai dialect)

Maranga: Basi asante sana Bwana Commissioners kwa jina mimi nitwa Councillor Maranga na natoka(Inaudible) council, nafikiri tumeongea mambo mengi lakini kile kitu tunatilia mkazo kabisa ambacho kimetuumiza roho na kimeumiza watoto wetu. Kitu cha kwanza kinaitwa land control board. Land control board, DC ndio Chairman na ni mtu amekuja tu kwa siku moja, siku ya pili anaenda na ye ye ndio anatawala kumpatia yule mtu anataka shamba anaunue. Tunasema mambo hayo ya land control board yaanze kwa hiki kitu mliweka kwa review, kusema village council ianziwe hapo kwa village. Kwa sababu unakuta hapa kwa land control board mzee anakuja ana rokota mama mwengine anamwambia wewe kwenda sema wewe ni bibi yangu anarokota vijana wengine anawapatia shilingi tano anawaambia kwenda sema wewe ni mtoto wangu. DC hajui land control hawajui kwa hivyo tunataka ianzie mahali tunajua mama ya fulani ndio huyu, kitu kimetuumiza sasa miaka nne na ndio kimemaliza mashamba ya Masaai.

Kitu ingine tunasema hawa ma head up department kama hapa Narok akiletwa mtu anaitwa forester sahii tukiwa hapa ye ye ndio anauza mba wawo ndio wanaiza makaa lakini mwenye shamba kabisa hawezu kuuza kwa sababu anashindwa kumwambia wewe kwa nini unafanya hivi anyanganywa? Na hiyo kitu inatakiwa mwenyewe asimamie.

Kitu ya tatu, kwa sababu nataka kwenda haraka haraka, kitu kinaitwa boundaries, boundaries ya Narok inashangaza sana ukienda hapa Mau, unakuta area kama hapa ni Nakuru. Kwa sababu Mzungu ndio alikuwa amefunga shamba, anaingia Narok

mpaka katika Narok tunasema yaani ni Nakuru. Lakini corner ingine hapa ni Narok.

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: Asante sana. Jambo ambalo ningependa kuwakumbusha wananchi ni kuwaambia ya kwamba, wakati tutakuja kuongea juu ya mambo ya devolution, juu ya mambo ya kuleta utawala kwa districts, kutakuwa na District Council. Kwa sababu wananchi wamelalamika kuhusu ma afisa wanaotumwa kutoka Nairobi, halafu wanakuja katika sehemu za jamii na wanakuja kufanya mambo ambayo hayakubaliwi na jamii. Mtakuja kuona ya kwamba hizo District Councils ambazo zitakuwa hasa serikali italetwa kwa District Councils. Watakuwa na nguvu ya kuwaajiri watu kutoka kwa district yao. Kwa hivyo hamtakuwa na shida ya watu kutoka nje, kuja kunyakua ardhi zenu ama kuharibu mali yenu.

Simeon Lemurusu: Asante Bwana Commissioner. Kwa jina ninaitwa Simeon Lemurusu kutoka Lamek Ward, na mimi ni Councillor wa area hiyo. Kweli mengi yamesemwa lakini kidogo tu, ningependa kufanya repetition kidogo na ninaomba uniruhusu niendelee kidogo.

Kuna kitu kinaitwa (inaudible) land ni life. In any way tukiishi, tukifuta hewa, chakula tunapata katika ardhi. Kwa hivyo, ardhi ni baba au ni kitu ambacho kiliumbwaa na Mungu ili binadamu wote wafaidike nayo. Kweli, imesemekana kuna land grabbing, land grabbing imeingia hapa na immeanzwa na wakubwa huko mpaka hapa hata wadogo wameingia. Laini hii imeingia kwa ajili land officers, registrars wameanza kutoa titles mbili. Katika district hii kuna watu ambaa wako na titles mbili ya shamba moja. Na hii ni njia moja ya ku-grab land bila mtu kujua, hata za wengine zinauzwa.

Kitu kingine kipo ambacho tunaita land lease katika nchi yetu, hapa Maasaini. Sisi ndio wenye ardhi, lakini chakula ambacho inatoka huko, mavuno yanayotoka huko na pesa zinatoka huko, zinaenda, zinapelekwa na wahindi. Serikali imetutupa sisi, kwa vile ardhi hii ni yetu lakini hatufaidiki nayo. Kama ni laws zinatengwa, (inaudible) kama ingekuwa hivyo, bado inaenda kwa watu wengine ambaa wanamiliki, ambaa sio wenye mashamba. We are being milked by the foreigners. Kwa hivyo, ardhi hii yetu ichungwe sana. Hapa tuna ninety nine years, hii ni lughya ya nani? Ni ya white people. Tangu Wamaasai kutoka kwa turbo ya mama yake, wale ambaa walikuwa huko, hawajui ninety nine years ni nini. Kwa hivyo so long as sheria imejulikana imetoka wapi na inaelekewa wapi, hii tu kuchukua first title (inaudible) inherited by the family line na kusiwe na ninety nine years ambazo zitabidi baadaye tena niende ku renew, hiyo tumekataa.

Kulingana na haya mambo ya colonial masters, ardhi hii, kwa mfano mliposikia Laikipia, pande za Marsabit, Nakuru na hata Nairobi hapo zamani, iliponyakuliwa ilijulikana kwamba inatoka kwa watu fulani, watu wa mlango fulani au clan fulani. Je kama inawezekana, chochote ambacho saa hii wazungu wanacho, zile big ranches ambazo wazungu wanazo, zinapokwisha hizo ninety nine years ambazo zimekuwa ni kitu kama kikwazo, basi ardhi irudi kwa original people, owners, bila condition yoyote.

Nikiendelea kidogo, kuna kitu ambacho kinaitwa kiosk, kiosk inaonekana, mtu yejote akija hapa anasema wacha nipate kiosk.

Maasaini mhesimiwa, kiosk hakipatikani kwa central. Na kwa vile hiki kitu mmetupatia, hati hii hata ingawa imetokea, haikulengwa pahali pengine, inalengwa Maasaini kwa ajili Wamaasai ndio bado wana ardhi, na ardhi hii tuachiwe sisi. Yule mtu ambaye anaona anataka pahali pa kuishi, kwa vile inaonekana watu wanataka kutafuta tu pahali pa kuishi, waedeele kujenga gorofa zikielekea mbinguni pahali hakuna mtu anang'ang'ania kupata.

Sina mengi ni hayo tu nitasema, tuko pamoja na nyinyi na sheria hii itulinde sisi Wamaasai kwa ajili sisi ndio tumebarikiwa kuwa na resources hizi. Kama wanyama kwa mfano, hakuna pahali unaweza kupata 300,000 hectares ya ardhi ambayo inapatikana pahali pale wanyama wanafugwa. Na ardhi kama hiyo iangaliwe sana isiende kwa watu wengine bali ibaki na wenyeji ambao ni sisi Wamaasai. Sina mengi kuhusu hayo.

Nikiendelea kwa mambo yale ambayo mnasema kuhusu nini...

Speaker: Ya local... Commissioner atatusaida kuhusu hiyo.

Simeon Lemurusu: Ooh, sawa nilikuwa ninataka kuendelea.

Maurice Ole Raria: Ningependa kuwaomba kwamba hoja ambazo mtatoa, mjaribu kabisa msirudie jambo ambalo limezungumziwa. Mambo ya lease yameshazungumziwa, mmeamua ni miaka thelathini na tatu. Kwa hivyo mambo kama ya lease, hayo tafadhali msirudie. Lile jambo ambalo utazungumzia liwe ni hoja ambayo ni mpya kabisa.

Speaker: (*In vernacular*).

Rael Ologoyiero: Asante sana. Mimi ninaitwa Rael Ologoyiero. Nimesikia ambayo yale mmeongea kuhusu ardhi na nimeyapendelea sana. (inaudible)

(Interjection) **Speaker:** Ongea ukitumia microphone na upaze sauti.

Rael Ologoyiero: Mimi nitaongea kuhusu mambo ya ardhi, kwa sababu wakati ambao mlipata taabu ndio sisi pia tulipata taabu. Ninaongea kuhusu ardhi ambayo tulinyang'anywa na wabeberu. Sijui wengine wanasesma ati sijui ati iko pahali ambapo pamechukluliwa, wameshajenga, wakati ambapo wametuhamisha sisi kweli hatujajenga? Si nimejenga kama hao? Hata kama ni nyumba ya udongo. Kuhusu hiyo ningetaka waturudishie sisi ardhi yetu.

Jambo la pili, wakati wa wabeberu tulijua kule beacons ziliwekwa. Sasa hakuna beacons, tunaona tukipotea

(inaudible). La tatu, mimi nimesikia umeongea mambo ya ardhi. Kuna pahali panaitwa Maasai Game Reserve, na ni nchi

ambayo unajua sana. Kweli sisi tuna serikali, tunasikia ati wanyama wakiua mtu ati analipwa elfu thelathini, na wakati wewe mwenyewe ukiguza mnyama, hata wanaua roho yako, roho ya kibinadamu. Ikiwa mnyama ameua binadamu, analipwa shilingi elfu thelathini. Si hiyo ni kinyume cha haki zetu? Pia ninataka kama wanyama wanaumiza mtu, alipwe kama milioni kumi! **Applause from the audience** Nitakomea hapo kuhusu hayo mambo ya kuwalipa binadamu wanapoumizwa na wanyama na ambao wanatakikana kulinda ardhi yetu.

Na kama ninataka kulinda, ardhi kwa sababu kila pahali kuna wakili, hata kama sisi ni Maasai, lazima tukitaka, tukitoa (?) hata kina mama, si mmekwenda kuleta msichana wa mtu? Ni kulewana, na kwa nini unaandika kwa title deed jina langu pekee yangu na ni sisi wawili tunajenga hiyo boma pamoja? **Applause from the audience**. Lazima mkiandika title deed, bibi yako anasimama hapa, karibu na wewe. Ukitaka kuuza, muuze pamoja na mkikosa mnunuzi, mkose pamoja. **Applause from the audience**. Jambo lingine permit iko, permit... Ndugu zangu (inaudible) hatua akichukua halafu asiuze title deed, msiuze ardhi. Nikiuza ardhi kuna permit na lazima utajulisha wakili awe anasimamia hiyo shamba wakati mtauza akuje kueleza matatizo alipata halafu apate kuuza. Sio ati yeze anaondoka, sisi tumekuwa wazee sasa, sio ati unaenda kuuza ardhi, lazima muwe pamoja.

Jambo lingine kuhusu ardhi (inaudible). Lakini kila mtu yuko na nyumba yake ambayo alijenga. Wakati Mungu alitupa sisi ardhi alisema Wamaasai wakae hapa, Kalenjin wakae hapa, Turkana wakae hapa. Hicho kitu ndicho kinawasumbua Wamaasai sasa, sana. Wengine wanawaingilia wengine, kuwanyang'anya ardhi yao na vile I see it, sio mbaya kununua. Kama mmeshaongea na kusikilizana na kuamua huyo mwengine akubali anunue si ni sawa? Hata kama ni Mkalenjin hata kama ni nani, hata kama ni nani. Lakini kutuingilia sisi na kutoa wengine, iko wengine wanakaa Torten Maasai, (*In vernacular*). Ati kuamisha Wamaasai ndani ya... **Applause from the audience** kwa ardhi yao! Hiyo ni njia ya kunyang'anya mtu. Hiyo isimamishwe na kila mtu ajue ni ardhi ya wenyewe ambayo tunaenda kuomba pole pole au kununua kwa njia ya amani.

Msitu, ningependa kuongea juu ya misitu. Lakini hiki kitu nyinyi mnachekelea, haya maendeleo ya juzi juzi (?) hata nyinyi mnasema "ni maendeleo, maendeleo". Zamani Maasai hakuna... hata ni dhambi sisi kukata ardhi! Mungu alitoa ardhi kwa kila mtu, hakuna ati kukata, lakini maendeleo kama yatapatikana basi sawa sawa. Lakini tukikata misitu, wakati sisi Wamaasai wenyewe tulikuwa tunachunga, hatuwezi kufyeka namna hii, hata tunafyeka (*in vernacular*), hatuwezi kufyeka namna hii. Wamaasai watatoa nyumba, Wamaasai watanunua fimbo, na siku hizi wamekuwa kama ng'ombe, wanafyeka tu misituni mpaka saa hii sisi hatuna maji uko Magadi. Kwa sababu wamefyeka, hiyo hiyo ardhi (?) wenyewe wachunge haki yao. (?) iende kwa D.C., iende kwa polytechnic, iende kwa (?) iende kwa ... wacha wenyewe wachunge na kama watamaliza ni shauri ya nani, si ni yao? Yangu ni hayo tu, nimemaliza.

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: Asante sana. (*In vernacular*) maoni yako ni mazuri sana na nimefurahia sana mambo mawili ambayo umezungumzia. Kwanza ni juu ya mazingira, umesema kwamba tusema kama ni misitu iliyokatika sehemu ya jamii, ni jamii hiyo inapaswa kulinda. Na ukienda katika sura ya kumi na mbili(12) ambayo inahusu mazingira na mali asili, imesema kwamba kila mtu nchini Kenya, anawajibu wa kulinda na kuendeleza mazingira. Kwa hivyo itakuwa ni juu yako mwenyewe katika sehemu uko ama katika sehemu ambayo jamii yako iko, mhakikishe kwamba ni nyinyi amba mnaangalia mazingira na sio watu wengine kutoka nje.

George Nakholi: Basi, nitawaomba mkija hapa mchukue muda mfupi ili tuweze kuendelea mbele. Na lile jambo ambalo limezungumziwa, tafadhalu wachana nalo. Tutaita watu kumi, nafikiri tutakuwa ni kama tumemaliza na nitajaribu kuwahimiza kina mama pia watoe maoni yao, tusije tukawaacha nje. Tutanzia number1, huyu mama hapa, yule mzee number 2, mzee hapa number 3, mama hapa number 4, number 5 last, number 6, mama mwengine, kina mama wako wapi? Mama? Haya number 7, number 8, kwa corner ile number 9, hapo mzee, wewe number 10. Tumalize na hawa, basi muwe haraka, tumalize haya mambo.

Hellen Kipetu: Asante sana ma Commissioners na wale wananchi wetu wako hapa. Mimi ninataka kuzungumzia kidogo kwa sababu watu wamezungumza sana. Ninataka kuzungumza mambo...

(Interjection) **Speaker:** (Inaudible)

Hellen Kipetu: Mimi ninaitwa Hellen Kipetu, na mimi ni nominated Councillor hapa. Ningependa kuzungumza juu ya haki za kina mama katika umilikaji wa ardhi. Ningependa kusema kwamba kina mama amba ni widows, wananyanyaswa sana na community na hawa kina mama hawapewi haki zao. Unakuta mzee akifa kwa familia, mama, wazee wale amba ni ndugu za mzee wake ndio sasa watakuwa wanahaki ya kumiliki ile ardhi ama wanaifanya hiyo ardhi vile wanataka. Ningependa kusema kuwa iwe automatic kwamba mzee akifa, mama directly hiyo ardhi ni yake. Na hata hakuna maneno ya kusema ati unaenda kuchukua letter of administration, automatically ardhi hiyo ni yako na watoto wako.

Ile ingine ninataka kusema hata wale orphans, unapata huu ugonjwa wa Ukimwi, watu wanakufa sana. Mama anakufa na baba anakufa. Unakuta tena saa hizi ndio watoto wanaumia sana. Ningependa tu kusema hiyo ardhi ama whatever property ambayo imeachwa, ikuwe directly inherited na watoto na isiwe ati kuna ndugu wa mzee ambaye anasimamia hiyo familia. Kama ni title ama ni kitu fulani kiwe ni cha watoto, hata kama serikali itachunga mpaka watoto wakuwe wakubwa, serikali ichunge ili watoto hao watumie hayo mali.

Kile kitu kingine ambacho ningependa kuzungumzia ni hawa foreign buyers. Sijui tutakuja kuweka katika sheria vile ninasema kwa sababu, hapa Umaasaini kuna wazungu wengi sana na wahindi, wamenunua ardhi ya Wamaasai. Sijui tutaweza kuwekaje katika Katiba, ili mtu mwengine aje aseme vizuri kwa sababu sielewi. Ili tuweke katika Katiba ili Wamaasai au wale watu

ambao wameuza kwa sababu wengine wameuza blindly, ili hiyo ardhi iweze kurudishwa kwa Wamaasai. Kwa sababu unakuta mtu anauza even 1,000 hectares, hana hata chochote na sasa yeye anaranda randa tu, hana pahali, na watoto wake sasa ni kama orphans.

Kile kitu kingine ambacho ninataka kuzungumzia kwa sababu ya saa, ni land office. Hizi ofisi za land na survey office wananyanya sana Wamaasai. Unakuta hawa watu hata kuenda kupima shamba na iko ile pesa ya serikali tunalipa tunarudi kunyanyaswa mpaka inabidi ulipe pesa zaidi ni kama unanunua shamba na ni ardhi yako unaenda kupatiwa. *Applause from the audience.*

Na kwa sababu labda sitapata nafasi nyingine ya kuja hapa kuongea, ningependa tu kuongea juu ya environment kidogo tafadhali. Nataka tu kusema hawa watu ambao wanalease mashamba ya Wamaasai hapa, wanapollute environment. Sasa umekuta pahali kwengine hata hakuna ndege, hakuna hata nyuki kwa sababu ya vile wanaweka hayo madawa yao, wana spray na hawajali. Unakuta ndege inakuja inaspay hata watu wakikaa chini. Kwa hivyo ninataka tu kusema hiyo iangaliwe kwa sababu labda sitakuwa na nafasi ya kuja hapa tena. Asanteni sana.

Maurice Ole Raria: Asante sana Councillor. Kwa kusema kweli amezungumzia mambo ambayo ni ya muhimu sana. Hasa kama tungepata nafasi kwa sababu niliwaambia kuna mambo mengi sana katika Katiba hii na hatuwezi kuyazungumzia yote. Lakini kwa sababu ameongea juu ya mambo ya environment, hata hii shida ilionekana sana katika sehemu ya Kajiado kwa sababu mnajua kuna quarries, kama Kipini Quarry. Portlands wakifanya ile quarrying wanaacha sehemu hizo zikiwa ni mbaya sana.

Lakini katika Katiba hii, hao private developers ambao wanakuja kutoa madini hapo, watakuwa chini ya sheria ili baada ya kufanya tuseme kama ni quarrying ama baada ya kufanya kazi ambayo wanafanya katika sehemu hiyo, itakuwa katika sheria hii, katika sheria imetolewa na Katiba, ni lazima wa-reclaim ile land. Kabla hawajaacha hapo kwenda mahali pengine, ni lazima wafanye reclamation na kwa community wahakikishe ya kwamba wamefanya reclamation ya kutosha ile waweze kuenda mahali pengine. Kama hawajafanya hivyo, basi watashtakiwa katika korti kuu ama Supreme Court, ambayo Katiba hii imebuni.

Speaker: Asante sana. (*In vernacular*) *Applause from the audience* Hawa watu wakora wako hapa. Ndugu yangu mimi niko na uchungu, mimi ninauza (*in vernacular*) mpaka ninashtuka sana. Na ni shamba wakbadilisha na ndugu zangu, sio kununua au kuuza, ni kubadilisha tu. Unahakikisha mimi (*in vernacular*) nimekuta tu Ksh 30, 000. (*in vernacular*).

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*).

Applause from the audience

Lerionka: Bwana Commissioner, wazazi na watu wengine hamjamboni. Kwa jina ninaitwa Lerionka Ole Mairbe, ninafanya kazi na NGO, mambo ya Civic Education katika Narok District. Jambo langu la kwanza ni kusema kwamba kwa kifupi no tax on idle land. Kwa sababu wengine wanasesma kwamba Maasai land ni idle land, kwamba hakuna kitu kinapandwa, hakuna mimea inapandwa huko kwamba it is just idle.

Mimi ningependa kusema kwamba nchi ya Wamaasai sio idle kwa sababu kuna wanyama ambao wanaishi kwa ardhi ambayo tuko nayo...***Applause from the audience*** kama wildlife, elephants ambao wana-interfere na watu huko na pia hiyo ni source of revenue from the tourism industry. Halafu ya pili pia kuna wanyama wa Maasai ambao kama livestock wanakaa katika hayo mashamba. So that land is not idle, because our animals are grazing there plus the wildlife. Pia ninaweza kusema kwamba, 55% – 80% on the wildlife roams of private people's land not on reserves and game reserves.

Ya pili ni abrogation of the thirty three year leasehold by the community. Hii ni kusema kwamba hii leasehold ya thirty three years isiwe huko. Community wakivote, 30% of the community, waandike signature wavote, hiyo leasehold iwe abrogated, irudi back to the community. So it should just be temporary because thirty-three leasehold you must have a mortgage thirty years old but thirty years is very long. It should be renewable, for instance we consider like Narok North, if thirty people, 30% of the voters in Narok pass a vote and sign the memorandum, both the leasehold should go back to the community. So we should have a right to dissolve the leasehold.

Halafu ingine...

(Interjection) **Speaker:** (inaudible).

Lerionka: (inaudible) because even in the Katiba they say that we can recall a Member of Parliament. Members in the constituency vote 30% (inaudible) so that means that should also be added also in the list (inaudible).

Then another thing is that 90% of the revenue from the Parks and Reserves should go to the community, 90%. Like for instance Maasai Mara Game Reserve, 90% of the revenue should come to the community not to the central government. Something else I would like to add on is the (?) . We know that everybody in Kenya eyes Maasai land because we have vital resources, our land is very productive, most people come to buy our plots of land. So we want to say that the people who are not Maasais they can come and stay with us but they should stay as aliens, not as citizens. They should stay as aliens and (?) . ***Applause from the adience***

Something else is equalization of land, we don't want land to be equalized. Some people are saying that each person in Kenya

should have 50 hectares of land and some people say 25 hectares. We, the Maasai say let them live in their own communities, but not in Maasailand. *Applause from the audience.* So we want to own our land as much as we want, because we are different from them. One thing they should know is that Maasais are indigenous, they are minorities and marginalized. So, in this draft constitution we must put a clause, like the way you have empowered women and children and people with disabilities, you must see that the Maasais, the Ogiek and other communities also have a right to own land because it is not there, it is just the minority. Who are the minority? The Maasais are the minority. It is Maasais, Ogiek and other tribes in the community. Thank you very much.

Applause from the audience.

Maurice Ole Raria: Thank you very much. Ukiangalia, ninahakika kwamba anaelewa Katiba vizuri sana na kwamba he is talking from a very informed position. Na kile ninaweza kukuomba tafadhali hebu unakili hayo maoni yako kwa maandishi, kusudi umpatie district co-ordinator ili tupate hayo maoni kule Nairobi ifikapo tarehe ishirini na mbili ili Commissioners waweze kuzungumzia haya mambo tarehe ishirini na nane. Tafadhali make sure that is included.

Eeh ni lazima pengine kila mtu awe na fifty hectares kwa sababu kuna concept ambayo pengine kuna watu wengine wanaelewa inaitwa land carrying capacity. Kwa sababu ukisema, ukiangalia akari mia moja katika sehemu za Narok, the value of that land ni chini ya quarter of an acre katika Kiambu District. Kwa hivyo Katiba ikisema equalization of land, kuna hilo jambo la land carrying capacity ambayo ni lazima izingatiwe. Kwa sababu kuna ardhi zingine ambazo zinaweza kuwa kidogo ukipima on the ground lakini ukiangalia ile value yake ni ya juu. Na sehemu ya Maasaini ambayo inaonekana ni ardhi kubwa sana lakini ile value yake ni ya chini.

Kwa hivyo, equalization of land haimaanishi kwamba pengine ni acreage 50 na kila mtu awe namna hiyo. Kwa hivyo lazima muelewe pia hiyo concept ya land carrying capacity. Nafikiri kuna wengine wananielewa.

Response from the audience: Tunaelewa.

Speaker: (inaudible) hebu tupatie definition ya idle land.

Maurice Ole Raria: Asante sana. Pia juu ya idle land, katika mjadala wakati ma Commissioner walikuwa wanajadilia juu ya hiyo concept ya idle land, ilisemekana kwamba hakuna idle land, hasa kwa sehemu ambapo watu wanafanya kufuga mifugo, kwa sababu sehemu ambazo hawaishi ni sehemu ambazo wanalisha mifugo wao. Kwa hivyo walisema hakuna mambo ya idle land hasa kwa sehemu ya watu ambao wanategemea mifugo kwa hali ya maisha yao. Kwa hivyo hiyo concept ya idle land haiko kabisa.

Applause from the audience.

George Nakholi: Asante sana. Sasa number 4.

Jonathan Ole Ronko: Kwa majina ninaitwa Jonathan Ole Ronko kutoka sehemu za Lamek, Narok.

(Interjection) **Maurice Ole Raria:** Jonathan?

Jonathan Ole Ronko: Jonathan Ole Ronko. Kwanza ningependa kuwashukuru nyote kwa kufika kwenu, kwa sababu huu mswada tumeuonjea kwa hamu sana. Kwa hivyo mkirudi kule head quarters, muwaambie wale watu kuwa tunawaunga mkono kwa dhati kabisa kwa maana hii Constitution mpya ina faida kwetu na italeta mabadiliko zaidi. Kwanza ningependa niongea kwa lugha ya mama na ya Kiswahili.

(In vernacular) *Applause from the audience* (in vernacular) *Applause from the audience*. (in vernacular). Sasa wacha niongee kwa Kiswahili kidogo. Nimegusia kwanza ahadi ya miaka, mimi ninasema kwa maoni yangu, hiyo ni ishirini kwa maana huo muda ni mrefu.

Kuhusu wanyama, wanyama kwanza wanatuletea shida sisi watu wa upande wa Lamek kwa maana sisi hatulimi na tuna uwezo wa kulima na tuna uwezo wa kulima lakini ukilima ni kama ndovu wanangoja tu kuja kuvuna. Nay o hiyo pia iangaliwe kwa maana watu wakiamuwa kuwa piga wanyama ati wanafungwa. Kwani inamaanisha ndovu wanapatiwa license ya kutuuwa kwa nini sisi hatuwapigi?

Hii hali ya mashamba, watu wawe wana equal shares kwa maana mashamba ambayo ni ya pande hii imechaguliwa lakini watu bado wanamashamba zaidi, hiyo pia iangaliwe. Kama bado kuna uwezo wa kurudishiwa, turudishiwe na iletwe kwa committee watu waje wajadiliane wenyewe. Asanteni.

Maurice Ole Raria: Asante Bwana Ronko, tumenakili maoni yako.

George Nakholi: Number 5.

Supeiyo Ole Lelei: Asante sana Bwana Commissioner. Kwa jina mimi ninaitwa Supeiyo Ole Lelei.

Maurice Ole Raria: Nani?

Supeiyo Ole Lelei: Supeiyo, Ole Lelei kutoka hapa Lamek. Kwanza kwa maoni yangu, ningependa kuunga mkono kwamba

mambo yale yule jamaa amesema, our land should not be taxed, kamwe! Kwa sababu sisi ni watu ambao tunachunga ng' ombe, tunafuga, hatuna ma plot, kama wengine wanasema land, nchi ambayo inakaa hakuna kazi inafanya... ai!

Maurice Ole Raria: (*in vernacular*)

Supeiyo Ole Lelei: (*In vernacular*) trust land huwa inaangaliwa na County Council ya area. Itolewe mara moja! Iende kwa community, kwa sababu ukijaribu saa hii kuangalia Mau Forest, it is out na wenye community hawajui. Imefanywa hivyo chini ya central government kupitia kwa County Council na ardhi imeisha bila wenyewe kujua. Zipelekwe kwa wenyewe. Iwe kama kitu ambacho ni cha watu wote kinatumika, kiwe kinatumika na wenyewe ndio wameongea wote na kupatiana, lakini not individuals (*in vernacular*).

Inginge, selling of land, ardhi ya zamani. Kama mimi Lelei niko na watoto, mimi niandike shamba na bibi yangu lakini sio kwamba mimi niwe na shamba, bibi hana shamba, mimi ninaenda ninauza shamba na ninawaacha watoto wakikaa hivyo, no. Tuwe very, very clear. (*in vernacular*) **Applause from the audience**

Lingine ni juu ya titles, ma titles unapata imechukuliwa hata title mbili kwa shamba moja, very wrong. Title mbili kwa shamba moja! Hii shamba itaenda kuwa ya nani? Lelei ako na title, (?) aka na title the same land! Itakuwa ya nani? Tutafanyaje? Hiyo ni swali na imeingia. Ianfgaliwe the first one ambaye alichukua hiyo title iwe yake, yule amekuja kuwekelewa (*in vernacular*). Asante.

Speaker: (inaudible) baada ya miaka miwili au moja, they divorce na mmeandikiwa hii title, na hamjapata watoto na mme-divorce itakuwaje?

Supeiyo Ole Lelei: Sawa sawa, hiyo mimi nitajibu. Hiyo umemtoa huyo msichana kwao na mmekuja mkakaa, mkaoana, kama mta-divorce mtoe!

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: Ninaweza eh, ngoja kidogo, ninaweza kukujibu. Ningependa kukujibu kuhusu kama umeoa halafu mfanye divorce, kwanza kama uko na nia ya kumpatia bibi yako talaka, kama uko na nia ya kusema kwamba nitamo lajini pia tena unafikiria ya kwamba utamdivorce ili pia aweze kunyakua ile title, inasemekana ya kwamba iwapo umemoa huyo bibi na mko na title moja, kwa sababu kwa ndoa hata haupaswi kufanya talaka na hata Wamaasai hawatambui talaka ama kupatia bibi divorce. Kwa hivyo ukim-divorce ukiwa na sababu zako, basi atakuwa pia ana haki katika sehemu ambayo imebaki. Kwa hivyo hautafanya talaka.

Speaker: Swali, na wakianza biashara? Mimi ninauliza tu (inaudible) na kama ni biashara unarudi tena na unakuja “come-we-stay”, unaona umeandika halafu kesho anaenda kwa bwana mwingine kisha unakuja kugundua ako na mabwana watano...

(Interjection) **Maurice Ole Raria:** Asante sana, jambo la ‘come-we-stay’ sio ndoa.

Speaker: (inaudible).

George Nakholi: Okay, wacha tumpatie nafasi aulize.

Speaker: (*in vernacular*)

Noise and murmuring from the audience

Speaker: Sasa ningependa kujibu hilo neno halafu nisikilize kwa maakini ya kwamba umejua umeenda kwa baba yangu na mimi kwa Wamaasai mnaoa sisi tukiwa watoto wadogo, sasa shida ndio hiyo. Inaenda (inaudible) miaka inaenda, inaenda ishirini unarudi unaniambia...

(Interjection) **Speaker:** (inaudible).

Noise and murmuring from the audience

Speaker: Sasa nimesema yenyewe huyu mzee ni wangu na amenioza, na amenitoa kwa baba yangu nikiwa mtoto mdogo sana. Anakuja amenivuruga na maisha imekwisha, halafu ananiambia ati niende, halafu aoe mwingine. Kama anataka kuo yeye ndiye anajua watoto wake na mzigó wake, mimi anipatie haki yangu, nikae huku, nizalie huku na hata kama hanipendi ni yeye ndiye amenileta. Akirudi alete mwingine ni shauri yake...*Applause from the audience* kama anauwezo. Kwa hivyo mimi ninaonelea...

Noise and murmuring form the audience

Maurice Ole Raria: Tafadhalini, mpatie mama nafasi yake kwa sababu hata wewe ukizungumza utapewa nafasi yako. Tafadhalini tuheshimiane.

Speaker: Kwa hivyo vile mimi ningonelea kwa wakati huu, nyakati ingine imepita. Kwa katiba ya saa hii, oa, somesha mtoto na sasa hutaambiwa usomeshe mtoto, utaambiwa usomeshe mtoto kwa nguvu. Oa bibi mmoja akuzalie, ukae na yeye,

uni-divorce unipe haki yangu kaa na watoto wako.

Maurice Ole Raria: Basi tafadhali kwa sababu ninataka... Kwanza tafadhali ngoja niwaeleze. Ijapokuwa tuko katika mjadala, ningependa pia kuwaambia msimamo wa katiba kuhusu jambo kama hilo. Msimamo wa katiba unasema kwamba ikiwa umemuoa bibi kwa halali na kama mtakuwa mnashikilia title, itakuwa ni haki yenu nyinyi wawili. Na iwapo pia utamwoa bibi mwingine kwa njia ya halali, basi (*in vernacular*).

Noise and murmuring from the audience

Speaker: (*in vernacular*).

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*) matters of detail. Hii katiba haiwezi kuzungumzia, kuna mambo mengine yatazungumziwa kutokana na legislation, kwa mambo ya legislation na pia kwa mambo ya policy. Na pia tumesema ya kwamba kutakuwa na serikali ya vijiji, na kazi yake hasa ni kuzungumzia mambo kama hayo, mambo ya details.

Applause from the audience.

Maurice Ole Raria: Kutakuwa na serikali ya kijiji. Kwa kusema kweli hata tukienda kwa judiciary, mtakuta ya kwamba kuna village tribunals. Katika korti, tafadhalini hebu tuelewane... Mkiangalia katika structure ya korti sasa, itakuwa hali ya juu kabisa, itakuwa na Supreme Court, halafu ifuatwe na Court of Appeal, kisha High Court, kutakuwa na Magistrate's Court halafu kutakuwa na village tribunals.

Na mambo ya hizo tribunals na hiyo village government yatakuwa yakishugulikiwa katika hizo tribunals. Kwa hivyo mambo ya details tafadhali hebu tuache ili tuweze kuenda katika mambo mengine.

Speaker: (*in vernacular*) **Applause from the audience**

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*).

Speaker: Huyu ni number saba.

Speaker: (*In vernacular*).

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*).

Speaker: Number nane.

Solomon Ole Santai: (*In vernacular*).

(Interjection) **Maurice Ole Raria:** (*In vernacular*).

Solomon Ole Santai: (*In vernacular*). Ya kwanza, tuko na shida sisi Wamaasai sana hasa kwa upande wa uhuru ambao alipatikana hata kabla wengine wetu hapa hawajazaliwa. Shida hiyo inatokana na sababu hii, kwanza upande wa mawe, matunda yakipatikana kama upande wa barabara tena lami, kuna lami imekuja kutoka Nakuru na kufikia mwisho wa lami. Na sisi Wamaasai kama tungkuwa na barabara nzuri, tungesomesha watoto na hata hatungeweza kuuza hiyo ardhi kwa sababu nchi yetu ina rotuba sana. Ambayo iko na maziwa na kama tungkuwa na barabara nzuri hata saa hii, Narok nzima ingekuwa inalisha nchi. Maziwa ingeweza hata kufika Mombasa kwa sababu huko ni pahali hakuna au hawapati mvua.

Jambo la pili ni hali ya kilimo. Hapa ni mahali ambapo viazi vinaingia na mboga na hata pande ambayo inatoa mamilioni ya pesa. Na ukiangalia haya mambo ya barley haitufahidi sisi kabisa. Kwa sababu hata wakati wa kiangazi hatupati hata kile kitu tunaita stage one ya kulisha ng'ombe. Inakosa na hakuna mahali hata waajiri wa... kwa sababu nikifikiri watu wameajiriwa na Kenya Breweries kama wafanyikazi ni maelfu na hiyo barley inatoka kwetu. Kwa nini hiyo barley haiwezi kuwekwa mahali kama Purko ama mahali pengine ambapo Wamaasai ambao ndio wanakuza, wangeajirwa huko na kufanya hiyo kazi? Na hapa kama ingekuwapo, watu kama elfu nne ama tano wangefanya kazi kwa hiyo Kenya Breweries na ingefaidi Wamaasai.

Applause from the audience. Hata stage ya kwanza ile ya kulisha...

Speaker: Inyoroshwe kabisa! Kwa sababu ya hiyo basi sasa tunashindwa. Unashindwa hii ni Narok, hii ni Nakuru, inaendaje? Hizi corner, corner hizi, tunataka zinyoroshwe. Inatakikana mweke kwa hiyo review hicho kitu kinyoroshwe.

Kitu kingine ni grabbing of land. Wale watu ambao wamenyakua mashamba ya Wamaasai, imekuwa ni wakubwa hapa. Mtu analetwa kutoka kwao anakuja kuwasimamia na kuwachunga Wamaasai, halafu yeye anakuja ku-grab. Sana, sana officers wa serikali ndio wana-grab. Unakuta mahali tumetenga, tumetanga mahali ya kupanda miti, wanaweka nyumba ya gorofa, wana-grab. Na D.C. ndiye anasimamia kwa sababu ndiye Chairman wa Town fulani, ndiye Chairman wa kupeana plot. Tunataka plots ziwe zinasimamiwa na watu wenyewe na chairman awe ni mmoja wa Wamaasai ambaye tumemchagua sisi wenyewe. Kwa sababu tunashida sana, tumetatizika hapa zaidi.

Kitu kingine ni forests. Mambo ya forests mlisema zingine zinasimamiwa na County Councils na zingine zinasimamiwa na serikali. Tunataka hizi forests zirudi kwa wenyewe, kwa sababu hata County Councils siku hizi hatuwaamini. Wengine

wananunuliwa tu, na kwingine watu wengine wanaingia tu halafu unakuta D.C. pia ndio member kwa mambo ya forests. Anawezaje kuwakataza watu na labda analeta ndugu yake kutoka pale. Hatutaki hiyo pia, tunataka forests zirudi kwa wenyewe. Wamaasai wenyewe wachunge hizo forests zao.

Kuna kitu kimeongewa hapa na ni kitu cha ajabu sana. Haya mashamba ya Naivasha, Wamaasai kutoka area hii yote wanapita Naivasha, hakuna mtu mwingine pale. Lakini Wazungu wameenda kufunga, na wakubwa wengine Waafrika, ambao wamekuwa wazungu weusi, wamefunga njia hakuna sasa njia mahali watu wanaweza kupita wakiapeleka ng'ombe wao kunywa maji. Na hakuna mtu, na wanasema kuna mtu. Na serikali hajatupatia maji ya kunywa. Tunaomba kuwa pia hizo njia *zifunguliwe* ili ng'ombe wa Kimaasai waende kulishwa Naivasha kwa vile hapo ndipo pahali kuna maji katika area hii yote, vili mzee mmoja aliongea hapa, Councillor. Kwa hivyo kwa hiyo tunataka kuweka mkazo kuwa njia za maji *zifunguliwe*. Asante sana.

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: Asante sana. Jambo ambalo ningependa kuwakumbusha wananchi ni kuwaambia ya kwamba, wakati tutakuja kuongea juu ya mambo ya devolution, juu ya mambo ya kuleta utawala kwa districts, kutakuwa na District Council. Kwa sababu wananchi wamelalamika kuhusu ma afisa wanaotumwa kutoka Nairobi, halafu wanakuja katika sehemu za jamii na wanakuja kufanya mambo ambayo hayakubaliwi na jamii. Mtakuja kuona ya kwamba hizo District Councils ambazo zitakuwa hasa serikali italetwa kwa District Councils. Watakuwa na nguvu ya kuwaajiri watu kutoka kwa district yao. Kwa hivyo hamtakuwa na shida ya watu kutoka nje, kuja kunyakua ardhi zenu ama kuharibu mali yenu.

Simeon Lemurusu: Asante Bwana Commissioner. Kwa jina ninaitwa Simeon Lemurusu kutoka Lamek Ward, na mimi ni Councillor wa area hiyo. Kweli mengi yamesemwa lakini kidogo tu, ningependa kufanya repetition kidogo na ninaomba uniruhusu niendelee kidogo.

Kuna kitu kinaitwa (inaudible) land ni life. In any way tukiishi, tukifuta hewa, chakula tunapata katika ardhi. Kwa hivyo, ardhi ni baba au ni kitu ambacho kiliumbwaa na Mungu ili binadamu wote wafaidike nayo. Kweli, imesemekana kuna land grabbing, land grabbing imeingia hapa na immeanza na wakubwa huko mpaka hapa hata wadogo wameingia. Laini hii imeingia kwa ajili land officers, registrars wameanza kutoa titles mbili. Katika district hii kuna watu ambaa wako na titles mbili ya shamba moja. Na hii ni njia moja ya ku-grab land bila mtu kujua, hata za wengine zinauzwa.

Kitu kingine kipo ambacho tunaita land lease katika nchi yetu, hapa Maasaini. Sisi ndio wenyе ardhi, lakini chakula ambacho inatoka huko, mavuno yanayotoka huko na pesa zinatoka huko, zinaenda, zinapelekwa na wahindi. Serikali imetutupa sisi, kwa vili ardhi hii ni yetu lakini hatufaidiki nayo. Kama ni laws zinatengwa, (inaudible) kama ingekuwa hivyo, bado inaenda kwa watu wengine ambaa wanamiliki, ambaa sio wenyе mashamba. We are being milked by the foreigners. Kwa

hivyo, ardhi hii yetu ichungwe sana. Hapa tuna ninety nine years, hii ni lughya nani? Ni ya white people. Tangu Wamaasai kutoka kwa tumbo ya mama yake, wale ambaao walikuwa huko, hawajui ninety nine years ni nini. Kwa hivyo so long as sheria imejulikana imetoka wapi na inaelekea wapi, hii tu kuchukua first title (inaudible) inherited by the family line na kusiwe na ninety nine years ambazo zitabidi baadaye tena niende ku renew, hiyo tumekataa.

Kulingana na haya mambo ya colonial masters, ardhi hii, kwa mfano mliposikia Laikipia, pande za Marsabit, Nakuru na hata Nairobi hapo zamani, iliponyakuliwa ilijulikana kwamba inatoka kwa watu fulani, watu wa mlango fulani au clan fulani. Je kama inawezekana, chochote ambacho saa hii wazungu wanacho, zile big ranches ambazo wazungu wanazo, zinapokwisha hizo ninety nine years ambazo zimekuwa ni kitu kama kikwazo, basi ardhi irudi kwa original people, owners, bila condition yoyote.

Nikiendelea kidogo, kuna kitu ambacho kinaitwa kiosk, kiosk inaonekana, mtu ye yeyote akija hapa anasema wacha nipayate kiosk.

Maasaini mheshimiwa, kiosk hakipatikani kwa central. Na kwa vile hiki kitu mmetupatia, hati hii hata ingawa imetokea, haikulengwa pahali pengine, inalengwa Maasaini kwa ajili Wamaasai ndio bado wana ardhi, na ardhi hii tuachiwe sisi. Yule mtu ambaye anaona anataka pahali pa kuishi, kwa vile inaonekana watu wanataka kutafuta tu pahali pa kuishi, waedelee kujenga gorofa zikielekeea mbinguni pahali hakuna mtu anang'ang'ania kupata.

Sina mengi ni hayo tu nitasema, tuko pamoja na nyinyi na sheria hii itulinde sisi Wamaasai kwa ajili sisi ndio tumebarikiwa kuwa na resources hizi. Kama wanyama kwa mfano, hakuna pahali unaweza kupata 300,000 hectares ya ardhi ambayo inapatikana pahali pale wanyama wanafugwa. Na ardhi kama hiyo iangaliwe sana isiende kwa watu wengine bali ibaki na wenyeji ambaao ni sisi Wamaasai. Sina mengi kuhusu hayo.

Nikiendelea kwa mambo yale ambayo mnasema kuhusu nini...

Speaker: Ya local... Commissioner atatusaida kuhusu hiyo.

Simeon Lemurusu: Ooh, sawa nilikuwa ninataka kuendelea.

Maurice Ole Raria: Ningependa kuwaomba kwamba hoja ambazo mtatoa, mjaribu kabisa msirudie jambo ambalo limezungumziwa. Mambo ya lease yameshazungumziwa, mmeamua ni miaka thelathini na tatu. Kwa hivyo mambo kama ya lease, hayo tafadhali msirudie. Lile jambo ambalo utazungumzia liwe ni hoja ambayo ni mpya kabisa.

Speaker: (*In vernacular*).

Rael Ologoyiero: Asante sana. Mimi ninaitwa Rael Ologoyiero. Nimesikia ambayo yale mmeongea kuhusu ardhi na nimeyapendelea sana. (inaudible)

(Interjection) **Speaker:** Ongea ukitumia microphone na upaze sauti.

Rael Ologoyiero: Mimi nitaongea kuhusu mambo ya ardhi, kwa sababu wakati ambao mlipata taabu ndio sisi pia tulipata taabu. Ninaongea kuhusu ardhi ambayo tulinyang' anywa na wabeberu. Sijui wengine wanasesma ati sijui ati iko pahali ambapo pamechukluliwa, wameshajenga, wakati ambapo wametuhamisha sisi kweli hatujajenga? Si nimejenga kama hao? Hata kama ni nyumba ya udongo. Kuhusu hiyo ningetaka waturudishie sisi ardhi yetu.

Jambo la pili, wakati wa wabeberu tulijua kule beacons ziliwekwa. Sasa hakuna beacons, tunaona tukipotea (inaudible). La tatu, mimi nimesikia umeongea mambo ya ardhi. Kuna pahali panaitwa Maasai Game Reserve, na ni nchi ambayo unajua sana. Kweli sisi tuna serikali, tunasikia ati wanyama wakiua mtu ati analipwa elfu thelathini, na wakati wewe mwenyewe ukiguza mnyama, hata wanaua roho yako, roho ya kibinadamu. Ikiwa mnyama ameua binadamu, analipwa shilingi elfu thelathini. Si hiyo ni kinyume cha haki zetu? Pia ninataka kama wanyama wanaumiza mtu, alipwe kama milioni kumi!

Applause from the audience Nitakomea hapo kuhusu hayo mambo ya kuwalipa binadamu wanapoumizwa na wanyama na ambao wanatakikana kulinda ardhi yetu.

Na kama ninataka kulinda, ardhi kwa sababu kila pahali kuna wakili, hata kama sisi ni Maasai, lazima tukitaka, tukitoa (?) hata kina mama, si mmekwenda kuleta msichana wa mtu? Ni kulewana, na kwa nini unaandika kwa title deed jina langu pekee yangu na ni sisi wawili tunajenga hiyo boma pamoja? **Applause from the audience.** Lazima mkiandika title deed, bibi yako anasimama hapa, karibu na wewe. Ukitaka kuuza, muuze pamoja na mkikosa mnunuzi, mkose pamoja.

Applause from the audience. Jambo lingine permit iko, permit... Ndugu zangu (inaudible) hatua akichukua halafu asiuze title deed, msiuze ardhi. Nikiuza ardhi kuna permit na lazima utajulisha wakili awe anasimamia hiyo shamba wakati mtauza akuje kueleza matatizo alipata halafu apate kuuza. Sio ati yeye anaondoka, sisi tumekuwa wazee sasa, sio ati unaenda kuuza ardhi, lazima muwe pamoja.

Jambo lingine kuhusu ardhi (inaudible). Lakini kila mtu yuko na nyumba yake ambayo alijenga. Wakati Mungu alitupa sisi ardhi alisema Wamaasai wakae hapa, Kalenjin wakae hapa, Turkana wakae hapa. Hicho kitu ndicho kinawasumbua Wamaasai sasa, sana. Wengine wanawaingilia wengine, kuwanyang'anya ardhi yao na vile I see it, sio mbaya kununua. Kama mmeshaongea na kusikilizana na kuamua huyo mwagine akubali anunue si ni sawa? Hata kama ni Mkalenjin hata kama ni nani, hata kama ni nani. Lakini kutuingilia sisi na kutoa wengine, iko wengine wanakaa Torten Maasai, (*In vernacular*). Ati kuamisha Wamaasai ndani ya... **Applause from the audience** kwa ardhi yao! Hiyo ni njia ya kunyang'anya mtu. Hiyo isimamishwe na kila mtu ajue ni ardhi ya wenyewe ambayo tunaenda kuomba pole pole au kununua kwa njia ya amani.

Msitu, ningependa kuongea juu ya misitu. Lakini hiki kitu nyinyi mnachekelea, haya maendeleo ya juzi juzi

(?) hata nyinyi mnasema “ni maendeleo, maendeleo”. Zamani Maasai hakuna... hata ni dhambi sisi kukata ardhi! Mungu alitoa ardhi kwa kila mtu, hakuna ati kukata, lakini maendeleo kama yatapatikana basi sawa sawa. Lakini tukikata misitu, wakati sisi Wamaasai wenyewe tulikuwa tunachunga, hatuwezi kufyeka namna hii, hata tunafyeka (*in vernacular*), hatuwezi kufyeka namna hii. Wamaasai watatoa nyumba, Wamaasai watanunua fimbo, na siku hizi wamekuwa kama ng’ombe, wanafyeka tu misituni mpaka saa hii sisi hatuna maji uko Magadi. Kwa sababu wamefyeka, hiyo hiyo ardhi (?) wenyewe wachunge haki yao. (?) iende kwa D.C., iende kwa polytechnic, iende kwa (?) iende kwa ... wacha wenyewe wachunge na kama watamaliza ni shauri ya nani, si ni yao? Yangu ni hayo tu, nimemaliza.

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: Asante sana. (*In vernacular*) maoni yako ni mazuri sana na nimefurahia sana mambo mawili ambayo umezungumzia. Kwanza ni juu ya mazingira, umesema kwamba tusema kama ni misitu iliyo katika sehemu ya jamii, ni jamii hiyo inapaswa kulinda. Na ukienda katika sura ya kumi na mbili(12) ambayo inahusu mazingira na mali asili, imesema kwamba kila mtu nchini Kenya, anawajibu wa kulinda na kuendeleza mazingira. Kwa hivyo itakuwa ni juu yako mwenyewe katika sehemu uko ama katika sehemu ambayo jamii yako iko, mhakikishe kwamba ni nyinyi ambao mnaangalia mazingira na sio watu wengine kutoka nje.

George Nakholi: Basi, nitawaomba mkija hapa mchukue muda mfupi ili tuweze kuendelea mbele. Na lile jambo ambalo limezungumziwa, tafadhali wachana nalo. Tutaita watu kumi, nafikiri tutakuwa ni kama tumemaliza na nitajaribu kuwahimiza kina mama pia watoe maoni yao, tusije tukawaacha nje. Tutanzia number1, huyu mama hapa, yule mzee number 2, mzee hapa number 3, mama hapa number 4, number 5 last, number 6, mama mwengine, kina mama wako wapi? Mama? Haya number 7, number 8, kwa corner ile number 9, hapo mzee, wewe number 10. Tumalize na hawa, basi muwe haraka, tumalize haya mambo.

Hellen Kipetu: Asante sana ma Commissioners na wale wananchi wetu wako hapa. Mimi ninataka kuzungumzia kidogo kwa sababu watu wamezungumza sana. Ninataka kuzungumza mambo...

(Interjection) Speaker: (Inaudible)

(Inaudible)

Hellen Kipetu: Mimi ninaitwa Hellen Kipetu, na mimi ni nominated Councillor hapa. Ningependa kuzungumza juu ya haki za kina mama katika umilikaji wa ardhi. Ningependa kusema kwamba kina mama ambao ni widows, wananyanyaswa sana na community na hawa kina mama hawapewi haki zao. Unakuta mzee akifa kwa familia, mama, wazee wale ambao ni ndugu za mzee wake ndio sasa watakuwa wanahaki ya kumiliki ile ardhi ama wanaifanya hiyo ardhi vile wanataka. Ningependa kusema kuwa iwe automatic kwamba mzee akifa, mama directly hiyo ardhi ni yake. Na hata hakuna maneno ya kusema ati unaenda kuchukua letter of administration, automatically ardhi hiyo ni vako na watoto wako.

Ile ingine ninataka kusema hata wale orphans, unapata huu ugonjwa wa Ukimwi, watu wanakufa sana. Mama anakufa na baba anakufa. Unakuta tena saa hizi ndio watoto wanaumia sana. Ningependa tu kusema hiyo ardhi ama whatever property ambayo imeachwa, ikuwe directly inherited na watoto na isiwe ati kuna ndugu wa mzee ambaye anasimamia hiyo familia. Kama ni title ama ni kitu fulani kiwe ni cha watoto, hata kama serikali itachunga mpaka watoto wakuwe wakubwa, serikali ichunge ili watoto hao watumie hayo mali.

Kile kitu kingine ambacho ningependa kuzungumzia ni hawa foreign buyers. Sijui tutakuja kuweka katika sheria vile ninasema kwa sababu, hapa Umaasaini kuna wazungu wengi sana na wahindi, wamenunua ardhi ya Wamaasai. Sijui tutaweza kuwekaje katika Katiba, ili mtu mwingien aje aseme vizuri kwa sababu sielewi. Ili tuweke katika Katiba ili Wamaasai au wale watu ambao wameuza kwa sababu wengine wameuza blindly, ili hiyo ardhi iweze kurudishwa kwa Wamaasai. Kwa sababu unakuta mtu anauza even 1,000 hectares, hana hata chochote na sasa ye ye anaranda randa tu, hana pahali, na watoto wake sasa ni kama orphans.

Kile kitu kingine ambacho ninataka kuzungumzia kwa sababu ya saa, ni land office. Hizi ofisi za land na survey office wananyanya sana Wamaasai. Unakuta hawa watu hata kuenda kupima shamba na iko ile pesa ya serikali tunalipa tunarudi kunyanyaswa mpaka inabidi ulipe pesa zaidi ni kama unanunua shamba na ni ardhi yako unaenda kupatiwa. *Applause from the audience.*

Na kwa sababu labda sitapata nafasi nyingine ya kuja hapa kuongea, ningependa tu kuongea juu ya environment kidogo tafadhalii. Nataka tu kusema hawa watu ambao wanalease mashamba ya Wamaasai hapa, wanapollute environment. Sasa umekuta pahali kwingine hata hakuna ndege, hakuna hata nyuki kwa sababu ya vile wanaweka hayo madawa yao, wana spray na hawajali. Unakuta ndege inakuja inaspray hata watu wakikaa chini. Kwa hivyo ninataka tu kusema hiyo iangaliwe kwa sababu labda sitakuwa na nafasi ya kuja hapa tena. Asanteni sana.

Maurice Ole Raria: Asante sana Councillor. Kwa kusema kweli amezungumzia mambo ambayo ni ya muhimu sana. Hasa kama tungepata nafasi kwa sababu niliwaambia kuna mambo mengi sana katika Katiba hii na hatuwezi kuyazungumzia yote. Lakini kwa sababu ameongea juu ya mambo ya environment, hata hii shida ilionekana sana katika sehemu ya Kajiado kwa sababu mnajua kuna quarries, kama Kipini Quarry. Portlands wakifanya ile quarrying wanaacha sehemu hizo zikiwa ni mbaya sana.

Lakini katika Katiba hii, hao private developers ambao wanakuja kutoa madini hapo, watakuwa chini ya sheria ili baada ya kufanya tuseme kama ni quarrying ama baada ya kufanya kazi ambayo wanafanya katika sehemu hiyo, itakuwa katika sheria hii, katika sheria imetolewa na Katiba, ni lazima wa-reclaim ile land. Kabla hawajaacha hapo kwenda mahali pengine, ni lazima wafanye reclamation na kwa community wahakikishe ya kwamba wamefanya reclamation ya kutosha ile wawzeze kuenda mahali

pengine. Kama hawajafanya hivyo, basi watashtakiwa katika korti kuu ama Supreme Court, ambayo Katiba hii imebuni.

Speaker: Asante sana. (*In vernacular*) **Applause from the audience** Hawa watu wakora wako hapa. Ndugu yangu mimi niko na uchungu, mimi ninauzo (*in vernacular*) mpaka ninashtuka sana. Na ni shamba wakibadilisha na ndugu zangu, sio kununua au kuuza, ni kubadilisha tu. Unahakikisha mimi (*in vernacular*) nimekuta tu Ksh 30, 000. (*in vernacular*).

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*).

Applause from the audience

Lerionka: Bwana Commissioner, wazazi na watu wengine hamjamboni. Kwa jina ninaitwa Lerionka Ole Mairbe, ninafanya kazi na NGO, mambo ya Civic Education katika Narok District. Jambo langu la kwanza ni kusema kwamba kwa kifupi no tax on idle land. Kwa sababu wengine wanasema kwamba Maasai land ni idle land, kwamba hakuna kitu kinapandwa, hakuna mimea inapandwa huko kwamba it is just idle.

Mimi ningependa kusema kwamba nchi ya Wamaasai sio idle kwa sababu kuna wanyama amba wanaishi kwa ardhi ambayo tuko nayo...**Applause from the audience** kama wildlife, elephants amba wana-interfere na watu huko na pia hiyo ni source of revenue from the tourism industry. Halafu ya pili pia kuna wanyama wa Maasai amba kama livestock wanakaa katika hayo mashamba. So that land is not idle, because our animals are grazing there plus the wildlife. Pia ninaweza kusema kwamba, 55% – 80% on the wildlife roams of private people's land not on reserves and game reserves.

Ya pili ni abrogation of the thirty three year leasehold by the community. Hii ni kusema kwamba hii leasehold ya thirty three years isiwe huko. Community wakivote, 30% of the community, waandike signature wavote, hiyo leasehold iwe abrogated, irudi back to the community. So it should just be temporary because thirty-three leasehold you must have a mortgage thirty years old but thirty years is very long. It should be renewable, for instance we consider like Narok North, if thirty people, 30% of the voters in Narok pass a vote and sign the memorandum, both the leasehold should go back to the community. So we should have a right to dissolve the leasehold.

Halafu ingine...

(Interjection) **Speaker:** (inaudible).

Lerionka: (inaudible) because even in the Katiba they say that we can recall a Member of Parliament. Members in the constituency vote 30% (inaudible) so that means that should also be added also in the list

(inaudible).

Then another thing is that 90% of the revenue from the Parks and Reserves should go to the community, 90%. Like for instance Maasai Mara Game Reserve, 90% of the revenue should come to the community not to the central government. Something else I would like to add on is the (?) . We know that everybody in Kenya eyes Maasai land because we have vital resources, our land is very productive, most people come to buy our plots of land. So we want to say that the people who are not Maasais they can come and stay with us but they should stay as aliens, not as citizens. They should stay as aliens and (?) . *Applause from the adience*

Something else is equalization of land, we don't want land to be equalized. Some people are saying that each person in Kenya should have 50 hectares of land and some people say 25 hectares. We, the Maasai say let them live in their own communities, but not in Maasailand. *Applause from the audience.* So we want to own our land as much as we want, because we are different from them. One thing they should know is that Maasais are indigenous, they are minorities and marginalized. So, in this draft constitution we must put a clause, like the way you have empowered women and children and people with disabilities, you must see that the Maasais, the Ogiek and other communities also have a right to own land because it is not there, it is just the minority. Who are the minority? The Maasais are the minority. It is Maasais, Ogiek and other tribes in the community. Thank you very much.

Applause from the audience.

Maurice Ole Raria: Thank you very much. Ukiangalia, ninahakika kwamba anaelewa Katiba vizuri sana na kwamba he is talking from a very informed position. Na kile ninaweza kukuomba tafadhali hebu unakili hayo maoni yako kwa maandishi, kusudi umpatie district co-ordinator ili tupate hayo maoni kule Nairobi ifikapo tarehe ishirini na mbili ili Commissioners waweze kuzungumzia haya mambo tarehe ishirini na nane. Tafadhali make sure that is included.

Eeh ni lazima pengine kila mtu awe na fifty hectares kwa sababu kuna concept ambayo pengine kuna watu wengine wanaelewa inaitwa land carrying capacity. Kwa sababu ukisema, ukiangalia akari mia moja katika sehemu za Narok, the value of that land ni chini ya quarter of an acre katika Kiambu District. Kwa hivyo Katiba ikitumia equalization of land, kuna hilo jambo la land carrying capacity ambayo ni lazima izingatiwe. Kwa sababu kuna ardhi zingine ambazo zinaweza kuwa kidogo ukipima on the ground lakini ukiangalia ile value yake ni ya juu. Na sehemu ya Maasai ambayo inaonekana ni ardhi kubwa sana lakini ile value yake ni ya chini.

Kwa hivyo, equalization of land haimaanishi kwamba pengine ni acreage 50 na kila mtu awe namna hiyo. Kwa hivyo lazima muelewe pia hiyo concept ya land carrying capacity. Nafikiri kuna wengine wananielewa.

Response from the audience: Tunaelewa.

Speaker: (inaudible) hebu tupatie definition ya idle land.

Maurice Ole Raria: Asante sana. Pia juu ya idle land, katika mjadala wakati ma Commissioner walikuwa wanajadilia juu ya hiyo concept ya idle land, ilisemekana kwamba hakuna idle land, hasa kwa sehemu ambapo watu wanafanya kufuga mifugo, kwa sababu sehemu ambazo hawaishi ni sehemu ambazo wanalisha mifugo wao. Kwa hivyo walisema hakuna mambo ya idle land hasa kwa sehemu ya watu ambao wanategemea mifugo kwa hali ya maisha yao. Kwa hivyo hiyo concept ya idle land haiko kabisa.

Applause from the audience.

George Nakholi: Asante sana. Sasa number 4.

Jonathan Ole Ronko: Kwa majina ninaitwa Jonathan Ole Ronko kutoka sehemu za Lamek, Narok.

(Interjection) **Maurice Ole Raria:** Jonathan?

Jonathan Ole Ronko: Jonathan Ole Ronko. Kwanza ningependa kuwashukuru nyote kwa kufika kwenu, kwa sababu huu mswada tumeuonjea kwa hamu sana. Kwa hivyo mkirudi kule head quarters, muwaambie wale watu kuwa tunawaunga mkono kwa dhati kabisa kwa maana hii Constitution mpya ina faida kwetu na italeta mabadiliko zaidi. Kwanza ningependa niongea kwa lugha ya mama na ya Kiswahili.

(In vernacular) *Applause from the audience* (in vernacular) *Applause from the audience.* (in vernacular). Sasa wacha niongee kwa Kiswahili kidogo. Nimegusia kwanza ahadi ya miaka, mimi ninasema kwa maoni yangu, hiyo ni ishirini kwa maana huo muda ni mrefu.

Kuhusu wanyama, wanyama kwanza wanatuletea shida sisi watu wa upande wa Lamek kwa maana sisi hatulimi na tuna uwezo wa kulima na tuna uwezo wa kulima lakini ukilima ni kama ndovu wanangoja tu kuja kuvuna. Nayo hiyo pia iangaliwe kwa maana watu wakiamuwa kuwa piga wanyama ati wanafungwa. Kwani inamaanisha ndovu wanapatiwa license ya kutuuwa kwa nini sisi hatuwapigi?

Hii hali ya mashamba, watu wawe wana equal shares kwa maana mashamba ambayo ni ya pande hii imechaguliwa lakini watu bado wanamashamba zaidi, hiyo pia iangaliwe. Kama bado kuna uwezo wa kurudishiwa, turudishiwe na iletwe kwa committee watu waje wajadiliane wenyewe. Asanteni.

Maurice Ole Raria: Asante Bwana Ronko, tumenakili maoni yako.

George Nakholi: Number 5.

Supeiyo Ole Lelei: Asante sana Bwana Commissioner. Kwa jina mimi ninaitwa Supeiyo Ole Lelei.

Maurice Ole Raria: Nani?

Supeiyo Ole Lelei: Supeiyo, Ole Lelei kutoka hapa Lamek. Kwanza kwa maoni yangu, ningependa kuunga mkono kwamba mambo yale yule jamaa amesema, our land should not be taxed, kamwe! Kwa sababu sisi ni watu ambao tunachunga ng' ombe, tunafuga, hatuna ma plot, kama wengine wanasesma land, nchi ambayo inakaa hakuna kazi inafanya... ai!

Maurice Ole Raria: (*in vernacular*)

Supeiyo Ole Lelei: (*In vernacular*) trust land huwa inaangaliwa na County Council ya area. Itolewe mara moja! Iende kwa community, kwa sababu ukijaribu saa hii kuangalia Mau Forest, it is out na wenye community hawajui. Imefanywa hivyo chini ya central government kupitia kwa County Council na ardhi imeisha bila wenyewe kujua. Zipelekwe kwa wenyewe. Iwe kama kitu ambacho ni cha watu wote kinatumika, kiwe kinatumika na wenyewe ndio wameongea wote na kupatiana, lakini not individuals (*in vernacular*).

Inginge, selling of land, ardhi ya zamani. Kama mimi Lelei niko na watoto, mimi niandike shamba na bibi yangu lakini sio kwamba mimi niwe na shamba, bibi hana shamba, mimi ninaenda ninauza shamba na ninawaacha watoto wakikaa hivyo, no. Tuwe very, very clear. (*in vernacular*) **Applause from the audience**

Lingine ni juu ya titles, ma titles unapata imechukuliwa hata title mbili kwa shamba moja, very wrong. Title mbili kwa shamba moja! Hii shamba itaenda kuwa ya nani? Lelei ako na title, (?) aka na title the same land! Itakuwa ya nani? Tutafanyaje? Hiyo ni swali na imeingia. Ianfgaliwe the first one ambaye alichukua hiyo title iwe yake, yule amekuja kuwekelewa (*in vernacular*). Asante.

Speaker: (inaudible) baada ya miaka miwili au moja, they divorce na mmeandikiwa hii title, na hamjapata watoto na mme-divorce itakuwaje?

Supeiyo Ole Lelei: Sawa sawa, hiyo mimi nitajibu. Hiyo umemtoa huyo msichana kwao na mmekuja mkakaa, mkaoana, kama mta-divorce mtroe!

Applause from the audience

Maurice Ole Raria: Ninaweza eh, ngoja kidogo, ninaweza kukujibu. Ningependa kukujibu kuhusu kama umeoa halafu mfanye divorce, kwanza kama uko na nia ya kumpatia bibi yako talaka, kama uko na nia ya kusema kwamba nitamoa lakini pia tena unafikiria ya kwamba utamdivorce ili pia aweze kunyakua ile title, inasemekana ya kwamba iwapo umemoa huyo bibi na mko na title moja, kwa sababu kwa ndoa hata haupaswi kufanya talaka na hata Wamaasai hawatambui talaka ama kupatia bibi divorce. Kwa hivyo ukim-divorce ukiwa na sababu zako, basi atakuwa pia ana haki katika sehemu ambayo imebaki. Kwa hivyo hautafanya talaka.

Speaker: Swali, na wakianza biashara? Mimi ninauliza tu (inaudible) na kama ni biashara unarudi tena na unakuja “come-we-stay”, unaona umeandika halafu kesho anaenda kwa bwana mwingine kisha unakuja kugundua ako na mabwana watano...

(Interjection) **Maurice Ole Raria:** Asante sana, jambo la ‘come-we-stay’ sio ndoa.

Speaker: (inaudible).

George Nakholi: Okay, wacha tumpatie nafasi aulize.

Speaker: (*in vernacular*)

Noise and murmuring from the audience

Speaker: Sasa ningependa kujibu hilo neno halafu nisikilize kwa maakini ya kwamba umejua umeenda kwa baba yangu na mimi kwa Wamaasai mnaoa sisi tukiwa watoto wadogo, sasa shida ndio hiyo. Inaenda (inaudible) miaka inaenda, inaenda ishirini unarudi unaniambia...

(Interjection) **Speaker:** (inaudible).

Noise and murmuring from the audience

Speaker: Sasa nimesema yenyewe huyu mzee ni wangu na amenioza, na amenitoa kwa baba yangu nikiwa mtoto mdogo sana. Anakuja amenivuruga na maisha imekwisha, halafu ananiambia ati niende, halafu aoe mwingine. Kama anataka kuoa yeye ndiye anajua watoto wake na mzigo wake, mimi anipatie haki yangu, nikae huku, nizalie huku na hata kama hanipendi ni yeye

ndiye amenileta. Akirudi alete mwingine ni shauri yake...*Applause from the audience* kama anauwezo. Kwa hivyo mimi ninaonelea...

Noise and murmuring form the audience

Maurice Ole Raria: Tafadhalini, mpatie mama nafasi yake kwa sababu hata wewe ukizungumza utapewa nafasi yako. Tafadhalini tuheshimiane.

Speaker: Kwa hivyo vile mimi ningeonelea kwa wakati huu, nyakati ingine imepita. Kwa katiba ya saa hii, oa, somesha mtoto na sasa hutaambiwa usomeshe mtoto, utaambiwa usomeshe mtoto kwa nguvu. Oa bibi mmoja akuzalie, ukae na yeze, uni-divorce unipe haki yangu kaa na watoto wako.

Maurice Ole Raria: Basi tafadhali kwa sababu ninataka... Kwanza tafadhali ngoja niwaeleze. Ijapokuwa tuko katika mjadala, ningependa pia kuwaambia msimamo wa katiba kuhusu jambo kama hilo. Msimamo wa katiba unasema kwamba ikiwa umemuoa bibi kwa halali na kama mtakuwa mnashikilia title, itakuwa ni haki yenu nyinyi wawili. Na iwapo pia utamwoa bibi mwingine kwa njia ya halali, basi (*in vernacular*).

Noise and murmuring from the audience

Speaker: (*in vernacular*).

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*) matters of detail. Hii katiba haiwezi kuzungumzia, kuna mambo mengine yatazungumziwa kutokana na legislation, kwa mambo ya legislation na pia kwa mambo ya policy. Na pia tumesema ya kwamba kutakuwa na serikali ya vijiji, na kazi yake hasa ni kuzungumzia mambo kama hayo, mambo ya details.

Applause from the audience.

Maurice Ole Raria: Kutakuwa na serikali ya kijiji. Kwa kusema kweli hata tukienda kwa judiciary, mtakuta ya kwamba kuna village tribunals. Katika korti, tafadhalini hebu tuelewane... Mkiangalia katika structure ya korti sasa, itakuwa hali ya juu kabisa, itakuwa na Supreme Court, halafu ifuatwe na Court of Appeal, kisha High Court, kutakuwa na Magistrate's Court halafu kutakuwa na village tribunals.

Na mambo ya hizo tribunals na hiyo village government yatakuwa yakishugulikiwa katika hizo tribunals. Kwa hivyo mambo ya details tafadhali hebu tuache ili tuweze kuenda katika mambo mengine.

Speaker: (*in vernacular*) *Applause from the audience*

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*).

Speaker: Huyu ni number saba.

Speaker: (*In vernacular*).

Maurice Ole Raria: (*In vernacular*).

Speaker: Number nane.

Solomon Ole Santai: (*In vernacular*).

(Interjection) **Maurice Ole Raria:** (*In vernacular*).

Solomon Ole Santai: (*In vernacular*). Ya kwanza, tuko na shida sisi Wamaasai sana hasa kwa upande wa uhuru ambao alipatikana hata kabla wengine wetu hapa hawajazaliwa. Shida hiyo inatokana na sababu hii, kwanza upande wa mawe, matunda yakipatikana kama upande wa barabara tena lami, kuna lami imekuja kutoka Nakuru na kufikia mwisho wa lami. Na sisi Wamaasai kama tungakuwa na barabara nzuri, tungesomesha watoto na hata hatungeweza kuuza hiyo ardhi kwa sababu nchi yetu ina rotuba sana. Ambayo iko na maziwa na kama tungakuwa na barabara nzuri hata saa hii, Narok nzima ingekuwa inalisha nchi. Maziwa ingeweza hata kufika Mombasa kwa sababu huko ni pahali hakuna au hawapati mvua.

Jambo la pili ni hali ya kilimo. Hapa ni mahali ambapo viazi vinaingia na mboga na hata pande ambayo inatoa mamilioni ya pesa. Na ukiangalia haya mambo ya barley haitufahidi sisi kabisa. Kwa sababu hata wakati wa kiangazi hatupati hata kile kitu tunaita stage one ya kulisha ng'ombe. Inakosa na hakuna mahali hata waajiri wa... kwa sababu nikifikiri watu wameajiriwa na Kenya Breweries kama wafanyakazi ni maelfu na hiyo barley inatoka kwetu. Kwa nini hiyo barley haiwezi kuwekwa mahali kama Purko ama mahali pengine ambapo Wamaasai ambao ndio wanakuza, wangeajirwa huko na kufanya hiyo kazi? Na hapa kama ingekuwapo, watu kama elfu nne ama tano wangefanya kazi kwa hiyo Kenya Breweries na ingefaidi Wamaasai.
Applause from the audience. Hata stage ya kwanza ile ya kulisha...

Speaker: Viazi lakini hata ukilima iwe gunia mia moja inaoza kwa shamba huwezi kula, huwezi kupatia mwenzako na inaletea sisi shida. Na hiyo ukipata mwaka huu, ulime pa upate mahali ya kuuzia kwa sababu ya barabara haikufaidi.

Ya tatu, ambayo ni kuhusu mambo ya katiba ya ardhi ambayo ndiyo inaendelea saa hii, ni kuhusu mambo haya ya ugawaji wa

ardhi. Sababu mahali tunatoka na nitapatiana example Oloputoi inagawanywa sasa Location mbili, kuna Naitipati Location. Na hiyo Naitipati Location, hakuna special purpose, hakuna mahali pa kuweka kama kiwanja cha tea ama mahali pengine pa kujenga shule, sababu haikujengwa. Na kama ilipokuwa hapo awali, watu walikuwa na maoni ya kutaka mahali kama hizo nafikiri ingeendelea mbele na kama sasa sababu mimi ninasikia watu wakiongea sana na wanajaribu, lakini unasikia mtu akiongea na ukijaribu kuangalia mahali anapotoka ye ye hajafanya chochote kama Masaai. Sasa, kwa sababu kuna mahali pengine pa Masaai ni ambayo haijagawanywa kama Mau Forest, mau Forest ingine iko na watu tuseme kama elfu ishirini ya wa Masaai amba wanataka kugawa hiyo ardhi na pengine haitoshi.

Mimi ningeomba kama hapo ingekuwa mahali pa kusaidia wa Masaai kwa jumla wapate mvua na wapate madawa na wapate kulisha ngombe zao wakati wa kiangazi.

Nakholi: Tuwe na mkutano mmoja.

Speaker: Na ile mahali ambayo inaangaliwa ama inatarajiwa kugawanywa, na hapo Bwana Commissioner ufikirie zaidi, hapo mahali tunatarajia kugawanywa sana iwe kusawanishwa, kusiwe na upendeleo, sababu ndiyo unakuta kuna mzozo, unakuta kuna mtu ana acre mia moja na mwingine ako na acre ishirini, sasa ugomvi utakosaje kuingia katika area hiyo.

Speaker: (in Masaai dialect).

Nicholas Ole Ndiya: (in Masaai dialect).

Translator: (in Masaai dialect)

Nicholas Ole Ndiya:

Nakholi: Nafikiri huyu ndiye wa mwisho kwa hii line, huyu ndiye wa mwisho.

Agnes: (in Massai dialect)

Raria: (in Masaai dialect) Nafikiri Bwana Nakholi tutakupatia nafasi uendelee kwa hicho kipengele kingine cha devolution ili tuweze kuendelea asante.

Nakholi: Asante sana Bwana Raria, vile tulisema mambo ya ardhi ndiyo yalikuwa mambo muhimu sana kwa jamii za Masaai, na ndiyo tulichukuwa muda huu wote kutoka saa nne na nusu mpaka saa nane na dakika kumi, saa hii sasa. Mnaona umuhimu wa mambo ya ardhi, kwa nyinyi na hamjachoka, watu bado wangeendelea lakini hatuma muda.

Kwa hivyo vile mmeambiwa, hiyo ndiyo ilikuwa jambo muhimu sana hata kwa sisi hata kwa Commission sasa tutaenda kwa mambo ingine lakini nitaenda haraka kwa hili jambo la kuleta utawala chini kwa wananchi. Inaitwa kwa Kiingereza devolution, sasa tutazungumzia hiyo kwa ufupi halafu muongee vile mtataka. Vile tulikuwa tunatembea tukienda round the country, tukienda kwa nchi tukiangalia mambo, tulipata watu wengi sana hata hapa nafikiri Narok North watu walilia sana mambo ya Provincial Administration, walilia sana wakisema hiyo inawanyanyasa hiyo sijui nini, inafanya hivi inafanya hivi. Na tunajuwa walikuwa labda na ukweli kwa mambo mengine na mengine labda hapana, lakini kwa ujumla watu walitaka Provincial Administration itolewe, walilia sana.

Tukiseme juu ya Provincial Adminsitration, sisi tunasema mambo ya Chiefs, Assistant Chiefs, DOs, DCs na Provincial Commissioner, hiyo ndiyo line up. Vile mnajua kwa ile katiba inayotoka sasa kuna ile kitu inaitwa Chiefs' Authority Act, ambayo inahusisha Chief peke na Assistant Chief peke yao, kwa sababu mkoloni alileta hiyo kuangalia maslahi yake. Kuangalia itafanya nini kwa wafrika wale wanatawaliwa na hao. Wale wengine mko hapa labda mumetembea nje kama Uingereza kama huko America hakuna kitu kama Chief au DO, au DC au PC hakuna, lakini walileta hii kwa sababu walitaka watumikiwe kwa sababu zao.

Kwa hivyo, watu walipoleta haya, Commission iliangalia ikasema watabadilisha mwenendo. Sio kutoa hawa kwa mamlaka kwa sababu tulizungumza juu ya Provincial na tulizungumza juu ya Chiefs Act ambayo tunatoa, Chief's Act ni Chief na Assistant Chief peke yake. Wale DO, DC, na PC, hao waliwekwa tu hapo bila Act yoyote, kwa hivyo tunasema hawa hatuwatoi kwa constitution hii kwa sababu huwezi kutoa kitu ambacho hakiko hapo ama jambo ambalo haliko, lakini kwa sababu wako katika Provincial Administration watatolewa wote kwa hii, constitution tubaki na mambo mengine. Wakitoka, wataenda wapee kazi mahali pengine kwa sababu, nikipeana mfano, mtu kama DC ataambiwa labda kwenda kwa Permanent Secretary, na aambiwe sasa wewe nenda kwa Ministry maybe Minsitry of Lands and Settlement or whatever Ministry na upewe kama Under Secretary au Deputy Secretary namna hivyo. Wataenda kwa wakubwa wao wapewe kazi lakini hii orodha ya Provincial Administration itatolewa. Sasa kitu gani kitakuwako?

Ya kwanza, kutakuwa na Village Council. Village Council itakuwa na, tukiongea juu ya village tunaongea juu ya sub-Location, ndio sasa kwa katiba hii inaitwa village. Watu wa sub-Location ambayo inaitwa village, wataaka chini na wachague watu kati ya sita na kumi ambao watakuwa wakiangalia maslahi ya hiyo village. Sasa, kuchukuwa hawa watu wenyewe ndio wataamua kupiga kura au kuchaguwa village elders wale wanataka, hiyo ni mambo yao wenyewe democracia inakuja sasa chini ya wananchi. Sasa hicho ndicho kiwango cha wananchi kabisa, village Council na itakuwa na mambo vile nitakuja kuwaambia na mtaangalia baadaye, ninaenda kwa ufupi.

Wataangalia mambo yao wenyewe mambo ya uchumi, mambo ya health, mambo ya education, kulingana ile jambo lingine ambalo litakuja ambayo inayofuata ni page 26, kwa hiyo pull-out. Ukurasa wa ishirini na sita sorry nilikuwa sijawaambia, devolution of powers Chapter ten mnawenza kuwa mnaangalia hiyo.

Sasa hiyo ndiyo structure village Council, kutoka kwa village Council tutaenda kwa Location Council, Location itakuwa kama Location tunazijua mpaka legislation labda ikuje ifanye mambo yawe tofauti lakini tutakuwa na hizo Locational, Councils, kuangalia mambo ya Location. Na hapa tutapata watu wawili na nikisema kwa hizi Councils hii katiba inasema, lazima asili mia thelathini iwe wamama, it must women 30% of the Councils. Sasa tukija hapa that is minimum wanaweza kuenda juu, tukija kwa ile kiwango ya pili ni Locational Council na Locational Council itakuwa na watu wawili kutoka kwa village Council. Watakuwa kutoka kwa village, watapigiwa kura na waletwe kwa Location, hawa watu wawili mmoja lazima awe mama ndiyo watakuwa katika Council two people from every village au kutoka kwa Sub-Location waje wafanye Locational Council.

Na hawa watakuwa na Locational Administrator, ambaye atapigiwa kura na wananchi wa Location, hiyo sasa ni Location Council, ukitoka hapo utaenda District government au District Council, hawa watakuwa kati kati ya watu hii Council ya District na ndiyo ya muhimu sana kwa sababu itahusika na National Government na mpaka kwa village itakuwa kama the go between. Itakuwa hapo kati kati na ya muhimu sana, itakuwa na wawakilishi kati ya ishirini na thelathini na hawa watu watakuwa wanachaguliwa na wananchi wa District, voters wote. Tukisema voters ni wale kutoka miaka kumi na nane wakienda mbele ambao wamekuwa registered kama voters watawapigia kura halafu ndiyo waendeshe mambo yao.

Watakuwa na District Administrator sasa anachukuwa mahali pa DC. Huyu District Administrator atapigiwa kura na watu wa District. Hiyo District Council ndiyo ya muhimu sana kwa sababu itatoa mambo huko kwa Province, huko kwa National hata ikiwa resources zitakuja kwa District halafu ziende kwa Location Council mpaka village Council. Vile mtakuja na Bwana Leriara alikuwa amezungumzia alikuwa amesema hata village tutakuwa na ile tribunal, korti itakuwa kwa village kwa wananchi.

Sasa tukitoka hapo tutaingilia Provincial Government, kwa Provincial government, kila District kwa Province itatuma two representatives kwa Province na mmoja wao lazima awe mwanamke na administrator wale wa kutoka kila District ndiyo watakaa pamoja na wazungumze pamoja na hii Provincial Council ambayo inafanywa na watu wawili kutoka kila District kama Rift Valley Province iko na Districts kumi na nane times 2 that is 36. Sasa hawa watakaa na wale administrators ambao wanatoka kwa kila District ambao wanakuwa elected ndipo washirikiane pamoja na wachaguwe mmoja wa hawa District administrators awe Provincial Administrator, kila mtu atakuwa anaenda kwa njia ya kuchaguana. Itakuwa namna gani upande wa kazi na ukiangalia huku nyuma kwa hizo pull-out zenu, mkiangalia utawaonyesha nyuma kabisa katika ukurasa wa arubaini na sita utaangalia hapo 7th schedule utaona powers of National and District governments. Utaona vile zinahusiana na hapo kati kati wa ukurasa utaona District government list, vitu ambavyo District itafanya kama development plans, local taxes, education services, nursery, primary and secondary education, medical services, water services, District planning. Haya mambo yote ukiyasoma hapo sitaki kuwachosha mtaona ni mambo sasa yanakuja kwa wananchi hapo kwa District na District sasa ipeleke mambo kulingana na vile village Council na Location Council zimesema. Inafanya pia collection of duties na wanafanya mambo yao kwa serikali zao vile zinalingana.

Basi sitaki kuwachosha, mtaangalia mkirudi nafikiri wengi walipata leo, wale walikuwa wamepewa wamesoma, wameona ni nini sasa mnawenza ku-react na kuona hii ndiyo constitution ya sasa vile nilisema Provincial Administration, sasa inatolewa hii ikianza kufanya kazi, ikipitishwa. Sasa ni hii ya uchaguzi, kuleta powers kwa wananchi wafanye mambo yao wenyewe wakisaidiwa na National government na those houses Bwana Lotia alikuwa akizungumza baada ya hii vile chambers mbili za Parliament zikitoa mamlaka na kupatiana na hizi devolved governments hapa chini, kwa village Council, National Council, District Council mpaka provincial Council. Kwa ufupi hiyo ndiyo serikali inayokuja sasa kwa wananchi.

Tuko hapa na Councillors wenu ambao wametoa mambo mazuri sana tukiwa kwa mambo ya ardhi, na mtu atakuwa anasema labda Councillor au sisi wapiga kura tutakwua tunasema sasa itakuwa namna gani, sasa nitaambia Bwana Raria anaweza ku-clarify hapo kidogo.

Raria: Kulingana na mapendekezo ya katiba ya sasa, ni kwamba kukiwa na serikali ambazo zimesambaza utawala hadi kwenye eneo za wilaya, ni kana kwamba kutakuwa nguvu za serikali ambazo zilikuwa hapo juu kwa National government zitakuja katika sehemu za District ambaye ndiyo itakuwa centre of devolution. Nguvu zote za serikali zimeletwe kwa sehemu za wilaya na ukiangalia katika structure hii ni kwamba local authorities hazitakuwa pale kwa sababu sasa kuna hiyo devolved government ama District Councils na sehemu ambayo mmeona ya Location itakuwa ..(End of Tape four side A)

Raria: (in Masaai dialect)

Interjection: (in Masaai dialect)

Raria: (in Masaai dialect)

Speaker: (inaudible)

Nakholi: If I say so, labda nikisema tu, these council members directly elected by the registered voters of the district na hao ndiyo lazima wawe ishirini mpaka thirty. Kumaanisha wao wanachaguliwa na district mzima directly.

Speaker: Kumaanisha wao wanachaguliwa na district mzima sio location?

Nakholi: Directly.

Speaker: Sio Location?

Nakholi: Sio Location.

Speaker: Hiyo ndiyo interpretation nilikuwa ninataka wajuwe iwe clear.

Nakholi: Okay.

Speaker: Na hawa district Council watachaguliwa na district mzima.

Nakholi: District mzima.

Speaker: Hapana location.

Nakholi: Watachaguliwa direct by the voters.

Speaker: Sasa itakuwa mambo yao katika location hapo(inaudible)

Speaker 2: Mkisema ya kwamba tutakuwa na district council ambayo inachaguliwa na voters ambayo imechaguliwa kwa district na kura inapigwa kwa district, itatokea basi kawaida ya kura ndiyo sasa tunataka kujuwa itakaaje kwa sababu hii(inaudible) na wakati tunataka kuna watatulazimisha na hapo watu wako majority ...

Nakholi: Tafadhali kuja uzungumze tuchukuwe maoni say the name so that we can record.

Cllr. Joseph Ole Koet: Jina langu naitwa Councillor Joseph Ole Koet nimerudi hapa kusema ya kwamba tumesikia hiyo ya kwamba inachaguliwa District Council 20 to 30. Hapo awali tulikuwa tunataka serikali ambayo inalinda kila mwananchi. Tuko na makabila mengi katika districts zetu za Kenya, kwamba hata hapa watu wengine hawatambuliki unasilika ako Ndorobo, wako makabila wengine ndogo ndogo amba wako ndani saa zingine na ingekuwa kama ni katiba ambayo inatengenezwa hizo viti katika kila district ya Kenya, igawiwe kulingana na ile community wako katika hiyo district. Kwa hivyo maoni yangu ni hayo, madaraka igawiwe katika community na kwa district.

Nakholi: Hilo ni pendekezo na Bwana Joseph amesema tribes au communities zote ziwe zinakuwa considered kwa distribution ya hii viti ambayo ni ishirini mpaka thelathini, hiyo ni pendekezo.

Speaker 3: Kuna kitu kingine kidogo, yaani hata katika hii na ni vizuri kusaidia yaani hapa katika hii nataka kuualiza hizi viti ishirini, mpaka thelathini zitakuwa distributed namna gani? Kwa hivyo wangesema kodi na wangesema ni nani au nani atakuwa na authority ya ku-distribute director of distribution of this district representative to ensure a fair distribution kama vile Diwani amesema ndiyo wasitoke tu pahali moja kwa sababu wengi, they can come with five at time of the geographical ndiyo ihakikishe ya kwamba sehemu zote katika district itakuwa represented in the district government. Na tena ionyeshe ni nani, nani atakuwa kwa maana kama haijasema ni nani amepewa hiyo wajibu ya kutekeleza na kupatia watu.

Nakholi: Nitasema hivi tu kwa Councillor vile anauliza, vile tulianza labda tungesema constitution ni kama ile road map kama barabara unaangalia kwa map. Huwezi kuambiwa ukiangalia unatembea west huwezi kujuwa hii pot hole iko wapi au kuna kitu gani kwa barabara, unaenda tu bila kujuwa details hizo na hivyo constitution iko. Sasa hii ni outline na lazima legislation itakuja kuonyesha hii itakuwa namna gani, legislation itatoka kwa Parliament kuonyesha lakini ni vizuri jambo umeuliza liingie hapa, wakienda huko na ni vizuri representatives wetu wa delegates wako hapa mama na Councillor. Sasa hiyo ni vizuri who has

come again? Oh you have come, sasa mko watatu that is good. Mkisikiza hii mambo mkienda huko ni juu yenu kuangalia kama watu wa Narok district kwa jumla kwa sababu mnaenda kwa district jumla, muone hii mambo inakuwa, inaingishwa kwa constitution iwe clarified au legislation itakuwa namna gani kwa sababu lazima hii details ifanyiwe ili watu wajuwu asante sana.

Hellen Kibitu: Naitwa Hellen Kibitu, I am a nominated Councillor Narok County Council. Nataka tu kusisitiza kuuliza ya kwamba kwa sababu saa hizi tuko na 42 wards katika Narok District na wale watu wanatakiwa katika hii katiba ya District Council ni watu thelathini, sasa hata wakina mama wataingiaje basi katika District Council, kwa sababu inaonyesha basi wakina mama watafungiwe nje kabisa katika hii community. halafu kitu kingine walemaru hawataweza kuingia katika hii local Council. Kwa hivyo tutafanyaje ili watu wote wajumuishwe katika ile local District Council.

Nataka tu kusema vile mumeelezwa tuko na makabila mengi sana hapa, inaonekana hata wale ambao wamekuja kukuta wa Masaai hapa katika hii District, wa Masaai watakuwa wachache katika local Council. Kwa hivyo tunataka kuthibitishwa ya kwamba hii katiba italinda haki zetu tukiwa wanawake wa Narok District asante.

Leriara: Asante Councillor. Kuhusu mbinu ya kuhakikisha kwamba kuna watu wote samahani (in Masaai dialect).

Patricia: Patricia nafanya kazi na Action-Aid Kenya. Maoni yangu ni kwamba section hiyo inataka mafundisho ya umbali juu inaonekana kuna giza kidogo wengine wetu hatujaelewa vizuri. Ninaona ya kwamba kuna Provincial Executive Committee ambayo administrator comes from the District isn't it lakini kwa district sioni, naona kwamba kati ya location na district iko mwanya kubwa sana hakuna hiyo link. Tena hii constitution haijasema, tunaona kwamba district administrator, mtu atakuwa akifanya kazi kubwa sana kwa district, haijasema qualifications za huyo mtu itakuwa nini sasa sijui hata kama mtu mwenye hajaingia darasa atakuwa district kwa sababu atachaguliwa na watu juu wanampenda lakini sasa tunataka iwe clear.

Leriara: Na kwa maoni yako ungependa district administrator awe na qualifications gani?

Patricia: Mimi ningependa hata akuwe na degree mbili ama moja.

Nakholi: Asante sana kabla sijakuita mama wacha tu ni Patricia ameuliza ya kwamba kuna giza kati ya district government na provincial government.

Patricia: Kati ya district na location na pia kuna mwanya kubwa, (inaudible).

Nakholi: Sasa kuna election ya kwanza, village council kati ya watu tisa na kumi, villagers wenyewe watacaa na village ni sub-location tumesikizana hapo?

Patricia: Ndio.

Nakholi: That is clear, ukitoka hapo utakuja kwa location government. Sasa kila village itakuwa inatuma watu wawili kwa location, mmoja wao must be a woman tumsesikizana hapo?

Patricia: Yes.

Nakholi: Lakini administrator wa location anakuwa elected directly by the voters in that location, hapo ni sawa?

Patricia: Ni sawa.

Nakholi: Okay, tunarudi kwa district government na hii ndiyo muhimu sana vile nilikuwa nimesema. Sasa hii district council inakuwa elected watu ni kati ya ishirini na thelathini na hawa watu wanakuwa elected directly by the registered voters in the district to arrive at these people. Hiyo ndiyo constitution, details will be in the legislation itaingia kwa ile orodha itatengenezwa okay?

Patricia: Hapo ndiyo ninasmea sio consistent.

Nakholi: It is not consistent ..

Patricia: From the village to the location, (inaudible)

Nakholi: The location administrator. Hiyo ni recommendation we are putting it down na delegates mnasikia? It is a recommendation by Patricia.

Joseph Ole Koet: Jina langu ni Councillor Joseph Ole Koet. Swalilangu ninauliza ya kwamba ilisemekana kwa hii katiba hatutakuwa na administration police, tutakuwa na council village. Kitu tunaona ya kwamba kwa hapo, tuchunge sana kwa sababu ya security, kwa sababu mahali mimi nimetoka nikiwa hapa Narok County Council ni zaidi ya kilometer mia mbili na arobaini na hatujawahi kuona ile polisi ingine bila administration police na tunapata shida sana ya security. Kuna wakati hata tulipata watu ambao wametoka Somalia wameingia huko, kama sio hawa watu wa administration police tungefanya nini na tukiambiwa saa hii ya kwamba tukae bila security lazima tuwe na wasi wasi kwa sababu mali yetu tunataka ichungwe na hizo siku zingine hatujawahi kuona aina ingine ya police, tunaona administration police na ndiyo wanatulinda na pengine iwekwe kila mtu asaidiwe awe na homeguard kama inawezekana.

Kwa sababu hii nchi yetu ingeweza kufanana na America, lakini sisi bado ni majambazi hatuwezi kufananishwa na America, tuna

majambazi ya bunduki misituni, tuna majambazi ya mishale, tuna majambazi ya kila aina. Kwa hivyo, hatuwezi kukaa bila security sisi wenyewe kwa hivyo, hiyo tungeelezwa ya kwamba tutakua na security ya aina hii kwa sababu tuna wasi wasi hata kila siku kila mmoja wetu hapa anajua, ng'ombe ya fulani imeibiwa, mbuzi ya fulani imeibiwa, twende kwa askari. Kama huna hawa askari tutaenda wapi, kwa hivyo mimi ninaomba tuelenze askari watakuwa wapi na watakuwa wakina nani kwa sababu hatuja wahi kuona hawa polisi wengine ambao wako katika district level.

Nakholi: Asante sana Councillor nitakuita mama wacha tu nimalize kitu kidogo asante sana Councillor, hii mambo ambayo iko hapa ya devolved government au serikali ya kuja kwa wananchi ni kitu ambacho kimeweza kufanyika kama wewe Councillor umetembea au utatembea lakini ile example ninaweza kupa nzuri sana ni ya Uganda.

Joseph Ole Koet: Ndio.

Nakholi: Ulikuwa huko nyumba kumi, ile inaitwa nyumba kumi haiwezi kumaanisha nyumba kumi. Kila boa tukichukuwa boma kumi..hapana bunduki kuna community policing na sasa hiyo ndiyo inaanishwa hapa because a village Council must have the security in fact hata sasa mambo itakuwa mzuri sana. kuangalia at every state. Sasa hiyo sio kutoa huko America au nini example ni hapa tu asante sana.

Pauline M. Kinyargu: Kwa majina ninaitwa Pauline M. Kinyargu na nitaongea Kiswahili nafikiri hapa sasa tunasikia sisi sote ninataka kuuliza swali ya kwamba nimesikia hii uchaguzi watu watachaguana vile mumetaja hakuna haja kurudi kutaja taja sana kitu ambacho tumeelewa. Ninataka kuuliza jee kama tuko hapa Narok na tumechanganyika na hiyo ndiyo ningetaka kujuwa sana na tunataka tuchaguliwe kuna watu wa kabile watasimama wachaguliwe au ni wenyefi? Juu mimi maoni yangu ningeonelea hata kama watu wako hapa makabilo zingine, hapa ni Masaini na ya kwamba, kama saa hizi mimi nikienda Kiambu lazima niende nifuate vile hawa wanasema, sio mimi ninaenda kusimama kutafuta kitu.

Kwa hivyo kwa maoni yangu, ningesema hata kama ni wangapi wako hapa wamekuja kututembelea na wamekuja kufanya kazi, sisi wenyewe tuchague yule mtu tunataka, na hatutaki mtu mwengine aamke kutafuta hiyo kit. Sisi wenyewe wa Masaai kutoka ma village na hata kama ni DC, Masaai mwenyewe ndiyo ataamuka kusimama lakini sio mwengine anaamuka kutafuta hiyo kit, ati tunatakikana ati hapana, kwa sisi tunasema wa Masaai wenyewe. Ninataka mimi unipe hiyo kitu kama kuna mtu mwengine atamka kusimama juu mimi hata nikienda Kiambu sisimami, hakuna pahali Masaai ako na kwa nini mtu anakuja kusimama hapa? Hatutaki.

Leriara: Okay, asante hayo ni maoni yake

Nakholi: Sasa nikimaliza mzee wewe utakuja mzee wewe kuna kitu kimoja we are forgetting, we have been with this thing, my daughter says this thing(inaudible) and then kutakuwa na wewe na wewe, tukimaliza hapo ndio tuendelee. Kuna mambo

mengi sana jamani kwa hivyo tuguzie na tuendelee.

Lelunka Malipe: Naitwa Lelunka Malipe nataka kuongea kuhusu mambo ya legislation. Umesema kwamba hii kitu ni draft tu, but you don't want to wait for the legislation because most of those Members of Parliament, we have lost their confidence so we can't wait for them to legislate on this Act of devolved government. We want the final draft to know, I mean to spell out the duties, qualification for members and again to add on top of that nataka kujuwa ulisema district administrator, I mean that means he or she is going to be an .. he is an Executive, body or a person ama ni governor or whatever or Chairman. We want to know something like Chairman of a District, Executive Director or maybe a governor.

Nakholi: Pendekeza

Lelunka Malipe: Okay, halafu ya mwisho ni kuhusu ile madam Pauline amesema kuhusu Masaai land.

Nakholi: Pendekezo ndiyo tunataka kwanza, you suggest what would you like it to be called.

Lelunka Malipe: District Governor, because this constitution is more or less like majimbo style. Mimi ninaona kama mmeleta lakini you don't want to use the name majimbo for the same that, it may bring some public civil and public debate.

Leriara: Devolution is a compromise between Kenyans who wanted majimbo and the Kenyans who wanted a military system of government, it was fifty fifty, there were as many Kenyans who wanted a military system of government and there were as many Kenyans who wanted a federal system of government, so devolution was their compromise.

Lelunka Malipe: Okay, that is devolution you must not use this name of province; you should just say that Kenya is a federal republic consisting of federal states. I think you should just go straight to the point because more or less it is a federal system like Nigeria. So, we should have a governor in the district, then a governor in the province. Halafu, kuhusu vîle Pauline amesema hapa kuhusu Masaai in every district like the Masaai minority communities and the marginalized communities, we must have a screening committee of council of elders to screen the people who are going to contest if you are not Masaais those council of elders wataema hapana we cannot accept ama namna gani? Hiyo screening committee ya wazee waseme wewe si Masaai, wanafanya interview wakiuliza maswali ya ki-Masaai kama wewe si Masaai huwezi ku-contest only in Masaai land because we are a minority community so write that one. Na kuwe na wa mama kama ni ten council of elders in the district pia kuwe na wa mama kama watatu, at least three women in the council of elders.

Then again, we must have reservation of seats in the state corporations because most of the state corporations haziko Nairobi peke yake, zingine zije kwa district. We must have reservation of seats for the National Corporation for the minority tribes like Masaai at least 10% of the seats ama employment opportunities kama Bank, kuwe na wa Masaai ndani yake kwa sababu we

are tax payers and we must share in the governance.

Nakholi: Unaweza kuongea Kiswahili.

Lelunka Malipe: Kwa Kiswahili, mimi ninafikiri nimemaliza yangu asante.

Speaker: (inaudible)

Lelunka Malipe: Kwa lugha ya kimombo council of elders seasoned politicians kama wewe, wewe umefanya kazi kwa muda mrefu, you are retired personnel you can join a council of elders pia kuwe na wazee ambao hawajasoma. Kuna wazee ambao hawajasoma lakini wana hekima, they know many things about the Masaai community. Wakiongea na huyo wanajuwa kweli huyu kijana si Masaai anadanganya. So, we must have a retired personnel wa serikali kama wewe ambaye umekuwa seasoned politician na pia kuwe na wazee ki-Masaai tradition na mzaliwa wa hii community wa ki-Masaai na pia wa mama asante.

Leriara: Kwa hivyo amesema qualification ya village elders, ni watu seasoned politicians, amesema pia inahitaji wazee na kina mama wenye hekima na pia maafisa ambao wamestaafu kutoka kwa uma na pia lazima wawe watu indigenous, asili wa sehemu hiyo.

Speaker: Asante sana Commissioners (end of Tape 4).

Speaker: Kulingana na mjadala huu naunga mkono jambo hilo, twaomba kuwe na watu ambao wanaelewa watu na watu ambao kwa kweli wanafahamu viziru Council of Elders na opinion leaders wawe(Inaudible) Ili hawa ndio watakuja kuangalia kuwa mambo ni sahihi. Sababu yangu ya kusema hivyo, juzi kulikuwa na elections ya delegatesno disabled person is elected kuwa representative katika delegates wale ambao waneenda huko. We are really bitter because of that, tuna watu zaidi ya elfu mbili au zaidi hapa Narok na hatuna mtu mmoja mwakilishi wetu hapa Narok na kilichosababisha kitendo kama hicho ni kukosa watu wa aina hilo ambao wana-credibility kuangalia wale watu ambao wanastahili. Angalau somebody ambaye anaweza kuenda Nairobi na aongee juu ya hawa watu, hiyo jambo Commissioners mu-note kwa sababu tuna jambo kama hilo na hata tulikuwa tunataka kuja Kencom House kuuliza why tume-apply, some of us tume-apply na tumekuwa neglected, discriminated na hatuko tayari kabisa kwa jambo kama hilo. Tuko katika laini ya watu, tupatiwe nafasi ya kutenda mambo kama hayo. For those who are going to Nairobi among the three of them there is no disabled person na Katiba inasema namna hivyo. Kwa hivyo tunaona kwamba even this one ya devolution of power ya 20 people or 30 tuna hofu, hatuna confidence na hiyo kwa maana bado tutakuja kutupwa tupwa. Tutawachwa tu kama ile takataka inatupwe kwenye pipa. Kwa hivyo tumesema kwamba a body should be formed ambayo itakuwa na wazee wale ambao wako na akili watateuwa wale watu

na wawe na special consideration kwa sababu tunaona tu kwamba vile inafanywa haitaingia. Kwa hivyo yangu yalikuwa ni hayo tu. Thank you.

Cllr. William Ligeilele: Jina langu ni Councillor William Ligeilele. Nimesimama kwa niaba ya wale district representatives wenzangu, Kimna yuko pale, naona mama ametoka nje. Nataka kuwahakikishia tu mnenaji ambaye ameongea ya kwamba tutawakilisha interest yao, si lazima uwe disabled ndio utetee disabled, ni roho ile mtu ako nayo. Kwa hivyo tutahakikisha, nataka tu kuhakikishia ya kwamba tutafikisha maoni yenu na hata siku ile Commission hapa ni ilipokuja nyinyi wenyewe mliongea na yalichukuliwa bado tutakuhakikishia ya kwamba imechukuliwa. Nilitaka tu kutoa hakikisho hilo. Tuwawakilisha bila ubaguzi, bila chochote kwa sababu you are also part of society na tumekuwa na nyinyi. Hata Wamaasai kabisa wanajua hiyo hata bila kuambiwa kwa maana tuko na watu namna hiyo manyumbani na wale wengine ambaao wamejaliwa na miili mizuri ndio husaidia wale wengine ambaao ni disabled. Kwa hivyo katika mila yetu ya Kimaasai hata hufundishwi.....(vernacular)

Maurice Kepoi Raria: *Ashoree* Councillor kwa kutuhakikishia ya kwamba pia mutaweza kuwakilisha hawa wenzetu ambaao ni walemavu kwa sababu kusema ukweli haiwezekani kila wakati kwamba watu wote wanaweza kuwakilishwa katika kazi kama hizo kwa sababu hata kuna sehemu zingine ambazo hawatakuwa wameakilishwa katika hiyo National Conference. Kwa sababu tunasema ya kwamba kuna watu ambaao wako chini ya umri wa miaka kumi na nane, tuseme watoto, na hawana wakilishi wao pale, lakini tunaamini ya kwamba wale watu wataenda pale ni lazima pia wawakililishe watoto. Kwa hivyo hata wale watu ambaao hawajapata kuchaguliwa, wale ambaao wamechaguliwa ni lazima wazingatie masilahi ya watu wote katika jamii.

Speaker: ...(Inaudible)

Steven Monik: (Inaudible) ...probably because of the uproar over women representation, nimeona wamepewa akina mama nafasi nyingi sana and if that was to be allowed then the boy child is disadvantaged. Sasa mimi naona hivi, I think the Constitution needs to address the issue of gender instead of women. Constitution iseme uf kutatakiwa kuwe na watu wawili, Constitution iseme, those members should not be of the same gender because if we are going to allow the campaign of the girl child to go on then we are going to reach a state where the boy child's interests will be forgotten and that is equally disastrous. So wacha iwe hivyo.(vernacular). So we should guard against such an eventuality.

George Nakholi:(vernacular).

Speaker: Thank you for that clarification. District Councils and districts generally should try to recognize the cultural homogeneity of the same. This is majimbo by another name, tuseme District Council iwave prominence to the indigenous people of the same place halafu tuseme hata Provincial Councils....because I am aware of this and I have gone through the

draft but I can't claim to have mustered it. I have a feeling that the draft Constitution should make it very clear that when the provincial boundaries are redefined then they should take into account the fact that people of the same cultural inclinations are lumped together, right. So that we have Provincial Council of the Maasai because they have everything in common and then the District Council should be empowered to make their own laws. I have not seen something like that in the draft. They should be empowered to make their own laws in keeping with their culture so that they handle cultural conflicts like family disputes, land issues, they are best placed to handle such, right? And the Provincial Council of course, having said that they should be cultural homogenized should have their office based at the province.

The draft Constitution does not have a provision for the(Inaudible) in the Council or even in the cabinet. Therefore I am suggesting that the draft should include this with a percentage of slots which should be reserved for disabled persons in the Councils or even in the Houses.

Maurice Kepoi Raria:(Inaudible)

Speaker: Adopt and I think the draft must have also overlooked, in fact as I have said in the Preamble and the Bill of Rights in fact it has tried as much as possible to expand on the needs in respect to the disabled persons but that is the only that(Inaudible), right. So I am of the view that the draft should state it explicitly that a third of positions in the Councils, in the Houses of Parliament and even in other organizations or even in the districts should be reserved for people with disability and people with disabilities can either be men or women. I think that will be fair and when we talk of people with disability, we should think of both men and women. I am actually through.

Elizabeth Kasira: Kwa majina naitwa Elizabeth Kasira. Langu ni tofauti kidogo lakini nitazungumzia kuhusu hii draft na mambo ya Constitution. Mimi na group yangu kutoka mwezi wa pili, tumefanya civic education na kusema kweli tumeona hapa Narok tumekubali huo mwito kabisa na tumeona kabisa tulikuwa tumenyanyaswa ya kutosha na nafikiri wengine sasa tumejua haki zetu. Sasa langu lilikuwa tu nataka kuzungumza kuhusu hii maneno ya Chapter 5 ambayo ni Bill of Rights, religion, mambo ya dini.

Serikali imekubali dini zote na mkiangalia kabisa kusema kweli wengine tunakuwa-confused hata tunashindwa kweli kwani ile dini ya kwanza, na ni Mungu mmoja, munasahau ni Mungu mmoja tunaomba sisi wote. Kwani ile dini ya kwanza ama ya pili na ya tatu zimeenda wapi kwa sababu kila mtu hata mimi nikiamka asubuhi na nianze dini yangu, ni kweli nimekubaliwa na serikali. Hilo jambo likiendelea hivyo tutafika wapi, kweli tutamwona Mungu? Hilo ni swali langu.

Maurice Kepoi Raria: Toa maoni yako.

Elizabeth Kasira: Maoni yangu ni kuonelea serikali ingechukua hilo jukumu halafu i-limit iweke limit kwa yale Makanisa

yanafaa kwa sababu sisi wote tunaomba Mungu mmoja.

Maurice Kepoi Raria: Ziwe kama ngapi?

Elizabeth Kasira: Kama tano.

Maurice Kepoi Raria: Kwa hivyo mama unaweza kubali Kanisa lako litolewe to be merged with another one? Wewe ni mshiriki wa Kanisa gani?

Elizabeth Kasira: I am a Catholic.

Maurice Kepoi Raria: Kwa hivyo unaweza kubali hiyo itolewe ili tupunguze. Okay, wacha nikujibu, keti tu mama.

Elizabeth Kasira: I have a point I want to mention.

Maurice Kepoi Raria: Oh, you have a point, okay.

Elizabeth Kasira: Tunajua hapa nchini dini ililetwa kitambo na Wazungu na kusema ukweli kuna yale makanisa ya kwanza na tuna yale yana wale watu wetu. Kuna haya yanatokea kama hii ya Apostolic ilikuja juzi na hiyo hata haitusaidii. Hiyo inaleta madhara hapa na wengine wanaenda wana-join dini kama hizo sasa tunajenga taifa aje tukiingilia mambo kama hayo?

Maurice Kepoi Raria: Kwa kusema kweli jambo ambalo mama amezungumzia ninaweza kusema namna hii; kwanza kusema kweli Katiba hii imetambua kwamba nchi hii ni nchi ambayo inamwabudu Mungu na kwa hivyo ndio sababu Katiba hii imetoa uhuru wa kuabudu lakini pengine jambo ama kipengele ambacho ungepende kiwekwe katika Katiba hii ni kuonyesha ya kwamba ni nani anayeabudiwa. Kwa sababu kwa kusema kweli kuna malalamisha na wananchi wamesema ijapokuwa ni vizuri kuwa na uhuru wa kuabudu lakini Katiba yapaswa kuzingatia ni nani huyu anayeabudiwa, kwa sababu Wakenya wamesema kwamba kuna watu wengine ambao hawamwamini Mungu. Lakini ningependa kuwaambia wananchi ni vigumu sana kujaribu ama Katiba hii kujaribu kusema ati tuta-limit idadi ya Makanisa. Ni vigumu sana na kama kuna mtu ambaye anaweza kuwa na formular yoyote ya ku-limit hizo Makanisa pengine jambo ambalo mimi ningeonelea ni kwamba kama dini iko pale mradi tu isiweze kudhuru ama kutisha maisha ya watu wengine, kwa sababu umepeana mfano wa Mungiki ambao tunajua wanajihami na silaha. Dini kama hiyo ina hatarisha maisha ya watu wengine ama inawatisha. Kwa hivyo dini kama hizo ni lazima Katiba ichukulie hatua.

Cllr. William Ligeilele: Mimi nafikiri huyo mama amesema point kubwa kwa maana uhuru ambalo hauna mipaka si uhuru. Uhuru ambalo hauna mipaka si uhuru, mtu akienda aseme leo mimi natengeneza Mungiki yangu halafu anaanza kuzunguka hapa

kukimbiza akina mama na nyembe na visu, hiyo ni primitivity, ni barbaric, kinyama. Na kwa hivyo tungesema dini ambayo itasajiliwa katika nchi hii ni ile kwanza ambayo haikuji ku-duplicate, kuongeza ku-duplicate zile organizations ambazo ziko leo. Kama ni Hare Krishna wakae namna hiyo, hakuna haja ya kuongeza. Hare Krishna zingine juu ya ile moja. Tena katika magazeti tumesoma kuna kitu kinaitwa devil worship na research imefanywa katika Kenya and there was a Presidential Commission ambayo ilichaguliwa ya devil worship na hata mpaka leo hiyo ripoti haijatoka. Kwa hivyo tuingize katika Katiba ya kwamba devil worship ni marufuku katika Kenya. Kuko pia na dini ambazo zinaonekana ya kwamba zinakuja na mbinu za kurudisha watu nyuma, hizo pia zikataliwe katika Constitution mpya. Mimi ningetaka kuchangia kusema mambo kama hayo ya devil worship tukatae, mambo kama ya satan worship kwa maana huko Amerika wamepeua hiyo freedom, na hiyo tukatae hapa. Kitu ambacho kinatokana na hayo tukatae.

Haya, jambo la mwisho kuko na hiki, hata kama hutujafika hapo lakini imeshikana na dini, kile kipengele kinasema mtu hatabaguliwa hata katika dini yake, katika mila yake including sexual orientation na hiyo sexual orientation hatutaki kitu kama hicho. Kwa sababu katika Kenya sisi ni Waafrika hata kama kuna watoto hapa tutasameheana leo. Sisi ni watu wazima wote, hata kama kuna watoto wetu, funga masikio. Hiki kitu kinaitwa sexual orientation ni kitu kibaya na katika Uzunguni wamejiingiza kwa hayo mambo na sisi katika Afrika hatutaki mambo kama hiyo, tunajua debate iko Zimbabwe saa hii hata karibu ilete vita juu ya hiyo sexual orientation. Kwa hivyo, mtu yoyote ambaye ameingia katika sexual affair ambayo sio natural sisi tuseme katika Kenya ni marufuku, mwanaume kuoa mwanaume mwingine, mwanamke kuoa mwanamke mwingine. Ndoa zingine ambazo.... kwa sababu kesho hatazitakuja kuvunja Kanisa kwa maana mkipitisha hii katika sheria mtu ataenda tu kwa Padri na amwambie unganisha mimi na huyu na ni wanaume wawili, ukikataa atapeleka wewe kotini kwa sababu Katiba imekubali. Kwa hivyo hiyo ndio tunasema mambo ambayo they are unnatural acts kama hiyo, mambo ambayo si ya kiumaumbile, si vile Mungu aliumba, mambo ya roho, mtu kusema tu mpenda roho hula nyama mbichi sisi tuweke katika Katiba yetu kusema hatutaki katika Kenya, hatutaki hiyo homosexuality, hatutaki hiyo mambo ya lesbianism, hatutaki hiyo maneno yasexuality. Laini ni mrefu lakini tusema tu katika Katiba, tutoe Katiba ambayo inasimamia the natural aspects, ile sheria ya Mungu ambayo ni ya kimaumbile si ile ya kupinga ubinadamu na fikira na desturi njema. Thank you.

Maurice Kepoi Raria: Asante sana Councillor na wewe ndio utakuwa wa mwisho kwa kuchangia hiyo. Ni vizuri Councillor ni delegate kutoka kwa district hii na wako hapa watatu wanaskizi vizuri nafikiri. Vile naomba tu muanze kufanya negotiations na lobbying ili mukienda huko pia mushike wale wenzeni, mtakuwa mia sita ishirini na tisa. Mupate hata juu ya nusu ya hao na muone kwamba haya mambo ambayo ni un-African yanaweza kuondolewa.

Nafikiri mutaniwia radhi kwa sababu tukiendelea hivi hatutafanya mengi na nafikiri watu wako hapa wa mbali. Si wako watu wa mbali hapa?

Audience: Ndiyo.

Maurice Kepoi Raria: So you will ask him, you can give him your contribution. You can come in away and contribute whatever you wanted but let us go to another chapter tafadhali unless something is very burning and you can even say it from there. Say from there.

Speaker: Dini hasa ambazo zimetokea nyingii zimetoka nje na zingine zina desturi nyingi sana ambazo hatuelewi ni namna gani.

Kwa hivyo wale wazee amba wanakuwa katika dini hizi watakuwa na responsibility ya kukataa hizi dini na kupeana kibali kwa hizi ili mambo ya injili kutoka nje ifutwe na isikubalika pahali hapo.

Cllr. William Ligeilele: Tafadhali nitaomba wale amba wameinua mikoni watuuwie radhi ili Bwana Ole Raria aingalie mambo ya Bunge au Parliament na elections, ni mambo marefu kidogo, halafu tuone vile tunaenda. Asante sana.

Maurice Kepoi Raria: Nikianza kuzungumzia juu ya Bunge, ningependa kutumia Kiswahili lakini baadaye kwa wakati wa kufafanua nitakuwa nikitumia pia lugha ya Kimaasai lakini kuanzia sasa ningependelea kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu kuna terminologies zingine ambazo zinaweza kuniletea shida na kunivuta nyuma kwa hivyo nafikiri mtaniwia radhi.

Basi tunaenda kwa Legislature, tunaenda kwa Parliament na ningependa kuzungumzia mambo ya muhimu ama mambo za kimsingi ambayo ni mpya katika Katiba mpya. Ningependa kuzungumzia ambayo hayakuwa katika Katiba tulionayo hivi sasa na ambayo yamebuniwa katika Katiba mpya. Na zaidi ya yote jambo jipya sana katika Katiba ya sasa kuhusu Bunge...(Interjection).

Cllr. William Ligeilele: Angalia page ya kumi na tatu na mnaenda page kumi na nne ya hiyo pull out.

Maurice Kepoi Raria: Ni kutoka page 13 na page 14.

Cllr. William Ligeilele: Hasa ni page 14.

Maurice Kepoi Raria: Hasa ukurasa wa kumi na nne. Nikitumaini ya kwamba nyote muko hapo hivi sasa, ningependa kuwaambia jambo jipya sana ambalo limebuniwa katika Katiba mpya. Ni kwamba mwajua hivi sasa tuko tu na Bunge moja lakini Katiba hii imependekeza kuweko na kumbi mbili za Bunge. Katika Katiba hii tumependekeza kuwa na two chambers of Parliament, kutakuwa na Upper House ama kumbi la juu na kutakuwa na Lower House ama kumbi la chini. Kumbi la juu litakuwa likiitwa National Council na kumbi la chini ile mnajua na litakuwa linaitwa National Assembly. Kwa hivyo Parliament itakuwa na two chambers, chamber ya juu ambayo itakuwa ikiitwa National Council na ya chini itaitwa National Assembly.

Basi ningependa kuwaambia ama kuwajulisha vile wakilisha ama Wajumbe wa hizi kumbi mbili watakuwa wakipatikana na nitaanzia na ile ambayo mnajua ambayo ni kumbi la chini ama National Assembly amba wajumbe watatoka katika zile sehemu

za wakilishi Bunge mnazojua. Katika taifa hii kuna sehemu za wakilishi Bungeni mia mbili na kumi katika taifa la Kenya. Kwa hivyo Wajumbe wa kumbi la chini National Assembly litakuwa na Wajumbe mia mbili na kumi vile ilivyo hivi sasa na hakutakuwa na Wajumbe wanaoteuliwa. Mnajua Katiba ya hivi sasa inapea fursa kuchaguliwa ama kuteuliwa kwa wajumbe ambao huwa kumi na wawili lakini sasa hakutakuwa na kuteuwa kwa sababu wananchi wamesema ya kwamba tunahitaji wajumbe wawe ni wale tu wanaochaguliwa na wananchi. Hivyo basi kuna mbinu nyingine ambayo imebuniwa ya kwamba kwa hilo kumbi la chini ama National Assembly, kutakuwa na Wajumbe wengine wa ziada tisaini na nitawaeleza jinsi hao watakavyopatikana.

Kwanza nia ya kuwa na orodha nyingine ya wajumbe tisaini ni kwa sababu Tume ilionelea ya kwamba kuna watu katika sehemu ya jamii ambao huwa wakijiwasilisha kwa uchaguzi wa kawaida, hawawezi kuchaguliwa waakilishe wananchi katika Bunge. Ninasema watu hawa ni akina mama na pia watu walemovu. Kwa kawaida, na mmoja wao aliwahi kulalamika hapa, wao nakuwa wanabaguliwa wakati wa uchaguzi. Na Tume ya Kurekebisha Katiba walikuwa pia katika mjadala, kwa sababu wananchi waliwaambia ni lazima kuwe na mbinu ya kuhakikisha ya kwamba pia watu hao ni lazima waweze kuwakilishwa katika nyadhifa kama za Bunge, basi lilikuwa ni jukumu la Tume ya Kurekebisha Katiba kutoa mbinu ya kuhakikisha ya kwamba watawakilishwa. Basi walipendekeza kuwe na orodha ya wajumbe tisaini na kabla ya uchaguzi kila chama cha siasa kitakuwa kikitoa orodha ya majina tisaini na kupatia Tume ya Uchaguzi. Kila party itakuwa na list yake ya 90 members list ambayo itapelekwa kwa Electoral Commission. Basi wakati utaenda kwa uchaguzi utakuwa ukichagua mjambe wako halafu utachagua pia chama ambacho unafikiri ni maarufu. Vile ninasema ni kwamba, umekuta mara kwa mara ya kwamba pengine unampenda Mjumbe wako, ungependa kumchagua lakini kile chama ambacho kinamdhmini haukipendi ama haupendi sera zake kwa sababu mara kwa mara moja au nyingine haipendelei masilahi yako.

Hivyo basi vyama vitakuwa vikijaribu kuvutia orodha hii ya tisaini, itakuwa ni akina mama peke yake na watu walemovu. Wale watu wengine, wazee ambao wanaweza kujiwasilisha katika uchaguzi wa wale 210 members hawatakuwa kwenye hiyo list, hii list ni pambo ama ni mbinu ya kuhakikisha akina mama na watu walemovu watakuwa wameakilishwa. Pia watu wengine wanaotoka katika sehemu kame kama people from marginalized areas ama minority communities ndio watakuwa katika ile orodha, watu ambao kwa jamii wanaonekana kwamba wanadhuriwa sana na ambao kwa hivi sasa katika Bunge ya sasa wako na uakilishi mdogo sana. Basi orodha hiyo ya vyama itakuwa na watu kutoka minority groups, itakuwa na watu walemovu na itakuwa pia na akina mama. Hivyo basi watu kama hawa

Kile chama ambacho kimeahidi ya kwamba kikishinda ama kikipata viti vingi katika Bunge watapewa nafasi ya kuzidi kwa akina mama basi akina mama huenda wakaenda kuchagua kile chama. Kwa hivyo wanaweza kuchagua Mjumbe wake lakini hachagui chama ambao Mjumbe yuko kwa sababu chama chake hakizingatii mambo ya akina mama. Kwa hivyo utachagua mjambe wako halafu uangalie ni chama gani ambacho kinajali masilahi ya akina mama halafu ikapigie hicho chama kura. Hivyo hivyo watu kutoka sehemu kame, minority groups wataangalia ile orodha ambayo imepeanwa na vyama vya kisiasa na wakiona kwamba kwa mfano ni Safina ndio imeahidi ya kwamba viti hamsini za kwanza, iwapo itapata viti vingi katika Bunge, katika

orodha hiyo ya wajumbe tisaini basi sehemu kubwa watapatia watu kutoka kwa sehemu kame basi utakuta watu kutoka sehemu ya Kajiado, utakuta watu wa sehemu ya Narok, utakuta watu wa Transmara na watu wa North Eastern wataenda kupigia hicho chama kura kwa sababu hicho chama kikipata majority katika Bunge basi wao wataingia katika ile list na wataweza kukilishwa katika Bunge. Na katika hii list ya Wajumbe tisaini tutakuwa na zip system ya kuhakikisha ya kwamba kutakuwa na mama na mzee, tutakuwa na mama na mzee, tutakuwa na mama na mzee hadi wa tasaini. Hivi kwa mfano, kama itakuwa ni chama cha Safina ndicho kitashinda viti vingi tuseme imeshinda 20% ya viti katika Bunge basi watapatiwa 20% ya ile list ya Wajumbe tisaini.

Kwa hivyo basi hicho chama kikipatiwa 20% ya wale watu tisaini ya ile orodha ya wajumbe tisaini basi itaonekana tutakuwa na akina mama wengi amba wataenda katika Bunge. Pia watu wale mavu wataagalie kile chama fulani kinazingatia mambo yao na katika ile list watu arubaine wa kwanza ni watu wale mavu. Kwa hivyo wale mavu wataenda bila shaka kupigia kile chama kura.

Kwa hivyo hicho chama kikipata majority katika Bunge na watapatiwa majority kwa ile list basi wale watu wale mavu amba wamekekwa katika ile orodha yao wataweza kuwakilishwa katika Bunge. Kwa hivyo hiyo ndio nia ya kubuni hiyo list ingine ya orodha ile ingine ya wajumbe tisaini kuhakikisha ya kwamba watu kama hawa amba wanahudhuriwa katika jamii ili waweze kuwakilishwa katika Bunge. Kwa hivyo mpaka hapo ningependa tu njue kama tunaelewana kabla sijaenda kwa jambo lingine, sijui kama mnaelewa hiyo.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Ninasema ya kwamba kabla ya uchaguzi kila chama cha siasa kinapatiana kwa Electoral Commission list ya watu 90. Promise ni kwamba hawa wajumbe tisaini amba wamechagua kutoka kwa akina mama, wamechagua kutoka kwa wale mavu, wamechagua kutoka minority groups, wana-promise ya kwamba wakishinda ama wakipata asilimia kubwa katika Bunge basi ile asilimia ya ushindi katika Bunge basi watapata pia asilimia hiyo hiyo, kwa vile orodha ya wajumbe tisaini. Kwa hivyo hiki chama Electoral Commission ikitangaza ya kwamba wamepata 50% katika Bunge, basi wanapewa pia 50% kwa ile orodha ya wajumbe tisaini ambayo Electoral Commission iko nayo. Kwa hivyo hiyo sio kuteuliwa wamechaguliwa kulingana na ile party list. Nafikiri tunaelewana hapo.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Hakuna ku-appoint tena. Ile list ambayo mlikuwa mmepeana kwa Electoral Commission, nyinyi hamuwezi kubadilisha tena. Kwa hivyo hata vile mmewe ka number one, number two and number three, hiyo system haiwezi kubadilishwa kwa sababu mnaweka in terms of priority. Kwa hivyo kama mmepewa 50%, it is that 50% ya wale kutoka juu kwa hivyo hamwezi ku-manipulate tena kwa sababu hiyo list itakuwa kwa Electoral Commission haitakuwa kwa chama tena.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: The Electoral Commission watahitaji ile list kabla ya uchaguzi. Nilisema before election kila chama kitapeleka kwa Electoral Commission list yake ya wajumbe tisaini. Kwa hivyo ni Electoral Commission ndio wataangalia waseme chama fulani kimeshinda asilimia hamsini katika Bunge, kwa hivyo wanaangalia katika ile list wanasesma hawa the first part kwa sababu ndiye atapewa 50% ya 90, basi hao watachaguliwa vile wako kutoka one, two.... that is the order of priority.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Yes, nasema kile kitapata 50% wanachukua 50% ya 90 seats, kile chama kingine kinapata 20% wanachukua 20% ya 90 seats, kile kingine kinapata 10% katika Bunge wanapatiwa 10%. Kwa kusema kweli kila chama kitaweza kuwa na wakilishi kutoka ile list ya 90 seats na hao wote watakuwa either ni akina mama, disabled ama ni watu kutoka minority groups.

Speaker:(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Hiyo list ya 90 na ningependa sana tujaribu kusikizana kwa sababu nimejaribu kueleza kwa umakini sana. Hii list ya 90 seats vyama vitakuwa vikitoka nje, tusema kama chama kina strong hold, tusema kiko na strong hold Central Province, watakuwa wakitaka kuvutia makabila mengine wapigie hicho chama kura. Kwa hivyo watatoka Central wakuje Narok halafu wakuambie ya kwamba katika hii party list ambayo ni lazima wa-submit kabla ya uchaguzi sisi tutawapitia nafasi ya the first five positions, number one, two, three, four and number five. Hicho chama kutoka Central Province wanawa-promise ya kwamba, tuseme ni DP watakuja Maasai waseme mkipigia DP kura the first five members na wanawaandika, tumpatia huyu mama halafu pia mtu mwagine kutoka Narok, mwagine kutoka Kajiado na mwagine kutoka Transmara, mama mlemavu namna hiyo. Halafu wanasesma sisi tukishinda ama tukipata asilimia kubwa katika Bunge tutahakikisha kwamba the first five members kwa hii list watakuwa ni hawa watu. Mnanielew? Yes, watahakikisha ya kwamba kabla ya uchaguzi wametoka nje kwa zile communities zingine, hawatakubaliwa kutoa members kutoka Central tuseme, nilikuwa naongea juu ya DP. Ni kwa sababu tayari basi wale watu wengine kutoka districts zingine hawawezi kupigia hicho chama kura kwa sababu wanaona ni cha Central peke yake lakini watakuwa wakitoka kwa mkoa wao wanaenda North Eastern wanawa-promise ya kwamba tutawaweka the first four positions na tutahakikisha tutaweka akina mama kutoka sehemu hii. Basi itabidi watu hawa waone kile chama ambacho kinazingatia mambo yao. Kama pastoral communities, kile chama ambacho kimeweka Wamaasai katika nambari za juu, the first seats basi tutaenda kupigia hicho chama lakini je mukiona kile chama ambacho kimeweka pastoralists kutoka nambari 70 kuenda chini hamtapigia chama kama hicho. Kwa hivyo hivyo ndio watakuwa wakipata kwanza hiyo list. Itakuwa ni njia ya ku-attract communities nje ya mkoa wao kuwa-attract ili wapigie chama na ili wapate national outlook. Nafikiri tumeelewana sasa.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Hakuna kitu kama bait kwa sababu nimesema hiyo list baada ya wao kuenda katika mikoa zingine halafu wamechukua hiyo list ya 90 kabla ya elections wanapelekea Electoral Commission na no anindependent Commission. Kwa hivyo haitakuwa bait kwa sababu ile promise, mlifanya ile ahadi mliitoa mpende msipende Electoral Commission watawatumia hawa watu barua waambie chama hicho kimewachagua muende katika Bunge. Kwa hivyo hakuna bait ati kuwa-attract halafu tena kufuta kwa sababu hiyo list itakuwa kwa Electoral Commission.

Basi ningependa kuenda katika...

(Interjection)

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Asante bado sijakuja hapo, nilikuwa naenda hapo sasa. Nilikuwa naongea juu ya Lower House ama National Assembly. Membership itakuwa namna hiyo 210 kulingana na sehemu za wakilishi Bungeni na tisa kulingana na orodha ya vyama 90, usamahani. Halafu basi kuna hiyo Upper Chamber ama kumbi la juu ambapo sasa watakuwa members ama wajumbe ambao wataenda katika Bunge la juu itakuwa ni members mia moja na hawa members mia moja watakuwa wakitoka katika wilaya. Kuna members sabini ambao watatoka katika kila wilaya, sasa hivi kuna wilaya sabini katika nchi hii lakini Nairobi itakuwa iko na special status kama national territory. Kwa hivyo ninataka kusema ya kwamba kutakuwa na districts tisini na tisa kuongeza Nairobi ambazo zitakuwa sabini. Basi kila district itahitajika kuchagua mtu mmoja wa kuenda katika National Council. Hivyo basi kutakuwa na orodha nyingine ya watu thelathini ambayo Tume ya Kurekebisha Katiba ilionelea kwamba ipatiwe akina mama kwa sababu tukisema kwamba ni vizuri katika kila ukumbi kuwe na one third representation ya akina mama na bila kubuni mbinu fulani basi haitawezekana. Kwa hivyo basi Tume ilionelea kwamba mbali na mtu mmoja ambaye atakuwa akichaguliwa katika kila wilaya, wilaya sitini na tisa pamoja na Nairobi ambayo itakuwa sabini kutakuwa pia na Wajumbe thelathini ambao watakuwa ni akina mama. Na hawa watakuwa wakichaguliwa kulingana na mikoa, sasa kutakuwa na mikoa saba kwa sababu tunasema Nairobi itakuwa na special status kwa hivyo haitahesabiwa kama mko. Kwa hivyo basi kutakuwa na mikoa saba na hizo mikoa zitachagua kina mama wanne. Wakichagua akina mama wanne basi watakuwa ishirini na nane na Nairobi itapatiwa nafasi ya kuchagua akina mama wawili. Hivyo basi hawa watakuwa thelathini, hivyo basi hawa thelathini na wale tena sabini ambao walichaguliwa kutoka wilaya ama district watakuwa mia moja. Kwa hivyo hiyo ndio itakuwa composition ya National Council.

Kabla hatujaenda kwingine ningependa kujua kama tunaelewana ama kuna swala lolote kuhusu composition ya National Council.

Speaker: Umesema 30%.

Maurice Kepoi Raria: Sijasema 30% nimesema thelathini.

Speaker: ... (Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Yes wale kutoka province watakuwa wakichaguliwa na wananchi.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Hapana wakati tutakuja kwa elections utakuta kwamba kutakuwa na elections tofauti kati ya Upper Chamber na Lower Chamber kwa sababu fulani ambazo nitakueleza wakati tutakuja kwa election.

Speaker: Hizi positions zitagawanywa namna gani.....(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Basi mbinu hasa ya kujua ni wilaya gani zitatoa, kwa sababu huu ni uchaguzi wa moja kwa moja basi watu ambao wangependa kuania kwa uchaguzi huo wa province watajiwasilisha tu kwa Electoral Commission. Wale ambao wangependelea kugombea hivyo viti watajitolea kule na wachaguliwe vile hata hawa wajumbe wengine kutoka district vile wanavyochaguliwa. Kwa hivyo watajiwasilisha kwa uchaguzi na wachaguliwe katika ngazi ya mkoa.

Basi ningependa pia kuwaambia kwamba nia ya kuwa na Bunge mbili au nia ya kuwa na Lower and Upper Chamber ni kwa sababu wananchi walilalamika ya kwamba Bunge tulionalo hivi sasa ina nguvu nyingi sana na mara kwa mara huwa wanapitia miswada ambazo zinawapendelea wenyewe na wakiketi wanapitisha kwa urahisi. Wananchi walizungumzia mambo hasa walizungumzia kwa hasira sana kwamba Bunge la sasa wakati wanapoketi wakijadili mswada wa nyongeza za mishahara yao basi lile Bunge halitakuwa tena na upinzani na mswada kama huo unapitishwa moja kwa moja bila pingamizi na kutiwa sahihi na inakuwa sheria. Basi wananchi walionelea kwamba lazima kuwa na system ya checks and balances, lazima kuwe na mbinu ya kukadiria nguvu ambayo Bunge la sasa liko nayo. Hivyo basi wananchi walionelea ya kwamba ni vizuri kama kuna kumbi nyingine, chamber nyingine ya kuangalia ya kwamba hii kumbi ya chini haitakuwa na nguvu zaidi kwa sababu watakuwa wakipitisha sheria. Kumbi la chini likipitishia sheria fulani ama wakitoa mswada fulani ni lazima wapate approval kwa ile kumbi ingine ya juu, kwa hivyo haitakuwa ni kumbi moja inapitisha sheria bali itakuwa likitoka katika kumbi ya chini na hiyo sheria pia linapitishwa kwa kumbi la juu na hiyo litakuwa sheria. Pia kumbi la chini, kumbi la juu pia wanaweza kuanzisha sheria ama mswada, wanaweza kutoa mswada halafu wakipitisha wanalete pia kwa kumbi ya chini halafu wakipitisha basi iwe inakuwa ni sheria na kama kuna kumbi lolote ambalo halijakubaliana na mswada wowote, basi hautaweza kuptishwa.

Jambo lingine ni kwamba kulikuwa na mapendekezo ya kuwa na qualifications ya members of Parliament kwa sababu wakati huu kwa Katiba tunayo hivi sasa haielezi hasa mahitaji ya masomo ambayo Wabunge wetu wanapaswa kuwa nayo. Na ndio sababu kuna nyakati zingine ambapo kumekuwa na Wajumbe katika Bunge letu ambao hawaelewi hata miswada ambayo

inapitishwa katika Bunge, wengine hawaelewi Kiswahili, hawaelewi Kiingereza kwa hivyo ilikuwa mambo yao ni kuenda pale na kusahihisha allowance na kulala hapo hadi Bunge itakapofungwa na wakienda katika constituencies wanaenda kuambia wananchi ya kwamba serikali imefanya hii na serikali imefanya vile na kumbe wanasikia habari hizo kwa fununu. Hivyo basi wananchi walisema ya kwamba ni vizuri kwanza zaidi ya yote Mjumbe awe ni Mkenya na katika National Assembly ama kumbi la chini, mahitaji ni kwamba Mbunge awe na miaka ishirini na moja. Lower limit litakuwa ni miaka ishirini na moja na kuenda juu lakini kwa National Council ama kumbi ya juu kwa sababu linaitwa ni kumbi la wazee na unaona hawa watu wanawakilisha sehemu kubwa kuliko constituency, wanawakilisha district ama wanawakilisha province ni lazima wawe ni watu ambao wamekomaa. Kwa hivyo haitakuwa tena ni miaka ishirini kwa kumbi la juu bali minimum qualification ya kuenda katika kumbi la juu itakuwa ni miaka thelathini na tano.

Educational qualifications, Tume hii ilionelea kwamba educational qualification ya kuenda katika Bunge iwe ni minimum ya form four na iwe mtu amepita vizuri. Pia wajumbe wanatakiwa wawe wanaelewa na kufahamu, kuandika na kusoma Kiingereza na Kiswahili. Katika qualification ya lugha pia, imesemekana kwamba wale walemavu ambao wanatumia sign language ama wanatumia lugha ya ishara, pia hiyo itakuwa ni qualification. Kama mtu mlemavu anaweza kutumia sign language na hawezi kuandika Kiingereza ama kuandika Kiswahili lakini anaweza kutumia lugha ya ishara basi hiyo ni qualification ambayo itamwezesha kuwa kuania kiti ya ubunge. Pia Wajumbe wetu wanahitajika wawe morally and ethically upright. Qualification hii ni kusema ya kwamba ni vyema kabisa Wajumbe wetu, wakiwa ni akina mama wawe wameolewa, wawe wako na familia. Kama ni mzee ni lazima awe ako na bibi, ako na familia na wanaishi kwa furaha. Sio kusema ya kwamba pengine ameo na tena mzee amempatia bibi talaka kwa hivyo hawaishi pamoja. Ni lazima kuwe na moral na ethical qualification, iwe a man or a woman must be married and happily married.

Jambo lingine kuhusu Wabunge ni kwamba wananchi kwa Katiba hii wamepewa idhini ya kutimua Wabunge ambao ni wazembe. Kuna provision katika kipengele cha 112...

(Interjection)

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Okay, tutaendelea, ni maoni, ni vile tu mnajua kwa jamii ya Kiafrika ikiwa ni moral wanakumbuka kwamba pengine mzee ambaye ako na bibi ama pengine mama ambaye ako na.... Wewe unaongea kama dot.com.

Speaker: Dot com lakini mimi ninawakilisha wote.....(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Asante sana.

Speaker: Hata wananchi wataona kwamba kweli nawakilisha dot. Com.....(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Very good, asante.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Asante. Hata mimi nafurahi kwa sababu sasa nitawania Ubunge.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Asante sana.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Thank you very much. Don't even labour on that, I have taken note of it. Thank you.

Speaker: ...(Inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Okay, thank you very much that, one has been taken very seriously.

Pia nilikuwa naongea juu ya kutimiliwa kwa Wabunge. Wananchi wamesema ya kwamba mara kwa mara Wabunge ambao walichaguliwa huwa wanatukomea Nairobi na hawarudi tena kuwakilisha watu katika sehemu ambayo ilimchagua na hivyo basi wananchi wamesema lazima tuwe na nguvu ya kuweza kufuta hawa Wabunge Kazi. Na wananchi kwa kusema kweli, majirani wetu hapa Uganda wao wamewahi kufanya hii na katika wakati huu Katiba ya Uganda ni kati ya Katiba ambazo zimekomaa sana katika Afrika. Ni Katiba ambayo imefana sana, kwa hivyo pia Wakenya waliona ni kwamba kama kuna Wabunge ambao wanakuwa wazembe ambao hawawakilishi ni vyema wawe na idhini ama wawe na nguvu katika Katiba hii ya kuweza kuwatimu. Basi iwapo hamjatosheka na kazi ya Mbunge wenu, Katiba hii imesema ya kwamba ni vizuri mkichukua sahihi ambazo zinafika asilimia thelathini ya wale watu ambao walisajiliwa kama wapiga kura. Baada ya kupata sahihi hizo mnapeleka kwa Speaker wa Bunge halafu Speaker wa Bunge atapeleka hayo malalamishi kwa Electoral Commission na kuambia Electoral Commission ya kwamba waende katika ile constituency ambapo malalamishi yametoka, waende wathibitishe kwamba malalamishi ya hawa wananchi ni ya ukweli.

Basi baada ya siku saba Electoral Commission watarudi tena kwa Speaker waende kuthibitisha kama ni kizingizio ama ilikuwa ni mambo ya kweli. Na iwapo ni kweli kwamba Mjumbe huyo ako na kosa fulani na kwamba wananchi hawaridhiki na yeze basi Speaker wa Bunge atatangaza kwamba hicho kitu ni wazi na hapo baadaye kutakuwa na uchaguzi mwengine.

Nilikuwa nimezungumzia juu ya elections mara mbili kwa sababu tumesema sasa kuna kumbi la juu na kuna kumbi la chini na kumbi la chini, ile National Assembly vile mnavyojuua hivi sasa inakuwa na awamu ya miaka mitano. Parliament mnavyo jijua hivi sasa iko na five year term ambapo baada ya miaka hiyo Bunge huwa linavunjwa. Kwa hivyo National Assembly ama kumbi la chini hata sasa litakuwa na awamu ya miaka mitano lakini kumbi ya juu au National Council itakuwa na awamu ya miaka minne peke yake. Kwa sababu ya kuwa na uchaguzi mara tofauti wananchi walisema ya kwamba kuna nyakati ambapo Bunge linavunjwa na pengine kuna janga la taifa na Bunge lote litakuwa nyumbani kwa hivyo hakuna Bunge linaweza kujadilia janga la taifa kama hilo. Kwa hivyo ilikuwa ni maoni ya wananchi ya kusema ya kwamba iwapo kuna kumbi moja ambalo liko na miaka minne na kuna kumbi lingine ambalo liko na miaka mitano basi hakutakuwa na wakati moja ambapo hakuna Bunge linaloketi katika Bunge. Kwa hivyo kama kuna janga la taifa lazima kuwe kuna Bunge moja ambayo itajadiliana kwa mswada kama huo.

Pia nilikuwa nimezungumzia juu ya mambo ya mishahara ya Wabunge ambao wamekuwa wakijipatia mishahara ya hali ya juu kwa sababu sasa wako na Commission ambayo ni independent, Parliamentary Service Commission na mapendekezo ya Katiba hii ni kwamba Wabunge hawatakuwa ama Parliamentary Service Commission haitakuwa na idhini ya kujiongezea mishahara. Kutakuwa na Salaries and Remuneration, kuna Tume ya Salaries and Remuneration ambayo imebuniwa na Katiba hii, ambayo itakuwa ikijadili mambo ya mishahara ya Wabunge, mishahara ya Mawaziri, mishahara wa Rais, mshahara wa Makamu wa Rais, mshahara ya Mabalozi na mshahara ya wafanyakazi wa ngazi za juu katika serikali. Kwa hivyo Salaries and Remuneration Commission itakuwa ikihakikisha kwamba watu hawa ambao wako katika nyadhifa za juu serikalini watakuwa na harmonization of salaries kwa sababu si haki kwa Wabunge kuketi na kujipatia mishahara ya hali ya juu na kumbe kuna watu wengine ambao wako na qualifications kama wao ambao wako katika nyadhifa zingine za serikali lakini wao hawawezi kujiongezea mishahara. Kwa hivyo Salaries and Remuneration Commission vile imependekezwa katika Katiba hii ndio itakuwa ikijadilia pia mishahara ya Wabunge.

Jambo la mwisho ambalo ningependa kuzungumza juu ya Bunge ni kwamba sasa Rais wa nchi hatakuwa na nguvu ya kuvunja Bunge kwa sababu wananchi wamesema ya kwamba iwapo uvunjaji wa Bunge utakuwa kwa mikono ya Rais basi atakuwa akitumia hiyo kama mbinu ama kama chombo cha kujinufaisha kisiasa na inatia wasiwasi wananchi kwa sababu wanakaa katika hali ya taaruk, hawaelewi wakati wa kuvunjwa kwa Bunge. Hawaelewi ni wakati gani uchaguzi utakuwa na pia itafanya vyama vingine viwe na wasiwasi na hali ya kutokuwa wamejitayarisha kwa uchaguzi. Kwa hivyo sasa itakuwa ikihitajika kwamba itakuwa ni shughuli ya Bunge. Wakati Bunge litakapofunguliwa kulingana na hii Katiba itakuwa ni shughuli ya wiki ya kwanza kwa Parliament kupanga ratiba yao kutoka mwanzo hadi mwisho ili katika Katiba watakuwa wakieleza wananchi kwamba Bunge litafunguliwa siku hii na wataenda recess ama wataenda mapumziko tarehe hii na Bunge litavunjwa tarehe fulani. Pia siku ya uchaguzi itakuwa katika Katiba ili mwananchi baada ya uchaguzi uliopita atakuwa anajua uchaguzi ujao utakuwa ni tarehe fulani, mwezi fulani. Kwa hivyo tarehe ya.

.....na wote tutafufahi tukijadiliana. Asante

George Nakholi: Asante Bwana Raria kwa hayo umezungumza juu ya Bunge na sasa ni wakati wananchi wa Narok North wanaweza kuuliza au kujadiliana na sisi na mtoe maoni kama vile mlikuwa mmeanza kutoa ili tuendelee tumalize malize kwa sababu sasa tumefika saa kumi na dakika kumi, kama kuna jambo moja ama lingine, sasa ni wakati wenu.

Pauline.....: Kwa majina ninaitwa Pauline..... na ni swali tu ninauliza kwenu. Mnasema sheria itakuwa, kama ni Bunge, wananchi watakuwa wakijua ni siku fulani Bunge litavunjwa na ni siku fulani Bunge litafunguliwa. Na je, saa hii ikifunjwa wakati huu kabla hamjamaliza hii Katiba itakuwa namna gani?

Maurice Kepoi Raria: Jawabu ambalo ninaweza kuwapatia ni kwamba, iwapo Bunge litavunjwa kabla ya kutimia kwa hii Katiba, basi kazi ya Katiba itakuwa imewekwa katika shida kubwa sana kwa sababu composition ya National Conference inahitaji kwamba kuwe na wabunge wote. Na iwapo Bunge litavunjwa, inamaanisha ya kwamba kuwe na wote watakuwa wamefutwa kazi. Kwa hivyo itakuwa ni shida kubwa sana kwa Constitution Review Commission kuweza kwenda kwa National Conference na vile ninaweza kukwambia itakuwa ni shida kubwa sana kwa Commission kuendelea na kazi yake.

What I am saying is that, should Parliament be dissolved at this moment before the National Conference, then the operations of the Constitution Review will be in jeopardy

Speaker: (Maasai Dialect).....

Maurice Kepoi Raria: Because in the National Constitutional Conference(interjection)

Speaker: (Inaudible Masaasai dialect)

Maurice Kepoi Raria: All members of Parliament are supposed to be in the National Conference.

Speaker: (Inaudible Maasai Dialect).....

Maurice Kepoi Raria: (Maasai dialect).....kutakuwa na nini itafanyika na nitawajibu pia kwa kizungu. What I want to say is that should this happen, then it is not within the mandate of Constitution to speculate what is going to happen.

Speaker: (inaudible Maasai Dialect).....

Maurice Kepoi Raria: But in short I can tell you that it might not be desirable.

Speaker: Inaudible.....

Maurice Kepoi Raria: Thank you.

Mwaniki: Jina ni Mwaniki,hawa wamama wamesema kwamba kutakuwa na wamama wanen, nafikiri kungekuwa na wamama wawili na wazee kwa sababu unaona kwamba District the ita-elect members waende National Council, halafu sasa wamama wanen wanakuwa elected na Province, which means they are going to be more stronger. Watakuwa na numerical majority ama strength katika National Council. Kwa hivyo tungenesema hivi, wamama wawili na minority groups ama disabled na pia kuwe na wazee wawili ama mzee mmoja. Wanaumme wawili au wazee.

Halafu pia kuna kitu kingine ambacho ningalipenda kuchangia kuhusu religion, ambayo ulikuwa umesema ukija kuongea uchangie. Mimi nina-propose kwamba, Constitution inge-draft kwamba kuwe na religions kama Christianity ambapo all other denominations zitakuwa ndani yake, kuwe na Hindus ,kuwe na Muslim, kuwe na JainS, Jainism kuwe na Buddhist,kuwe na Judaism ama the Jews, halafu hizo ndizo zingelikubaliwa na Serikali. Halafu hizo zingine kama cults and occults should be illegal or illegitimate in the Constitution. I know any other religion in the world apart from those ones (inaudible)

Maurice Kepoi Raria: And African Traditional religion?

Mwaniki: Yes the African Traditional Religions, I forgot that one. So.....(Inaudible)when you say just have the freedom to worship, we say our society to free and all people are free to worship but you must spell out and enumerate acceptable religions in the world.

Halafu pia mambo ya citizenship, sijui kama tutaguzia huko kwa sababu ninaona kama tunamaliza. Tungenesema kwamba tuwe na dual citizenship between... a citizen of Kenya should be a dual citizen (interjection).....

Maurice Kepoi Raria: It is allowed

Mwaniki.....: This is different from what I am saying, dual citizenship for federal states, for the Province that you come from, and (inaudible) department for Nation itself In other words you are a citizen of your local District and Province and at the same time you have a citizenship of the Nationality.

Speaker: Inaudible.....

Mwaniki: That one again should be another point. You should also be a dual citizen of Kenya and many other countries.

Speaker: (Inaudible).....

Speaker: Sasa kwenye hii desturi hakuna mbahali penye mama hawesi kutoka. Na katika ile destri tangu Mungu alipoumba ulimwengu, tangu enzi za Adam ana Hawa, alikuwa bibi akitoka Turukana aje Maasai hawesi kuja kuzaa Turukana, atakuja kuzaa Maasai. Kama anatoka kwa Wabaluhyia huko Bugusu, aje aolewe Mijikenda, hawesi kuzaa Buguzu huko, anaenda kuzaa Mijikenda. Kwa hivyo mtoto wangu akiolewa Germany, yaani wangu ni yule wa kutoka Kenya, akiolewa huko, atazaa wajerumani, na waende huko kwa sababu mpenda roho hula nyama mbichi.

Maurice Kepoi Raria: Lakini ijapokuwa pendekezo lako linaweza kufurahiwa katika sehemu hii ya nchi, ningependa kukupatia msimama wa Katiba, kwa sababu Katiba imesema ya kwamba mtoto yeoyote atakaye zaliwa na mzazi mmoja ambaye ni mwana-Kenya huyo mtoto ni Mkenya. Hiyo ndio stand ya Constitution. Yule aliyezaliwa katika Marikani ama Ujeremani, ikiwa mmoja wa huyu mzazi ikiwa emmoja wao ni citizen wa Kenya, basi huyo mtoto huyo ni.....(interjection)

Speaker: Na baba yake ama mama yake akiwa wa nchi nyingine?

Maurice Kepoi Raria: Mradi mzazi mmoja awe ni Mkenya

Mwaniki....: Bwana Commissioner ingine nilikuwa ninasema ni dual citizenship, between a Kenya citizen and another country. Like if you can became a citizens of Kenya, America or Britain or whoever. Halafu lingine ni kuhusu vile wamesema kwamba citizenship is. (inaudible) ningelipenda kusema kwamba Kenyans should be citizens of East African Community and should be entitled to have a passport of the East African Community as well as the Kenyan Passport and ID.

Then again on citizenship, illegal immigrants should be penalized because since this Draft Constitution is so lenient and mild on illegal immigrants, they are not deported. They should be penalized and deported. It is lenient and tends to favour the people like refugees who just come to Kenya and get citizenship through application.

Then finally naturalized citizens should not vote, for a specific period of time. If you have stayed in Kenya for seven years you became a naturalized citizen of Kenya , ndio Draft imesema, lakini tunataku kuwa kwamba, according to me Naturalized Citizens should start voting fifteen years or more often, or more often after gaining citizenships.

Speaker: Inaudible.....

Mwaniki:..... But you see they are just naturalized, they are not born in Kenya, they just came to stay here for seven years, how come somebody from another country comes to stay here for seven years and becomes a citizen then starts voting? I don't

think it should happen, because when you go to another country you are not entitled to vote in that country. So they should be given a span of time to stay in Kenya and become natural citizens and they start voting after maybe fifteen years or more.

Maurice Kepoi Raria: Perhaps to compromise what you are saying and her sentiments is that for naturalization I think there should be time where you have set a time limit, when this naturalized citizen should have stayed in Kenya before gaining citizenship. Because once you have naturalized a citizen and he has gotten citizenship through naturalization, then he will enjoy every other right from that minute.

Speaker: Katika Katiba ya Kenya ambayo ni moja ya Katiba za ulimwengu mzima, hakuna mtu atawezu kuwa President wa Republic ya Kenya kama zi mzaliwa wa Kenya. Haya, mtu ambaye amekubalika hata kwa njia ya naturalization ama nyingine hawezu kukubali wa awe a member of Parliament. Kwa maana, tukipewa uhuru tutumie huo uhuru kwa njia inayostahili. Kwa maana hapa ni Kenya tunaongea juu yetu na watoto wetu. Na sasa akili imeongezeka duniani kwa hivyo kisha kunaweza kuja mtu ambaye ni mkora na ama pesa nyingi sana, aje atafute naturalization, kesho amenunua nyinyi na achaguliwe President, amechaguliwa Member of Parliament, na amefanya mambo mengi. Watoto ni wetu hatubagui, lakini yule ameamua kwenda kuoa hata kama ni wangu na ameenda kuoa uingereza, mwanaume aende kuoa uingereza na bib yake amlete hapa. Msichana wangu ameenda kuolewa uingereza wacha waende wakae uingereza kwa maana hilo ni chaguo lake. Sijasema ni vibaya, na sijasema ni vibaya kuolewa. Hapana hiyo ni segregative, nimekubali aende so long as she is sure she is making the right decision. Lakini si aende aolewe atuletee wa-negro hapa. Sorry, like a dot. com. we must also talk about dot.com rights. Kwanza hawa ma dot.com tunataka hata nyinyi mjue haki zenu. Yes Bwana Commissioner mjue hata haki ya dot.com. Sikusema .com ni mtu amabye hajui haki, dot.com ni mtu ambaye ni very intelligent. Dot.com ni mtu ambaye anajua haki zake, ni mtu ambaye anataka kuchangia maendeleo ya nchi katika njia zote. Si asiwe mtumwa wa DP, si awe mtumwa wa nchi geni au ama wa pahali pengine. I think that is what I mean by dot.com

Mwaniki: Halafu, finally, my last point is that I want to pendekeza kuhuzu the name of the National council and Legislature. We should just call it Senate for simplicity and party then the Lower House should be called the House of Representatives. Because it seems that we are a federal republic after we adopt this Constitution.

Maurice Kepoi Raria: Yaani majina yeye anajaribu kutoa majina mafupi, juu ya hizi kumbi mbichi pili. Na ninaweza kukwambia kulikuwa na mjadla wakati Ma-Commissioner walikuwa wanajadiliana juu ya majina, nominclature juu ya hizi kumbi. Hiyo idea ya house of Senate na House of Representatives iliweza kuja lakini, sasa walisema wakita Senate basi itaonekana kwamba ni Majimbo, na wewe ulishasema juu ya huo wasiwasi wako kwa kuwa yaonekana kama tuko katika majimbo. Lakini hata hivyo nimenakili maoni yako na tutayafikisha katika Commission.

Mwaniki.....: Ninataka kurudi nyumba kidogo for one minute. When you were talking about land issues I forgot to tell you something. That we should be create parks and rest places and gardens. Because we see that every town you just get brown

revolution against the green revolution. We just just erect houses and forget to create parks. So lets see that we have parks and then the acquisition position of public utility for the common good. Thank you.

Maurice Kepoi Raria: Hiyo ni kazi ya District Councils kuhakikisha katika miji kuna

Speaker: Mimi ninajibu yale Kirunga aliongea ya wamama. Na ningetaka kusema sisi wamama, hii Katiba mpya imetuiali sana. Na vizuri sana hii Katiba mpya imekuja sababu, sisi hatutambuliki hapa Kenya wamama kwa Katiba ya kitambo. Na hii Katiba inkuja kuona sisi wamama tukianchwa nyuma pia hali sisi ni binadamu. Na hata sisi ni watu, na bila mimi kunioa wewe hiyo boma siyo boma. Sasa hii Katiba mpya ikaona heri tuwajulishe tunawapenda, na ndiposa tumepatiwa hivi viti juu sisi hatuna nguvu ya kung'ang'ania viti, kwa sababu hatuna pesa. Sasa wakaonelea wanaumme wana pesa ya kung'ang'ania viti na wamama bado hawana. Sisi tumeolewa na Bwana tunaomba Bwana yako unaenda kumuomba akusaidie pesa za kununua nguo. Sasa hii Katiba ikasema heri tuwapatie viti, tuwa-promote ili waone hata wao ni watu. Halafu nasi tukiinuka kidogo wale walipaatiwa watakuja kung'ang'ania viti kama wamepata nao kitu kidogo. Kwa hivyo tunaonelea hivyo viti ambavyo mmetupatia hakuna haja ya kgawa vipatiwe wazee at mbili mbili. Waja sisi tupate hizo, nyinyi mng'ang'ane ndio mko na nguvu za kwenda America na kila pahali mkirokota pesa, iala mimi nitatoa wapi? Kwa hivyo mtujali na mjaribu sana kushika hiyo na msipatie wanaume tena.

John Oketch: Kwa majina ni John Oketch kutoka CPTA. Mimi nitazungumzia juu ya Bunge kwa sababu tumeonelea kwamba kwa hii Katiba mpya tunaenda kuwa na fursa mpya. Kwa mfano Rais anaenda kupunguzwa madaraka yake, hatakuwa na Executive powers, which is good. Tunaonelea, hapo, kwa sababu ukiangalia saa hizi hii current Constitution inaonekana saa hizi ndio ana Executive powers yeze ana ile nguvu ya kuchakua from the Vice President, hizi Administrative positions mpaka chini kabisa. Sasa hapo tunaonelea inanyima viongozi wengine wenyewe tunachakua kutoka mashinani kwenda juu uwezo. Sasa tumeonelea ya kwamba kwa mfano saa hizi Constituition ya Kenya inaenda through Draft Constitution, ninaona iko na Prime Minister which is good. Sasa kati ya Prime Minister, tunaonelea kwamba yeze ndiye atakuwa anachagua waziri. Nao mawaziri tunaona kwa draft Constitution inaonekana kwamba mawaziri wanatoka outside the Parliament. Hili jambo tunaonelea ni nzuri kweli? Ndilo nilikuwa ninataka kuuliza.

Maurice Kepoi Razria: Natumaini mko hapo, ukurasa wa kumi na moja ndio utapata mfumo wa uchaguzi. Na tunasema ya kwamba, mambo ya uchakuzi ama mfumo wa uchafuzi umekuwa hata kwa wakati huu ni jambo ambalo lazima linafikiria na wakenya wengi kwa sababu wakati umeyoyoma na hivyo basi ilikuwa pia ni jukumu la Tume ya Kurekebisha Katiba waweze kutoa mwongozo kuhusu uchaguzi na kwamba uchaguzi umekuwa ni wakati mzuri sana, ama imekuwa ni fursa kwa wananchi kuweza kuwaandika kazi mpya viongozi walio wachagua na pia ni fursa ya wananchi kuweza kufuta kazi wale viongozi wazembe ambao waliwachagua ambao hawajatimiza malengo yao. Basi inakuwa hasa katika uchaguzi ndio tunaona msingi wa democrazia wa nchi. Kwa hivyo mara kwa mara kila baada ya ya miaka mitano katika nchi yetu huwa kunakuwa na uchaguzi wa jumla ama General Election ambayo kwa hivi sasa tunaitazamia na kwa wakati huo wananchi tena wanapaswa katika

demokrasia ya nchi yao kuweza kuwaandika kazi upya viongozi ambao wanawapenda. Na katika uchaguzi kuwa wananchi watatazamia kuchagua wale viongozi ambao ndio sawa kabisa, ambao wanaona ndio stadi na ndio viongozi ambao ni bora kuwaongoza na ndio wanajali masilahi yao.

Na basi tulisema kama mwenzangu Bwana Nakholi alisema ya kwamba umri wa kusajiliwa kupiga kura itakuwa ni miaka kumi na nane na zaidi. Na mambo ambayo ni mpaya katika uchaguzi huu ni kwamba wananchi walisema tunahitaji kuwe na transparent ballot boxes. Wananchi mnakumbuka ya kwamba wakati wowote mnapoenda kwa uchaguzi huwa mnaletewa box nyeusi kama mtambo huu wa kunasia sauti na kwamba hamuwezi mkajua ni nini kimo ndani ya box ile. Kwa hivyo wananchi wamesema wanahitaji katika uchaguzi kuwe na transparent ballot boxes. Transparent tunasema ni kitu wazi kama hiki kwa sababu tunawezakukatilia ni nini kiko ndani. Imekuwa ni chanzo cha kuvuruga kura ama rigging kuleta hizo black ballot boxes ambazo mara kwa mara kumbe hata zikiletwa tayari kuna kura zingine ziko pale ndani. Na wananchi wamesema tunahitaji uchaguzi ambao ni wa haki na huru na uchaguzi ambao ni wa wazi. Kwa hivyo Katiba mpya imeamua ya kwamba katika uchakuzi iwapo Katiba hii itaenda kutimia, basi uchaguzi utakao fuatia ni lazima uwe na transparent ballot boxes.

Pia pendekezo lingine la Katiba hii ni kwamba uhesabu wa kura ama kutumbukiza zile ballots katika hizo boxes, casting of votes na kuhesabu kwa kura, kutangaza kwa matokeo ya kura itakuwa ikifanya na presiding officer kwa hicho kituo ambapo mmeopia kura. Sijui kama tunaelewana hapo. Huwa kwa kawaida baaday ya kutumbukiza ballot zanu kwa zile boxes mnaenda nyumbani na hata hamjui kama hizo boxes zinafika mahali ambapo zinaenda kuhesabiwa. Kwa hivyo wananchi wanasema sisi tunataka tuweke kura kwenye zile boxes ambazo ni transparent, zi-hesabiwe, zi-record-iwe na zidhibitishwe na agents wa kila chama cha kisiasa halafu matangazo itangazwe papohapo.

Halafu hayo matokeo baada ya kudhipitishwa na agents wa kila chama na wananchi wote wamekubaliyana kwamba ilikuwa ni ya wazi, wananchi wanaweza kwenda nyumbani kwa amani halafu matokeo hayo ndiyo yatapekwa kule head quarters mahali ambapo zi zitenda kuesabiwa na wale agents watakuwa pale kwa sababu wananchi wamehofia ya kwamba, imekuwa hii sababu ya kupeleka boxes na hatujui kuna nini ndani, kumbe boxes zingine huwa zinapotea halafu mjumbe amabaye ulimchagua na mlikuwa na hakika kwamba mlimchagua kwa wingi, unakuta kwamba ye ye ndiye ameshindwa.

Pia kuna mambo ya ghost candidates, unakuta kwa ucahguzi mwengine kunaweza kuwa kuna mjumbe ama diwani ambaye hajapingwa na mtu ye yeyote. Katiba hii inasema, ijapo kuna uwezekano wa kukuwa na waakilishi ambao hawatapingwa, ni vizuri wananchi wajitokeze katika uleuchaguzi ili waweze kuhesabiwa ili ijulikane kuwa huyu mjumbe wako amepita kwa kura asili mia ngapi. Tunaelewana? Hata mahali kuna unopposed candidate, ni vizuri akijiwakilisha katika kituo cha uchaguzi kusudi Tume ya uchaguzi, Electoral Commission waweze kujua huyu mjumbe fulani hajapingwa lakini amepita kwa asili mia fulani. Kwa sababu msipojiwasilisha pale Electoral Comission wanaweza kufikiri kwamba pengine kulikwa na uoga wa wale watu, pengine kulikuwa na vita ama intimidation kwamba mkienda pale mtapigwa ama waweza kupata ya kwamba hata yule mjumbe mnasema kwamba hajapingwa huenda akapita kwa kura ambazo ni za chini, pengine ni asili mia ishirini pekee yake. Kwa hivyo

ni vizuri mkijitokeza kwa wingi hata kama hakuna mtu anayepinga mjumbe wako, jiwasilishe katika kituo cha uchaguzi.

Basi jambo ningalipenda kuwahimiza ni kwamba kama mngeangalia haki na jukumu za raia, ni jukumu la raia na ni haki, na ni a responsibility ya a good citizen kuhahakisha kwamba unajiwakilisha katika uchaguzi. Wananchi ningalipenda kuwaambia ya kwamba, kumekuwa na uzembe wa makusudi, kwamba wewe uko na voting card, ama kadi ya kupiga kura, lakini wakati wa kura ukifika unaketi nyumbani bila sababu yejote bila kwenda katika kura. Lakini sasa kwa haki ama jugumu za raia mwema ni kwamba raia mwema ni yule amabaye kila wakati kukiwa na kura kama ako nayo aende apike kura. Hii ni kwa sababu unakuta wananchi ambao wako na akili timamu, ambao huenda kanisani, watu ambao ni waja Mungu na ni watu wenye nidhamu na ni watu ambao wanaeshimiwa, hao ndio huwa hawaendi kwa kupiga kura. Hasa watu ambao wanaenda katika makinisa ambao ndio tunaamini ni watu ambao wanaweza kufanya uchaguzi wa haki. Lakini hao husema hiyo ni mambo ya watu wa siasa kwa hivyo waja hao waende kule. Basi wale watu ambao ni wabaya katika jamii ndio hujiwasilisha katika vituo vya kupika kura na basi wanachagua viongozi wabaya kama wao. Tunaelewana hapo?

Kwa hivyo ni jukumu lako mama ama mzee uweze kutekeleza haki yako ya kidemokrasia, uweze kufika katika kituo cha kupiga kura na uweze kushiriki katika uchaguzi kwa sababu usipofanya hivyo itakuwa umerudisha nchi nyuma na utasababisha wale watu wabaya kuweza kujiwasilisha katika uchaguzi na tupate viongozi wabaya. Na wewe ambaye ujapika kura, na hujapiga wewe ni mtu wa kwanza kulalamika ukisema ya kwamba hawa viongozi waliochaguliwa ni wabaya sana. Nani wewe ndiye haukuchukua jugumu jugumu la kuchakua yule kiongozi mzuri ambaye unampenda.

Na ningependa kuzungumzia kwa ufupi juu ya political parties, vyama vya siasa ili niweze kushikanisha hayo mambo pamoja na elections kwa sababu zina uhusiano wa aina iliuweze kuokoa wakati ambao unaenda sana. Na tunasema ya kwamba, political ama vyama vya kisiasa vinahitajika viwe na national character. Sasa ni Electoral Commission ama Tume ya Uchaguzi ndio itakuwa ikisajili vyama. Haitakuwa tena usajili wa vyama nafanywa na Registrar of Societies. Hilo jambo litaenda liwe likifanywa na Electoral Commission ambao watakuwa wakihakikisha kwamba, kabla hawajasajili chama chochote, ni lazima chama hicho kiwe na national character, ni lazima ipate support ya percentage fulani katika kila mkoa katika nchi ili kiweze kusajili kwa sababu, wananchi wameofia kwamba kuna vyama vingine ambavyo ni vya kikabila. Ambavyo vinapata support kwa mkoa mmoja. Na sasa Electoral Commission itahakikisha kwamba vyama kama hivyo ambavyo viko na support ama vinaungwa mkono kwa mkoa mmoja basi. Electoral Commission ama Tume ya uchaguzi haitasajili vyama kama hivyo.

Pia kwa Katiba hii, kuna pendekezo ya kwamba vyama vya kisiasa vitakuwa vikipata fedha kutoka kwa Serikali. Itakuwa wakati wa kupanga Budget kutakuwa na fedha kiasi fulani ambazo zitatengewa vyama vya kisiasa. Na fedha hizo vyama vitapatiwa kulingana na uwezo wao katika Bunge lililoko. Kwa hivyo chama ambacho kina wabunge wengi kwenye Bunge ndicho kitapata fedha zaidi. Na chama ambacho kiko na waakilishi wachache katika Bunge wapata pesa chache.

Lakini licha ya kuwa watapatiwa state funding ama watapata fedha kutoka kwa Serikali, vyama hivi vinahitaji viwe vikikadirio

pesa hizi ambazo zinapewa na Serikali. Kwa hivyo Katiba hii imetua pendekezo kwamba, vyama vitawajibika kuwa baada ya kila miezi tatu wanapeleka vitabu vyao vya accounts kwa mkadiriaji wa Serikali ama Auditor General, kuhakikisha kwamba fedha hizo za Serikali zimetumiwa kwa njia ilio wazi na kwamba hazijhatumiwa kwa manufaa mengine ambayo Electoral Commission hawajatoa. Kwa hivyo Political parties zitapata state funding lakini ni lazima wakadirie matumizi ya pesa hizo.

Katiba hii inasema watu wasio wanakenya, watu wasio kuwa raia ama kampuni zozote za kigeni hasiwezi kutoa fedha zote kwa vya vya kisiasa. Non-citizens and foreign organizations should not fund Political parties. Kwa hivyo Katiba hii inasema ya kwamba ukiwa wewe siyo Mkenya, ukiwe wewe ni kampuni au shirika la kigeni haupaswi kutoa pesa zozote kwa chama cha kisiasa. Lakini wakenya wale ambao wanapenda vyama vyao, wanaweza kutoa donation yao kwa political parties. Kwa hivyo mbali na kupata state funding, wale watu wanao-unga vyama vyao mkono, wanaweza pia wako na uhuru wa kusaidia vyama vyao kwa kuwatolea fedha. Lakini kama wewe si Mkenya, kama wewe ni kampuni ya kigeni, haupaswi kudhamini chama chochote cha kisiasa.

Jambo lingine ambalo ningalipenda kuzungumzia ni kwamba, Electoral Commission ama Tume hiyo ya Uchaguzi ambayo ndiyo itakuwa ikifanya usajili wa vyama, itakuwa na uhuru wa kukata kusajili vyama fulani. Kutakuwa na cretria ama kutakuwa na mbinu fulani ya kukataza kusajiliwa kwa vyama. Na Katiba hii inasema kwamba, vyama vyovoyote ambavyo vimeundwa kwa msingi wa kidini havitasajiwa, vyama vyovoyote ambavyo vimesajiliwa kwa msingi wa kikabila havitasajiliwa, na vile ambavyo vinajihami kwa silaha, mnajua kwa mfano vyama kama mngiki ambavyo tunajua vinajihami kwa silaha hatari, vyama hivyo havitaweza kusajiliwa na Ectoral Commission. Kwa hivyo Electoral Commission inaweza kukataa usajili wa vyama ambavyo viko na msingi wa mambo kama hayo. Pia vyama mbavyo vinasababisha vurugu katika siasa zao ama katika campaign, vyama vyote ambavyo vinajulikana kwa uzushi na vurugu, ama violence, vyama kama hivyo vitatazwa usajili.

Jambo lingine ni kuhusu watu ama wajumbe ambao wanahama kutoka chama kimoja hadi. kingine, Katiba hii inasema kwamba watu hao wamekuwa ni gharama sana kwa fedha za umma kwa sababu wakiti wowote wakihamahama kutoka chama kimoja hadi kingine, inakuwa ni gharama sana kwa Taifa na basi tumesema ya kwamba iwapo kuna mjumbe yelete ambaye atahama chama chake hadi chama kingine basi kidi hicho kitatangazwa kuwa wazi na yeze hatakubaliwa kukombea katika chama kingine hati wakati wa uchaguzi ijao

Jambo la mwisho kuhusu vyama vya kisiasa ni kwamba hakuna chama chochote ... (tape ends words lost) to promote the interests of a political party. Wananchi walilalamikia na kusema ya kwamba vyama fulani vinatumia mali ya umma kufanyia campaign, wanatumia mali ya umma kama helicopter za police kufanyia capaign, vyombo kama vya KBC na hivyo basi Katiba hii imesema hiyo itakuwa ni kinyume na Katiba na itakuwa chama hicho kinaweza kushtakiwa. Wananchi ningefikisha hapo na ningefurahi nikipata maswali yenu.

Naiseku Yabani: Majina yangu ni Nasiefu Yabani, na kuna issue ya land ambayo nilikuwa nataka kuzungumzia. Kwa sababu

sisi kama jamii ya Wamaasai, kama kuna kitu kimetuadhiri ni ardhi. Na ningezungumzia kuhuSu ardhi hivi, ingawa tunasema kuhusu ile compensation kwa sababu tulitolewa kwa ile rdhi nzuri. Kwa sababu actually tuli-push-iwa kwa arid areas, sehemu ambazo ni kavu sana. Na pengine compensation itachukua muda, na nimeona kwa hii Constituion kuna mahali imekuwa very silent kwa issue ya land especially kwa sisi Wamassai, a marginalized group. Ni kwamba utakuta tuli-push-iwa kwa arid areas na utakuta ya kwamba hii imetu-affect sana especially sisi wakina mama ambao tunajua backbone ya economy ya community ni akina mama. Utakuta ya kwamba ardhi yetu ni arid, kwa hivyo chakula haikuwi na mambo kama hayo.

Tungependekeza kwamba as much as tunauliza compensation, tungetaka immediate compensation kwa sababu utakuta kwa hii Constitution tupewe a special consideration kwa sababu hii ardhi yetu kwa sasa inakuwa devalued, such that mtu akiwa in other places akipeleka title deed ya one hectare atapata loan ya million hata kumi. Lakini kwa ardhi yetu wanasema haina value, wanasema sasa hawezi wakatupa loans kwa hii land yetu. Na unajua ardhi ndio kila kitu, na sisi Masaai ardhi ndio kila kitu. Na tunajua ya kwamba ni kwa sababu ya hii marginalization utakuta hatujawekewa maji, na hatujapewa hizo resources, sasa hatuwezi tuka-irrigate land yetu. Na pengine kama tungepewa immediate compensation, tupewe hizi resources, ili tufanye ardhi yetu iwe na rotoma ili hata ardhi yetu iwe na value. Ndio sababu sasa tumekuwa backward hata kwa development. Ndio kwa sababu unakuta watu kutoka central wanaweza kuja hapa wanunue plot na wajenge, lakini sisi kwa sababu hatuwezi acess loan those facilities juu land yetu inakuwa kama haina value. Kwa hivyo tungeomba hiyo especially tupewe consideration as a minority and as a marginalized group. Ni hayo tu.

George Nakholi: Asante Naiseku kwa swali hilo au jambo hilo, tumeandika chini lakina vile tu nitasema kabla mwenzangu hajasema, Bwana Raria, ni ya kwamba kwa hii Constitution, tuna lile jambo ambalo linasema within two years, ya ku-enact hii Constituion, kutakuwa na jambo la Historical imbalance, kwa sababu Parliament itakaa na iangalie kamani miaka mia tatu ambayo Wamassai wamekuwa marginalized, kutoka 1904 au kutoka 1911, ili compensation ifanyike. Hili jambo haliko kwa Constitution straight lakini ni jambo hilo tumpendekeza ya kwamba hizo historical kinjustment injustices tulifanyiwa wakati wa ukoloni, ama miaka iliyopita, hivi karibuni wataangalia ni nini kinaweza kufanywa kwa zile marginalized communities. Wamaasai wakiwa mmoja wao, sana sana upande wa ardhi.

Speaker: Mambo ya ardhi ni moto kwa sababu ni sisi Wamaasai.....(Masaai Dialect).na ikiwa jambo la ardhi kama community ya Wamaasai, irrespective of wherever you are, ikiwa kwa wale wanao-itwa Elgon Maasai, utakuta kilio chao ni kimoja, Samburu, Baringo na hata Tanzania taabu yetu ni hiyo moja tu. Na hii Constitution ambayo inaendeea kuondoka, ambayo ni kongwe, although Constitution haiwezi kuwa kongwe kwa sababu ni barua na haizeeki, hiyo Constitution lengo na shabaha yake ilikuwa ni kunyang'anyang'a sisi ardhi, kwa njia ya(Massai Dialect)Hata hii sasa mnapo sema baada ya miaka miwili, mtu ambaye amepigwa kibogo siku my ingine akiambiwa aone kitu kingine ambacho ni suspicious bado ataogopa. Kwa sababu why do we have to post phone to two years later, whay not now? Kwa hivyo mimi ninasema jingie know. Si ati tunaambiwa tungojee tupiterishe halafu baada ya miaka miwili watu wamekaa kwa viti tuje tuambiwa sasa history, is history it can not be corrected. We want to correct history know.

Maurice Kepoi Raria: Asante sana Councillor na ninafurahi sana kwa sababu wewe ni mwakilishi mmoja wa wale wanaoenda National Constitutional kuhakisha hayo uakikishe hiyo mambo ya itaisha mwezi huu.

Basi ningewaomba tafadhalii kwa sababu tulikuwa tunaongea juu ya mambo ya election na political parties na tulimpattia huyo mama nafasi mzuri sana kwa sababu kwa kusema ukweli hatungepoteza hoja za muhimu kama hizo na ninafurahi Naiseku kwamba ulizungumzia hayo mambo na pia ningewapatia pia mchangie juu ya elections na juu ya political parties ili tuweze kwenda sehemu ya mwisho.

Na kama hakuna hoja yoyote kuhusu election process na political parties basi tutaenda kwa sehemu nyingine.

Speaker : (Inaudible).....

Maurice Kepoi Raria: Ningesema kwamba kama kuna shida zingine ama kuna jambo lingine lolote mtu anaweza fikiria, tukiendelea hata baada ya kwenda katika jambo lingine mtu anaweza zungumza tu baadaye.

Speaker: Pahali sikufuata ndugu yangu ni kwamba ni kwa nini kama tunataka hizi political parties ziwe state funded ni kwa nini tusipitishe katika Constituton kuwe tu na parties mbili tu Kenya, tuone kama tutaangamiza ukabila. Badala ya hizi parties nyingi, kuwe na mbili tu. Kwa nchi zingine ambazo zina democracy silikuwa hazina multiparty, na hizi nyingi ndizo sinaleta ukabila. Kwa nini kusiwe na mbili ndio kila party itafute mambo mazuri ya kuambia raia?

Maurice Kepoi Raria: So una-suggest ya kwamba there should be a limi to the number of political parties?

Speaker: Only two and one for independent candidates.

George Nakholi: Kabla hajakupatia, niambie councillor ya kwamba kama zile nchi zina demokrasia tunaangalia nchi kama America na Britain, kweli tunasikia ni vyama viwili tu pekee yake kama Britain Conservative na Labour. Na kule America ni Democratic party na Republican. Lakini kwa ukweli wana vyama hata kufika kumi na tano ama kumi, yaani vingine havisikiki. Ni vidogo sana kama Social Party, Liberal. Kwa hivyo ni maoni mazuri na tumeyaandika chini lakini wananchi wamelilia ya kwamba kuna vyama vingi sana. Kwa sababu saa hii kuna vyama arubaini na sita, ambavyo viko registered Kenya. Na hivyo kweli ni vingi, tumechukua hayo mambo.

Maurice Kepoi Raria: Pengine pia juu ya limiting ile idadi ya political parties, pengine pendekeso ambalo lingetusaidia sana ni kwamba lazima Electoral Commission wakuje na mbinu fulani, there should be a certain criteria ya ku-register political parties. Lazima kuwe na limit, pengine kusema ya kwamba chama ambacho hakina Mbunge ye yoyote katika Bunge basi wasiwe

wanasajiliwa, requirements kama hizo.

Speaker (Inaudible).....

Maurice Kepo Raria: Kwa hivyo anasema kwamba pendekezo lake ni kwamba katika Demokrasia huwezi kuzuia vyama vizidi kusajiliwa kwa sababu tutakuwa tukikataza wanachi demokrasia. Lakini anasema ya kwamba lazima kuwe na mbinu tusema kama Political parties, ili ziweza kusajiliwa ni lazima ziwe na national character, kama nimekupa vizuri, viwe vinapata support katika kila sehemu. Na niliongea juu ya hilo jambo. Na Electoral Commission itakuwa wakiangalia mambo kama hayo ili kujuu kama watasajili chama ama wasisajili.

Speaker: Inaudible:.....ninaomba kabisa ipitishwe katika Katiba mpya kwamba political parties waache vile zilivyo kwa vile ni sisi Wamaasai hatuna political party na tunataka sasa waandike katika Katiba mpya tupate kwa sababu ukingalia katika jamii yote ya Kenya wote wako na political parties na ninashangaa kwa upande wetu Wamaasai, kwa nini wale wameendelea mbele bado hawajaanzisha political party. Wakamba wako na yao, pia Wakikuyu na hata Wajaluo.....(inaudible)

Maurice Kepo Raria: Asante sana, hilo ni pendekezo lako na nime-record lakini ningependa sana kukumbusha kwamba nilipokuwa nikisema juu ya usajili wa vyama vyta kisiasa, nimesema ya kwamba, Electoral Commission ambayo ndio itakuwa ikisajili vyama, itakataza usajili wa vyama ambavyo vimeundwa kwa msingi wa kikabila. Kwa hivyo ni vizuri pia ukikumbuka hoja hiyo.

Cllr.Yene. (Inaudible).....wenyeji wa Kenya ni nani? Ni makabila arubaine na mbili, na tunata Katiba nzuri ni Katiba ambayo ina-recogonize makabila yote arubaine kwa maana hiyo ndiyo original (inaudible).....For example kama Moi alisema Kenya hatutaki ukabila, na ukiangalia ma-DC wote ni Kalenjine koti zote zina majaji na magistrates Wakalenjini, kwa hivyo kwa nini tusitambue hata Wamaasai, Waturukana, na kila mtu apewe nafasi yake? Kwa hivyo tunataka Katiba ambayo inatambua kila haki na kila kila kabila na haki yake. Kwa hivyo kwa kusema hatutaki political party yenyne ina ukabila huo ni uongo, kwa sababu hakuna mtu Kenya ambaye hana kabila.....(inaudible)

Maurice Kepo Raria: Asante sana councillor Yene natumaini kwamba katika National Conference utakuwa na ujasiri huu huu.

George Nakaholi: Kabla hujajibu councillor, nitaangalia-councillor kabla hujaenda nje- ukiangalia hiyo Preamble, kwanza kabisa tunasema sisi watu wa Kenya aware of our ethnic, cultural, yaan sisi tunajua, lazima tujue sisi ni Wamaasai, sisi ni

Wakamba, hilo ni jambo ambalo liko hapa. Kwa hivyo unasema ukweli kabisa.

Cilr. Yene: Kuongezea au ku-clarify, hapo awali administaration yote ilikuwa Kalenjin ukabila iko tu because of too much executive powers and they should be reduced. Mimi naona hii Katiba mpya yajaribu kupunguza Executives powers na pia kuwe na checks and balances na kuwe na Prime Minister maana atasaidia kupunguza zile nguvu za mtu.....(inaudible).

Maurice Kepoi Raria: Wacha tumzungumzie sasa we are going to the Executive very briefly. Unless there is something burning, we are going to the executive.

Claude Masinde: Kwa majina ninaitwa Claude Masinde. Nimeomba nigosie kuhusu District council maana mulisema ya kwamba kwenye Katiba draft inasema kuwe na uchaguzi wa watu kati ya ishirini na thelathini. Ambao watachaguliwa na watu ambao wanaishi katika hiyo district. Nikipatiana mfano wa district ya Narok, ingawaje kuna mmoja wetu aliyesema kuna kabilo tofauti katika District hii, na hapo nilielewa, lakini kuna mahali sikuelewa ndio ninataka niwekwe laini sawasawa, ya kwamba tukiwa katika District, hasa sisi Wamaasai tunakaa katika milango, tuna Purko milango mingine kama hiyo. Na hao watu hawajatoshana kwa idadi. Unakuta wengi kama Purko na ninasema bila kuwa malicious ni wengi leshinda wengine wote katika District. Na tukisema watu wa council wa District wachazuliwe na District nzima, kutakuwa na watu ambao watakuwa wamemezwa. Hivyo ninapendekeza ya kwamba, District Council isichaguliwe District nzima, ichaguliwe na wakilishi kutoka Locational Council. Pendekezo langu ni hilo. Kwa sababu kwa nyakati zilizopita, hata sasa hivi katika jumba ambalo tuko chini yake, ni vigumu sana kukuta mtu wa mlango mwengine ijapokuwa tu Wapurko. Na hilo ni wazi, sisemi kwa ubaya, ni historia ndio naguzia na ndivyo mambo yalivyo.

Nikija katika mambo ya ujaguzi, ningeomba tu Katiba ya sasa iseme registration of voters iwe Continous.

Maurice Kepoi Raria: Asante sana amezungumza zaidi, hoja ile ya mwisho ametoa ni kwamba angependa kwamba registration ya voters iwe continuos na kama ukiangalia chini ya election process, kwamba katika Katiba hii imetua haki ya kwamba registration itakuwa ikiendelea kila wakati kwa sababu. Wakenya wamesema kila dakika, kila siku, Mkenya mmoja au Wakenya wengi wanakuwa miaka kumi na nane.

Puli Emeli Kimekur: Swali umejibu, ni mimi niliuliza hilo swali, na ninataka kukuhakikisha kitu kimoja, sikufanunua nikasema Purko.....(inaudible)hapani Hapa hatukuja kubagua Maasai. Samburu ni Maasai, kila mtu aliye Kenya, sisi ni chama cha Wamasai, sisi wote ni wamaasai. Kwa hivyo hapa tuko na chairman na ni wa Loita, na hajatolewa, pengine akitolewa ma makosa yake. Na councillor waliomchagua, atatolewa akifanya na makosa, kama hana anaendelea. Kwa hivyo hatujasema kitu kama hicho. Tumesema na bado ninahimiza kusema, hapa ni Narok na ni kwa Wamaasai. Tunataka wamaasai tujitawale, kama.....(inaudible) mtu anayaamka siyo Kikuyu ama Mjalu au Mkamba, kama ni Loita hatutaki mtu

mwingine asimame, tunataka Masaai kwa sababu ni village ya Wamasaa. (MasaaiDialect):..... kwa hivyo vijana inatakikana vijana mkikuja hapa msikize mambo kwa makini.

Speaker; (Masaai Dialect).....

George Nakholi: Asante sana, tumezungumza mengi sasa tunaenda tukimaliza lakini kabla hatujamaliza nitazungumzia kwa ufupi sana juu ya upande wa Rais, au ile tunaiTa Executive. Halafu mtaangalia Executive wale wana haya magezeti ukurasa wa kumi na tisa, chapter eight. Tutazungumza halfu mwende mkaangalie wale ambao hawajaangalia muangalie. Tulipokuwa tunaenda kuchukua maoni kwa nchi yote, miezi iliyopita, tuliambiwa ya kwamba Rais yuko na mamlaka mengi sana na ni lazima ya ipunguzwe. Hata hapa bwana Oketch amesema ya kwamba Rais yuko na mamlaka mengi na labda ya itarudishwa chini kwa Katiba hii. Sasa tutaangalia tuone vile authority yake ama mamlaka yake vile iko. Watu wengi tena wamesema Raisi kwa Katiba hii amepewa yale mamlaka ambayo yanaitwa ceremonial au yale yasiyo na maana. Lakini ukweli ni ya kwamba Rais bado yuko na mamlaka ambayo ukiangalia utaona yako Kwa saa hii ye ye ndiye anateua ile office mpya iliyoundwa ya Prime Minister, ye ye ndiye mkubwa wa majeshi, ye ye ndiye mkubwa wa security council, defence council, yuko ana ipande wa shughuli za ceremonial, ye ye ndiye anaweza ku-appoint wale Ambassadors wetu, High Commissioners na wale wakubwa wengine. Yeye ndiye anaye wakaribisha Ambassadors wakiingia, ye ye ndiye anaweza ku-sign bill iwe Act, sheria, bado ni ye ye. Kwa hivyo mtu akija akisema ya kwamba Rais amenykuliwa mamlaka sivyo hivyo. Ijapokuwa ukiangalia sana, haya mamlaka nimetaja anafanya pamoja na Parliament au na Bunge. Anapata idhini ya Bunge na sasa ye ye ni huweka sahihi. Na kama hajaweka sahihi haiwezi kuwa jambo limepitishwa. Kwa hivyo Rais bado ana mamlaka ambayo mtaona kwa hizo section ambazo nimesema kwa ufupi.

Sasa nikiendelea tena, Rais akiwa amechaguliwa, sasa kwa Katiba hii, hachaguliwa na Constituency ya Narok North, na ninapeana hiyo kama example, ye ye atakuwa MP au mjumbe wa Kenya Nzima, atakuwa kwa chama mbacho kimemchangua lakini anapigiwa kura na Wakenya wote. Yaani constituency yake ni Kenya. Si kama sasa ati kuna Rais anasimama Narok North au mahali pengine, hakuna. Na sasa akipigiwa na Wakenya wote apate lazima apate asili mia hamsini na moja ndio awe amefaulu. Na juu ya hiyo lazima apate pia asilimia ishirini kwa Provinces au mikao ni tano, ndio atakuwa amepita kwa kura zxa wananchi.

Tena Rais akienda kwa kura anakuwa na Vice Wake ambaye ashamtaja kwa kile chama, na huyo anaitwa running mate. Sasa akishapita pia yule makamu wake ameshapita na wanaenda pamoja. Na huyo Makamu ni principal assistant, lasima atakuwa naye. Huyo Rais akienda safari huyo ndiye anakaa kwa kit, acting President mpaka yule arudi. Jambo likifanyika mbaya-na tunaomba Mungu haya hayawezi kufanyika-akifa yule ataingia kwa kit.

Sasa tunataangalia Rais atakuwa mtu wa aina gani, atakuwa mtu ambaye amezaliwa hapa Kenya, si by naturalization au nini, amezaliwa hapa Kenay na ana miaka thelathini na tano mpaka sabini, ni mtu ambaye Bwana Raria alikuwa amesema hapo

mbeleni ni mtu ambaye yuko na heshima yake. Kifamilia ye ye mama, na tumeongeza hapa note tukasema si ati awe ameolewa, lakini anaweza kuwa hata akiwa bachelor au spinster lakini ni mtu wa heshima yake. Awe na familia ile nzuri. Awe na tabia nzuri ambayo watu wanaheshimu. Awe na degree kutoka chuo- kinacho tambulikana, na ni lazima awe kwa party, nilisema ni lazima aingie na registered party au awe independent candidate Kwa hii Constitution kuna watu wanawenza kusimama kama independent, wale watu wanao simama kibinaksi, kama watu wanawapenda. Na nimesema hizo qualifications pia zinaingia kwa Vice President, kwa nini? Wanaenda pamoja.

Sasa jambo ambalo limeingia kwa Constitution hii ni chini ya President tunakuwa na Prime Minister, na Prime minister huyu ndiye atakuwa akiangalia Serikali au kuendesha mambo ya Serikali kutoka siku ya leo na kesho. Na tumesema kwa hii katiba ya kwamba tutakuwa na Prime minister halafu na two deputy Prime Ministers makamu wawili. Tena Prime Minister anatoka kwa chama kile kikubwa ambacho kiliongoza kwa Bunge. Ndio Wabunge ndio wanampigia kura wakiona huyu ndiye anaweza halafu jina linapelekwa kwa President. Kuidhinisha ya kwamb huyu ndiye amechaguliwa. Chini ya hao kuna Ministers au Mawasiri, Mawaziri lazima wasiwe juu ya kumi na tano. Na hao mawaziri si wabunge, wanatoka nje, wanachazuliwa kutoka kwa wananchi. Na sasa mambo ya kuchukua Army General, mtu wa Army kuwa minister wa afya hiyo imekwisha. Huyu minister lazima awe Professional, anakuja kama ye ye anaenda kuwa minister au waziri wa afya, lazima awe daktari. Kama wewe ni mtu anayeenda kufanya kazi kwa mambo ya elimu, lazima awe mtu anayejua mambo ya elimu. Na pia.....

Speaker: (inaudible)

Maurice Kepoi Raria: Hata sikuwa napendelea kukujibu lakini chukua pendekezo la draft kuwa ndio hasa stand ya Commission, kwa sababu ni lazima hao mawaziri wawe Professionals katika zile field wako nazo. Pengine Pime Minister anaweza kuwa na ujuzi wa zaidi kuliko minister. Lakini minsster vile alikuwa amesema haiwezekani mtu ambaye amesomea Agriculture aende katika Ministry ya Defence. Kwa hivyo ni lazima awe atleast professional katika hiyo field.

Speaker: Many people said that they wanted minsters to be qualified or in a particular field. you suggest that minister of health should be a doctor, the minister of education should be be a teacher, and so on. The problem of such arrangements is that the role of a minister is that of a politiciation. We need to understand the political side and also the technical side. What am saying is.....(tape ends words lost)

TAPE 7

George Nakholi: Baada ya hii utatoa maoni, yeah infact nitamaliza halafu utuoe maoni. Kuna pia hawa ministers, tutakuwa na

Deputy Ministers pia kumi na tano. Sasa jina ndilo lime geuka, badala ya kuwaita Assistant ministers, wanaitwa Deputy ministers. Na tutakuwa pia na Permanent Secretaries ambao watakuwa wakiangalia kazi ya kila Ministry, na kwa hao kumi na tano ambao ni Katibu Wakuu mmoja atachaguliwa na Bunge awe mkubwa wa ofisi ya Rais, awe Chief Secretary. Kwa hivyo hiyo kwa ufupi ndio orodha itakuwako.

Mambo muhimu ni ya kwamba kabla Rais hajapitisha kitu chochote, akiwa na Bill akitaka kupitii kwa Bunge, lazima apeleke chini kwa Prime Minister na Cabinet waangalie halafu wampatie. Sio kama hawa wanatoa Bill yoyote kwa Parliament ipitishwe. Lazima watajadiliana hapa chini halafu wapatie Rais. Rias akiipata anaweza kusema la hii muangalie tena. Niwapatie mfano, Parliament ikipitisha ya kwamba sasa tunaona kwa sababu tuko na shida sana labda tunaenda kwa vita. Rais anaweza kusema hapana muangalie hili jambo mjadiliane tena, au anaweza kupitsha na kuweka sahihi. Hilo ndilo jambo litakuwa lina-regulate kazi ya Rais hapo juu. Kwa hivyo vile tulikuwa tunalia ati Rais yuko na mamlaka mengi sana imekuwa hapo ndiyo lakini iko chini ya Prime Minister ambaye anaangalia serikali kutoka leo mpaka kesho namna hivyo.

Vile mwenzangu alisema ukiangalia ukurasa 21, tena malipo ya Rais, malipo ya Makamu wa Rais na hawa wote Ministers na wengine ya itakuwa chumi ya Salaries and Remuneration Commission ambayo imetengenezwa kwa Constituton, iko hapa ndani, tutaangalia.

Nafikiri kwa ufupi hiyo ndio structure nitasema, nitauliza kama mna jambo lolote kama mnaongeza muongezee, na ninawahimiza muende muangalie haya ambayo yameandikwa hapa kwa hii orodha ya President au Executive. Asante sana. Sasa mwenzangu ataongeza tu kidogo akiwa na jambo.

Maurice Karia: Sina jambo la kuongeza ningependa tu kutoa shukrani kwa kutupitisha sehemu hiyo ya mamlaka ambayo pia najua ni sehemu ambayo ni ya muhimu sana na tungependa kusikia maoni ya wananchi wa Narok North wanaweza sema nini juu ya mamlaka ya nchi.

Councillor Kisuru: Naitwa Kisuru kutoka Kipuniki Ward. Kuhusu mambo ya President, kwa maoni yangu mimi ni mtu mkubwa kama sisi wenyewe tulimchagua, mambo ya kubadilisha (inaudible) ----- Lakini mambo mengine anyanganywe kwa sababu President ni mtu kama mimi. Yeye pengine anaweza kuchaguiliwa President ni mtu pengine kwa roho yake ametukanwa, pengine wananchi wamekataa maoni yake, pengine mambo mengine yameharibika, waende watoe mambo yake, handle pia yeye ateremushiwe madaraka hayo, asiwe tu mtu wa kusema kitu mara moja bila Executives kuketi kujua President asiseme mambo yake yote bila kuptitia Executive. Mimi ningependa kwa maoni yangu, President arudishe maneno kwa Executive ndio President atoe tu maneno yake, sio tu kukasirika na kukimbilia na kusema pengine kwa mkutano nimesema leo na mambo fulani yafanyike siku hiyo.

Pia lingine hili la kusema vile nimeona kwa karatasi hii Wabunge wale wamechaguliwa na wananchi, candidates, Wabunge

wale wanaenda Parliament kuchaguliwa kutoka mashinani kwa wananchi, kwamba hawataenda kupewa ministries. Kuwa Minister wa Finance, kuwa wa Minister Education, kuwa Minister wa nini na nini na whatever, hawa pia mimi ningependa kusema hata ikiwa kweli mtu ataanza kupewa job saa hizi bila kuanza kufanya fanya kazi ya wananchi. Kwa sababu tunaona watu wakiwa minster wakiwa MPs ndio wananchi watasikia kuwaona wakati wowote kweli wakienda huko kazi itakuwa kubwa. Lakini kama mimi nimesoma niko na degree tatu au mbili, mimi nimesomea pengine mambo ya ngombe, au pengine mambo ya Ministry ya kilimo, ninatosha. Hata kama nimechaguliwa niende Parliament na niko na hiyo yote, mimi ningeomba tu nipewe kwa sababu mimi najua wananchi ndiyo wamefanya niende wapi, niende kule. Waruhusiwe, wapewe, kwa sababu hata Bunge, maoni yangu nasema wapewe hata walw wamechaguliwa ikiwa ana masomo ya kutosha ministry ambayo amesomea pengine masomo yake yanatosha wapewe.

Lingine la mwisho, ni mambo kuhusu sijui kama ingewezekana, hii mambo ya Wabunge kwanza kupata kauli kwa mishahara yao, wanaenda tu, unaona Wabunge wanaenda tu na kupidisha mishahara yao kuwa mingi, hata hawajaangalia mambo ya departments, ndio unaona hata walimu hawana mishahara. Na Wajumbe pesa zao ni mingi zaidi, hata councillors wana kazi kubwa kuliko hata Wabunge. Wao wana ukubwa tu kwa kazi, lakini si ukubwa katika mashinani. Hata hawa Wabunge pia wasikubaliwe wapitishe mishahara yao, hata ingawa Bunge ndilo likona nguvu, sababu hiyo mishahara ni mingi. Hawa iwe wanachaguliwa kuwa mawaziri wako na bendera, wako na nini, na ndio wanasimamia Ministry, hawa wamechaguliwa na wananchi. Mimi naona watakuwa wengi katika Parliament, mishahara yao iwe kidogo. Asante.

Maurice Karia: Asante Councillor. Juu ya mishahara tulikuwa tumezngumzia juu ya Salaries and Remuneration Commission, ambayo ndio itashughulikia mambo ya mishahara ya Waunge. Kkile tu ninahofia kama inawezekana ni kwamba pengine hakuna uwezekano wa kukata mishahara ambayo wako nayo hivi sasa kwa sababu italeta tharuki, lakini kutakuwa na Salaries na Remuneration Commission ya kuangalia mishahara ya Wabunge. Pia umezngumzia juu ya kwamba ni mapendekezo yako kwamba hata wale wajumbe amba mnawachagua waweze kuwa mawaziri. Hilo ni pendekezo lako na ni sawa. Lakini kumbuka ya kwamba wakati nyinyi mnapochagua wajumbe wenu huwa hamuwachague waende wakuwe mawaziri. Huwa mnawachagua ili waweze kuwatumikia wananchi. Na wakati mawaziri wanaenda kupewa hizo bendera ni kitu cha kujivunia, na ninaelewa kwa nini wewe ungependa mjumbe wako awe na bendera kwa sababu ni kitu ambacho constituency fulani inawenza kujivunia. MBunge wako az Wabunge wao hawana bendera, unafikiri wao wanasikia aje? Kwa hivyo tena yule mBunge wako ambaye ni minister anapotea, na nyinyi mkimuuiliza ulikuwa wapi anasema “Mzee alinituma wajua mimi ni minister. Kwa hivyo niko na hii kazi na ile.” Kwa hivyo kazi ya Wabunge ni kuwakilisha wananchi.

Lerioka Malite: Yangu ni mafupi tu, nataka ku-respond kuhusu Executive Umesema pale kwa Draft kwamba Prime Minister anawenza kuwa voted out of the government, on a vote of no confidence by 50 percent of the Members of Parliament. That one is going to create a lot of chaos because everytime we will have votes of no confidence. So let us make it difficult to dismiss a sitting Prime Minister. Let us make it two thirds majority for Members of Parliament, all present and voting. All present and voting, that is my own suggestion, not just a simple majority, two thirds majority 65 percent, all present and voting.

Halafu ya pili, tumelema kwamba tutakuwa na two Deputy Prime Ministers. That is going to be an expensive venture to have two Deputy Prime Ministers is too big. Let us make it just one Deputy Prime Minister, at least to save us some few cents or public money to invest in another project. Because it is very expensive to finance these people their salaries, per month we are going to spend one million shillings for one Prime Minister, Deputy Prime Minsiter. So let us just have one Deputy Prime Minister to lessen the bureaucracy.

Then Prime Minister should be in the Executive. Hapa mumesema kwa Draft kwamba the President is the Executive, plus I think the Vice President. Let us make the Prime Minister because he is the head of the government, in the Executive. Because as far as I am seeing this Constituion it seems as if the President will be a bit symbolic, you know ceremonial type. So the ke, ofy Parliament is the symbol of national unity. So let us make the Prime Minister the Executive, to exercise the powers of the President on behalf of the President or to exercise the powers of the Executive on behalf of the President. Hilo ni pendekezo langu.

Halafu the Vice President should be the presiding officer of the National Council or Senate, the Vice president should preside over the affairs of the National Coucil of Kenya. Because you see, the President will be, hatakuwa anafanya kazi mingi vile nimeona hapa. So if the President has less funtion then it means the Vice President will also be less functional. So what do we do with the Vice President? Let us make use of the Vice President, let him preside over the affairs of the National Council, as the Chairman of the National Council, he should be called the Chairman of the National Council. Then he should not have powers over the members of Parliament in the National Council. He should just preside but not to tamper with the Speaker, the Speaker of the Lower House has more powers. Let him just be a person within the Executive, but he should not censure a Member of Parliament, ama kuawaambia watu kuongea. Lakini Speaker wa Lower House ako na powers za ku-dismiss, Members of Parliamenet na kuwapitisha waweze ku-make speeches That is my own analysis and also he shoud be an ex-officio member of the National Council, the Vice President, because he is less functional and that is actually what I wanted to say.

Myself I support Cabinet Ministers to be non-members of Parliament, because we just elect Members of Parliament to go and represent us in Parliament. So let us appoint Cabinet Ministers outside Parliament like the American system, all Secretaries, you know, of State, Secretary of Defence, they come from outside. By the way, they don't even go to the Congress, they just make policies out of Congress, because when they go to Congress it means the Executive and the Legislature, you know they are separate, checks and balances. So let them not even go to Parliament. They should go only when it is necessary that they go to make speeches.

Interjection: (inaudible)

Lerioka Malite: That is what I am saying; they should not be there everyday. They should just be invited to give full

statements in Parliament. That is all.

Maurice karia: Thank you very much Malite. I had told you earlier that you should put down whatever you say because I really take your sentiments to be very strong, and we cannot do without them.

George Nakholi: Maliza. Delegate kuja uzungumze.

Ole Kina: My name is Ole Kina: I just want want to follow up what Mr. Malite has been saying, I concur with the powers of the President being limited, and at the same time ninaonelea ni vizuri kupunguza uwezo wa President. Vile vile, kuchagua minister ambaye si Members of Parliament naona ni vizuri. Ijapokuwa nina shida moja tukisema tufanye Minister awe ni daktari, tusema Minsiter wa Afya ni daktari, deputy ni daktari. Na pia tuwe na permanent Secretary katika ile Ministry, ninaona hapo ni kama tuna rudia rudia. There is a lot of duplication, kwa sababu kama tuna Minister ambaye ni dactari, deputy wake ni daktari, sioni haja ya kuwa na Permanent Secretary pia. Kwa sababu wakati huu tuna Permanent Secretary ambaye ni daktari, kwa sababu minitser si daktari. Kwa hivyo Permanent Secretary anaelewa ile kazi ya daktari. Je, kama tumefanya minister daktari' kwa nini tuwe na Permanent Secretary? I mean, naona hapo tunapoteza pesa za umma. Kama tutakuwa na daktari, ye ye atafanya kazi yake. Na kwa sababu haendi Parliament, bado atafanya ile administrative power yake ya ministry. Hilo ndilo pendekezo langu.

Speaker: inaudible:

Ole Kina: Ndio ninasema minister awe daktari kama ni Minister of Health, lakini ile sehemu ya Permanent Secretary katika ministry basi inakuwa redundant, haitakuwa na haja, kwa sababu kuna minister ambaye ni daktari, deputy wake ni daktari. So----

Interjection inaudible:

Ole Kina ----- No no no, ninapendekeza tusiwe na ile position ya Permanent Secretary kwa Ministries.

George Nakholi: Asante sana kwa huyo delegate wetu, nafikiri kama ni nafasi yako sasa.

Kanti Mwaniki: Mimi ni Kanti Mwaniki. Mimi nataka kuongea juu ya presidency. I have noticed that hii Draft imeamua ku-emasculate the presidency na sina shida na hiyo, but still I do have a lot of quarrel with the suggestion that the Houses of Parliament to determine their calendar own. I have a feeling that the President being the guardian of Constituion , and the symbol of the Nation should be able to dissolve Parliament if it acts unConstituion ally or has more convincing reason to extend its term or their terms. So the President should be empowered to dissolve the Parliament.

Intejection: Mr. George Nakholi: Actually there is a provision that the President can dissolve Parliament in a state of emergency.

Kagiri Mwaniki: In a state of war?

George Nakholi : In a state of war yes, he can.....

Kanti Mwaniki: So I am saying there are certain instances where Parliamentarians decide to extend their terms for no good reason, yes because of their good terms. So that should be very clear. But this time I should think they should be justified(inaudible).....Then I don't think it is necessary to put a ceiling or an upper age limit for Presidential candidates. I have a feeling that there should be no upper age limit for Presidential candidates, because -----

Interjection: (inaudible)

Mwaniki: ----- History shows us that there have been presidents in their late seventies and they have been able to do in their duties extremely well like Mandela and others. The Constitution should simply require the presidential candidates, minimum age limit should be 35. the Constitution should require that Presidential candidates be subjected to a medical check up at least to ensure that they are fit, they are not senile. Okay, to determine their fitness okay. Hakuna haja ya kusema mtu asiwe President kama ako more than 70 years, sababu in history kuna so many examples ya watu wamekuwa President even when they are aged 70, or even 80, and they have been able to do very well. Instead they should be subjected to a medical. or even sanity test to determine their ability and their (inadible)

Maurice Karia: Asante sana. Maoni yake kwa Rais amesema kwamba miaka thelathini na tano kama lower limit ni sawa lakini amesema kusiwe na limit ya juu, kwa hivyo hata Rais ambaye ako na miaka 71 kama Kibaki aweze kugombea urais. Na pia amesema ya kwamba ni vizuri sana Rais aweze kupimwa kiafya aangaliwe kama akili yake ni timamu, ama kama afya yake ni bora.

Councillor Kadera: Asante sana Commissioner. Jambo tu ni moja kwa sababu sasa nime chelewa na pole kwa kucheleva. Mimi naitwa Councillor Kadera. Jambo langu la kwanza, jambo langu tu ambalo ni la muhimu ambalo nimesikia kwamba nikienda bila kuuliza ni mbaya, ni kwamba tangu mzunguke kama Commission ya Constitution hii mpya ambayo tutafanya election, na wakati huu nasikia kwamba kama haita-fanyiwa, labda tufanyie ile tu ya zamani. Je kama, hilo tu ni swali ambalo kabla sijaendelea zaidi ni kuuliza nyinyi Commissioners. Itakuwa ni maana gani zile pesa ambayo mlitumia katika wakati huo wote itumike ama itakuwa na maana gani bado nyinyi mnazunguka na tunasikia tayari yakuwa hii Constitution haitafanya kazi?

Maurice Karia: Hilo ni swali ambalo mimi kama mwakilishi wa Commsision ningepawa kukuuliza wewe mwananchi. Kwa sababu hilo swali kwa kusema kweli lingekuwa ni wananchi wangkuwa wanasemwa, pengine ni kwa sababu gani Bunge livunjwe kabla Katiba ambayo tumeweka rasilmali nyingi sana, tumeweka pesa nyingi sana kabla haija timizwa. Kwa kweli swali hilo ingekuwa pengine ni sisi ndilo tungeuliza wananchi. Kwa hilo ni wanchi ndiyo wange tuambiakwamba iwapo Bunge litavunjwa kabla ya ku tekelezwa kwa hii Katiba nyinyi wananchi mta fanya aje?

Councillor Kadera: Basi asante sana. Hilo ni swali ambalo labda nitatoa kwa maoni yangu kwa niaba ya watu wa Narok ama watu ya Kenya ya kuwa Tume apewe nafasi ikamilishe kazi yake. Kwa sababu tangu hapo mbeleni kulikuwa na Commission ingine ikiongozwa na Raila, walijaribu, baada ya kufika mwisho, ikarudiwa, na baada ya kurudiwa, ikawa body independent body ambayo ingefaa kuwa wao wenyewe ndio wanatoa direction ama watatoa ya kwamba Constituion ile itafanyiwa kazi ndio imekuwa hivyo. Kwa sababu tunapoenda kwa uchaguzi huu, tunasikai kwamba kuna wengine wananga'nga'nia nafasi ya Waziri Mkuu, na mambo mengi, wakitarajia tu mambo ya Contitution mpya Kwa hivyo ningeunga mkono Constituion hii mpya ifanyike, kwa sababu hata unyanyasaji wa wale watu ambao labda walikiwa na power nyingi ya kunyanyasa wengine labda itaondolewa na watu watakuwa na kiti cha kisasa. Kwa hivyo mimi pia natoa jambo lingine ya kwamba inafaa Constituion hii mpya tuiunge mkono, na hata kiongozi yeote wa nchi asiwe na mamlaka ya kuvunja Bunge, na hata wale ambao wanatarajia kunyanyasa wengine ama kujaribu nafasi ya kuchukua mamlaka wa kupokonya wengine nafasi, tunaomba watu wapate hiyo nafasi.

Kwa hivyo sababu Constituion ni ya Kenya na inakubalika katika Kenya hii na inakubalika katika nchi za nje, hii Tume ikubaliwe ikamilishe kazi yake, kwa hivyo naunga mkono hiyo. Pia hii kazi ambayo mnapewa kutumia pesa kwenda wapi na wapi na ingali haitambuliwi, itakuwa ni makosa kwa kila mtu. Na hata kwa sheria ya Kenya na sheria ya dunia mzima. Kwa hivyo hata WaKenya wote wanafaa kuwa wanaungana pamoja tuweke hii mambo hata kama ni court itawekwa, hata kama ni pahali pengine, na ikubalike nayo pia kwa kupitia sauti ya Constituion, infaa pia tupitishe kuwa hii nafasi, iwe wakati mtakamilisha kazi, inapasa hao Commissioners wa Constituion wapewe uwezo wa kamilisha kazi yao, na baada ya hiyo Electoral Commission ishike kazi ya kuvunja Bunge. Sio President ndio atakuwa akivunja Bunge. Hayo ni maoni yangu, hata natumaini maoni ya Kenya nzima ya itakuwa hivyo, kuwa Electoral Commission wakati hii Constituion itakuwa tayari waitishe huo uchaguzi. hayo ndio maoni yangu, na ningeomba wa Kenya tuungane nao mambo yawe namna hiyo, asante sana.

Councillor Oyeli Mulano: Nataka ku-react sana juu ya kuvunja Bunge kabla Constituion Review haija maliza kazi yake. Hiyo itakuwa ni kinyume cha sheria, hiyo itakuwa ni misuse of resources, kwa maana nchi yetu ni masikini, na tumeweka pesa nyingi sana katika hii kazi ya Constituion. Itakuwa ni aibu, itakuwa ni udanganyifu, itakuwa ni ufidhuli na ningeomba ya kwamba kitu kama kicho kisikubaliwe hata kidogo. Itakuwa pia ni tisho kwa usalama wa nchi hii kwa mana billions hapana million, billions nne kuingizwa katika Constituion Review halafu ichukuliwe na upopo wakati 62% ya watu wa Kenya wanaishi katika poverty, itakuwa ni dhambi hata Mungu hatakubali kitu kama hicho. Na ni vizuri iingie katika record ya kwamba wale watu ambayo wateweza kuffanya kitendo kama hicho washtakiwe for committing economic treason and misuse of resources.

Ni vibaya sana na ni vizuri iingie katika report ndio kitu kama hicho kisifanyiwe watu wa Kenya kwa maana hiyo ni fujuma of the first order and the highest degree.

Jambo lingine hii hali ofisi ya President. Kwa nini huyu Prime Minsiter asichaguliwe na raia ndiyo apate power kama Prime Minister of Britain, kama Prime Minister of Israel, kama Prime Minister of Pakistan, kama Prime Minister of India, ndio President awe symbolic head, mnyanganye meno, mnyanganye meno. Awe tu symbolic head.

Interjection: (Inaudible)

Councillor Oyeli Mulano: Narudia, Prime Minister achaguliwe directly, na vote ya watu, na yeze awe accountable katika Parliament, na awe kila siku katika Parliament kujibu maswali na kuulizwa mambo ya serikali. Huyu primi minister wa hii Contitution leo anaitwa Leader of Government Business. Responsibility zile za Leader of Government Bbusiness ndio amepewa huyu. He is answerable to the President and not to the people of Kenya. We want a Prime Minister who is answerable, akichaguliwa na kura ya watu, ata kuwa answerable to the people, atakuwa answerable to Parliament. Nafikiri hayo ni maoni yangu, mimi natoa hayo kama mwananchi

Interjection: (inaudible)

Councillor Oyeli Mulano: Get me right, President hatachaguliwa na watu tena. Tunataka kutowa ile hangover of an Executive President. Tutoe hangover ya Executive President. President atachaguliwa na Parliament. Na mimi nimetoa example kama Israel ambao the President is elected by the people through Parliament. Kwa hivyo tunataka President ambaye atachaguliwa na watu kupitia Parliament. Lakini Prime Minister yule ambaye tunapatia day-to-day activities of running of the government awe answerable to the people of Kenya. Hayo ni maoni yangu, and thank you very much.

Maurice Karia: Asante sana Councillor kwa maoni yako ya kusimua kabisa. Councillor amesema ya kwamba yeze angependelea mfumo kama huyo wa nchi ya Israel ambao Prime Minister ndiye anachaguliwa na wananchi, halafu Bunge ndilo linachagua Rais. Hilo lilikuwa ni pendekezo lake na ninaweza kuwahakikishia kwamba hoja kama hiyo ilizingatiwa na Commission wakati walikuwa kwa mjadali. Walikuwa wamejaribu kuangalia watachukua model gani, ya Israel, tutafanya kama ya Britain ama ya France, halafa wakakuja na model kama hii. Kwa hivyo kama wananchi wengine watakuja watetee waseme wanahitaji Prime Minister awe anachaguliwa directly, basi tutaona kama kuna mabadiliko katika ukumbi wa National Conference.

Lerionka: My name is Lerionka. I just wanted to say that the Prime Minister should not be elected by the people because it is not logical, but the President should be elected by the people. If not then he should be elected by the Electoral College Electoral Council. So we have two cases; electing the President directly...

Interjection: (Inaudible)

Speaker: To elect a President directly ama a-elec-tive na Parliament by Electoral Council ama college

Maurice Karia: Kwa kusema kweli tukiongea mambo ya electoral college, wewe na mimi na yule mzee na pengine hawa akina mama wameelewa electoral college ni nini. Lakini hicho ni kitu kigeni sana, usijaribu kuuzia Wakenya. Kwa hivyo mambo ya electoral college tafadhali, kama unaweza kuongea kitu ambacho unajua inaweza kuvutia wananchi wengi, tafadhali hiyo itakuwa ni sawa. Lakini mambo ya electoral college ni jambo geni sana.

Lerionka: Okay, hiyo nasema electoral college ni Parliament yenyewe ku-elect President. Halafu Prime Minister nimesema kwamba awe tu ame-elect-iwa indirectly as Prime Minister by the people. So there is no need of having a Prime Minister again being elected directly by the people; I don't find any logic in by that. Thank you.

Maurice Karia: Okay, hayo ni maoni yako. Reverend hajawahi kuongea, tafadhali.

Reverend Ole Khol: Asante sana Commissioner, yangu ni mafupi tu. Naitwa Reverend Ole KholYangu ni fupi sana, ya kwamba President age yake iongezwe, ifike miaka hamsini mpaka sabini na tano. Kwa mfano sasa tunasema Uhuru is too young, he is forty one. Na ile age ambayo imependekezwa ni miaka 35. Huyo kijana bado mdogo. Kwa hivyo ili tupate mzee ambaa akikohoa anasikizwa mtu wa miaka hasini mpaka miaka sabini na tano. Na wakati term yake ni tenyears two five year terms, atakuwa miaka sitini na ita kuwa mzuri. Lakini chini ya miaka asrubaini afike amalize na fifty years, atakuwa bado very potential, na ata-retire tu hapo. atalipwa pesa mbingi ya retirement, labda hata kwa miaka mbingine thelathini, it is a waste of resources. Jambo lingine ni kuhusu Cabinet. Cabinet nasikia kwamba watakuwa nominated. Itakuwa aje wakati wanatakiwa wajibu maswali katika Bunge, kama wawo they are not Members of Parliament? Kwa hivyo pendekezo langu among the 90 nominated members, tuache 30, 15 ministers and 15 deputies. Sasa hiyo hesabu haita-zidi maana tukiongeza another thirty plus ninety itakuwaone hyundred and twenty. Watakuwa zaidi ya hata wale elected members. So ningetaka tuwache power hapo paahali pa nominated members ndio waweze kwenda Bunge akujibu maswali, and they must be qualified.

Maurice Karia: Asante sana Reverend kwa maoni yenu, asante sana kwa maoni yako. Yeye Reverend anaonelea kwamba kwa sababu Rais ana jukumu la kuangalia taifa lote, yeye anaona kwamba umri wa miaka thelathini na tano, ni kwamba ni umri mdogo. Kwa hivyo mtu kuwa Rais, pendekezo lake ni miaka hamsini hadi sabini na tano, kwa sababu anahofia ya kwamba iwapo mtu atakuwa Raisi akiwa na miaka kutoka thelathini, baada kumaliza awamu mbili ya miaka mitano atakuwa na miaka arubaini na tano na nchi-haita kuwa na fedha ya kulipa marupurupu yake kwa ziada ya miaka ambazo akonazo, bado yuko potential, bado yuko mchanga. Kwa hivyo hayo ni maoni ya Reverend, na pia tume nakili.

Councilor Surum: (inaudible).....

Maurice Karia: Asante sana Councillor Surum. Hata yeye Councillor Surum anaona ya kwamba ukumbi wa uRais ni ukumbi wa wazee, kwa hivyo sasa vijana sijui kama wako na wasiwasi na hiyo, kwa sababu walikuwa na matumaini kwamba kwa miaka thelathini na tano wataweza kupata uRais, na ninaona kwamba Councillor Surum anasema huo ni ukumbi wa wazee.

George Nakholi: Sasa wacha nipatie yule Mzee, kuja hapa halafu tuende mbele.

Dickson Kamage: Mimi naitwa Dickson Kamage, I have a suggestion, mimi nina maoni, samahani. Maoni yangu ni kwamba, kwanza kabisa tunaingia ofisi ya Rais. Rais akiwa yeye ndio ana ofisi kubwa katika nchi, in the highest office in the country, anatakiwa kuwa ni mtu wa umri wa makamu. At the age of forty five hakuna confusion. Hata kama wengine wakiona kama watu wanasema we want young people tunataka ile damu ambayo bado ni ya moto sana. Lakini damu changa isiwe ni changa sana ambaye inaingia mpaka Constituion inaingia ndani? Inatakiwa mtu wa umri wa makamu, at forty five years of age, kwamba unawenza keti na wazee, na watu wadogo, na watu wakongwe, na kisha baadaye utoe decision yako kama Rais. Au you can advise them uwe unawenza ku-advice, one.

Jambo la pili nasema ofisi ya Rais iwe na nguvu limited, iwe na limit of powers kwa sababu hzii nguvu zote zimezungushwa zikawekwa ofisi ya Rais ndio zinaleta kitu kinaitwa nepotism, kujuana. Fulani kama ni rafiki yangu, lazima ni mweke finance, na ile finance ni bank ya pesa ya nchi, ninaweka rafiki yangu, na maimi naongoza watu elfu thelathini, I mean thirty million people. Na thirty million and if I pick my friend there, he will take the 30 million, and people's funds and they will be debtors. na mimi nitakuwa naongoza watu masikini kabisa, na hiyo haita-kuwa leadership. Hiyo ndiyo inaleta kunyanya.

The other thing, jambo la pili kutokana tu na ndani ya ofisi ya Rais, Rais apunguziwe owezo wa kufanya nomination kwa sababu anaenda ana-nominate ama ana-appoint mtu kwa Cabinet ambaye hafai. You see tunaenda tunapata ma-professionals, kuna mtu ambaye ni qualified kwa finance ana Bachelor of Education ni mwalimu, ana degree ya Engineering, lakini, unakuja unakuta ni mwalimu ndio anakuwa Minister for Public Works. To become a road engineer, it means that wewe ni engineer wa barabara, umesomea mambo ya barabara unajua mambo yote yanayohusu barabara, na unawenza ku-advise kama kuna shida itatokea, unawenza kaa Bungeni na ujibu lile swali, na chochote kile inakuwa wewe ndio utaulizwa and utaweza jibu.

Nilisikia mapema mapema ikisemekana, zile sheria tulizo nazo ni zile za ukoloni, and I agree with ti kwa sababu some sheria zile watu wanatumia Bungeni ni zile out dated, za kitambo zimekaa kabisa. Kwamba zile sheria zinatumwa huko, unawenza chukua kitu ambacho hakinge faa kuingia Bunge na uingize Bunge. In such a manner, sasa ningetaka kusema namna hii. Kama hii Draft Constitution, ati hii ni mapendekezo juu ya yale mambo yanependelewa kuongewa huko, mimi mwenyewe ningesema yaongewe na yachukuliwe hatua hapo hapo. Kwamba kama ni sisi tumesema, tena sisi ni watu wa Kenya ambao hatutaki kunyanyaswa. Sisi ni watu wa Kenya ambayo nchi yetu tunataka kuishi hivi. Tukisema mambo ati hatutaki maneno yakae

namna ile, mambo ya Land Control Board, mambo ya Wamasaai na kila kitu, Katiba imalizwe ndiyo uchaguzi ufanywe ndio tujue kila kinacho semwa mahali hapa na huko Nairobi ni kitu kitachukuliwa hatua.

Isiwe ni ile Constituion ilienda kutengenezwa Lancaster House, baada ya kufika Nairobi ikapinduliwa na mtu binafsi, halafu inakuwa inam-favour yeye mwenyewe, ina mpendeza yeye mwenyewe na vile anataka kuendesha wale watu. Tumekaa miaka karibu arubaini ya uhuru ambayo unaona ni ule uhuru ni kama hamna. Kwa sababu huko ngambo Lancaster House, watu wanaweka serikali ya Majimbo, kufika hapa inabadilishwa inakuwa ni serikali ingine ya mtu binafsi. Kufika kwa wananchi, wananchi wanaambiwa maneno mengine mpkaka tunatuma watu wengine wanaenda ati kwa sababu fulani chagua fulani achaguliwe, itakuwe yeye. Commission ninawaambia nikijua representative wa Narok, one of them is Councillor Yiele who is a friend of mine, na ninajua ni mtu anaelewa kabisa kabisa, akifika huko Conference, tutasikiza kwa radio kama maneno yote yatasemekana, because I know he is not a simple man, and I know he can represent us. Kwa sababu kama ni sisi tungeulizwa, kuna watu whom we know they are good representatives.

Kwa hivyo ninapendekeza tena kwamba kama President atachaguliwa na Vice President awe huko, I also suggest kwamba tuwe na Prime Minister, who would be elected kama ni mimi ndiye ningesema, ndio akuwe controller of government business. Awe ni mtu ana powers to control the government, because you cannot control anybody without powers. If you control anything under somebody who may be controlling you, kama una-control watu, saa hii mimi kwa mfano ni kuwe Prime Minister, halafu kuna yule ana nguvu sana kushinda mimi aniambie you will control the way I want you to do, then hiyo haitakuwa control, haitakuwa control. So kama suggestion mzuri mimi ningesema Prime Minister comes from the party that controls the majority seats in Parliament, na Prime Minister awe ni elected to have what we call maximum powers to control everything.

Deputy Prime Minister, mimi ningependekeza wale wawili. Hilo ni pendeleko langu kwamba tuwe na Deputy Prime Ministers one to be in charge of Parliament affairs, na huyo mtu awe ni mwana siasa, kwa sababu huko in Parliament sisi ni wana siasa. The second Deputy Prime Minister awe in charge of the Civil Service na huyo mtu awe ni professional. Because you find in the civil service, kuna wale watu ambao siasa inawatatiza sana, na ukilete politician kwa civil service atakuwa ana shift watu, leo umeingia hii ofisi kesho umetolewa, siku ingine, tena unapolwewa kule. That is to avoid inconveniences kwa serikali na tuwe Kenya mpya, ambayo ni Kenya tunasema hii Kenya tutajitawala kama wananchi wa Kenya. Sio mtu anatutawala individually. Kwa hivyo mimi ningependekeza tuwe na two Deputy Prime Ministers. Na nimependekeza tena tuwe na Deputy President, tuwache hii mambo ya kusema ni Vice President. Ati President akitoka kwa mlango anaenda nchi za ng'ambo unakuwa kama bibi, unakaa tu, hata heri bibi kwa sababu bibi anaweza dunga ngombe mgonjwa shindano ikiwa bwana hayuko. Na Deputy President can take action immediately after the President goes out.

Maurice Karia: Na ningeli furahia sana usitumia mfano wa akina mama kwa njia usiyofaa kwa sababu tunesema Katiba hii italicinda jamii yote na itawapatia usawa. Ningependa kuwambia kwamba Vice President, inasemekana ya kwamba, wakati Rais hayuko katika nchi Vice President atakuwa acting. President takalia kile kiti kwa sababu hivi sasa Rais akienda katika nchi

ingine, Makamu wa Rais hapatiwi ruhusa kwa Katiba ya hivi sasa kukalia ile kiti. Kwa hivyo atakuwa acting President Pia tumesema kwamba jambo lolote likitokea, ama tuseme Rais ameaga dunia, basi ni makau wa Rais ndiye atamaliza hiyo awamu yake. He is going to complete the term of the President until the other election.

Interjection: Un announced: Not ninety days?

Mourice Karia: Not ninety days, atakalia hicho kiti na a-act kama President mpaka the end of that term.

Dickson Kamage: I think kile kitu kilikuwa kwa njia hiyo ya Rais kusema yeze Rais akitoka, Deputy President afanye kazi, awe acting lakini kama nimetumia akina mama kutoa mfano I apologise for that kwa akina mama, I apologise. Kwa sababu if you don't apologise may be huwezi kuwa ni mtu ana msimamo mzuri. Thank you for today, I wish this session would have continued but due to time, it is not possible. Thank you.

Maurice Karia: Asante sana Doickson Kamage kwa hoja zako ambazo ni za muimu sana. Pia ningekuomba hayo maoni yako uweke in writing, uweze kuweka in wiriting kwa sababu sisi tunaandika sketches na vile ninaona uko na mambo mengi ambayo ungetaka kuzungumzia in details, kwa hivyo pia unaweza kuandika halafu umpatie District Coordinator, ili wakati atakuja sehemu za Nairobi nafikiri kabla ya tarehe ishirini na mbili aweze kuleta hoja hizo ili ziweze kuzungumziwa tarehe ishirini na nane na Commissioners, ambao watakuwa wakitayarisha na kuzungumzia juu ya haya maoni yametoka kwa wananchi.

John Okech: Kwa jina ni John Okech. Langu la kwanza ni kusema kwamba Katiba mpya ndio dawa ya wana Kenya wote. Kwa sababu hii Katiba, tukisema, uchaguzi saa hizi na Katiba mzee, then hakuna kitu tutakuwa tumefanya. Hata hawa ma-Commissioners, saza hivi wamekaa hapa kwa roho yao hawasikii vizuri. Kwa sababu kama kuna Draft Constituion, hii ni kusema eighty five percent ya kazi wamefanya. Imebaki tu National Convention na approval ya Rais, halafu inakuwa ni Katiba, bacause we have almost spent four billion, and that is a lot of money. Because saa hizi Wakenya saa hii hawaendi kwa kazi juu ya pesa. They also need that money, around four billion sio waendelee kufutwa kazi. Kwa hiyo mimi nasema itakuwa jambo la ubinaksi mtu kusema kwamba tunaenda kwa uchaguzi na Katiba mzee. Hiyo tunasema ni makosa, tutakataa, hata tutaenda kwa demonstration, peaceful demonstration itafanywa kila mahali Kenya ili Kenya tukombolewe. Tumechoka na unyanyasaji.

Kwa sababu hii Katiba mzee imeleta haya mambo yote, kama corruption, kuna ile power ya ubinaksi, Executive power, kutoka tangu tupate independnce in 1963, 1964, tumetumiwa na hiyo Katiba mzee ya Lancaster, imebadilishwa hapa, hata Nairobi hata mzee mmoja amesema, hiyo ni ukweli, imefanya mashamba za watu zimeenda, imefanya corruption iko ndani ya serikali, imefanya nepotism iko ndani ya hii serikali, imefanya ukabila, imefanya land clashes kwa sababu ya nini, Executive powers. Na hiyo inafanywa na mtu mmoja, because those powers are too expansive. Kwa hivyo tunasema heri wapewe nafasi yao, maana ibaki kazi kidogo. March sio mbali, ama February sio mbali, wamalize ili Wakenya tukuwe relieved. Kwa sababu huu ndio wakati tumefika pahali tumechoka, hakuna kazi kwa vijana wetu, masomo ni pesa, primary hata nursery, we spend a lot of

money. Unaona, kwa hivyo tunasema Bwana Commissioner, mfanye kazi, malizeni hii kazi yenu, mpaka mfike hata March. Tuki-extend term of Parliament kwa muda wa miezi miwili kuna ubaya? Ili wamalize kazi yao. Haya, hiyo nimemaliza. Tunasema kwamba kila mahali tukienda Wakenya wanasesma they want a new Constituion ndio watoke kwa ile jela wamefungwa.

Upande wa Executive powers, tunasema kwamba Rais, vile mumesiskia ikitsemwa kwa Draft Constituion , kulingana na Commissioner anasema the President will be head of state. Kwa njia nyingine ile kazi yake itakuwa imepunguzwa lakini. Mimi naonelea ni sawa kwa sababu saa hizi atakuwa ana-appoint ndiyo but with approval. Approval ni kusema nini. Through Parliament, kwa sababu tume-elect Wabunge wetu kutoka mashinani waende huko juu ili wasiwe dormant kama saa hizi. Saa hizi unaona wako dormant. In fact wakitaka kuitisha kitu saa hizi, wanapitisha. Akisema mkulima aende kuwa ambassador saa hizi straight away tomorrow, ana kuwa US ambassy mara moja, na hiyo ni makosa. Lazima kuwe na kitu kinaitwa approval.

Ya pili, ambassador..... Nimemaliza. Hiyo, in fact tunaona haya ni matatizo ambayo yanatendeka, tangu tupate uhuru, hatusemi Rais huyu, ni Constituion tunasema, hatutaji mtu binafsi, tunasema the old Constituion imetu-lead astray. Tunasema kwamba hata akiwa saa hizi na powers ambazo amepewa bado Rais lazima tutaisha katika Africa a ikuwe na nguvu, kwa sababu MuAfrica ndiyo ana-develop. Hatuwezi ku-compare America na Kenya. Lakini tunaanza pole pole tufikie pale. Kwa hivyo tunasema na tunakubaliana hapo vile mnasema kwa Draft Constituion kuwa atakuwa na uwezo fulani, na pia kama Parliament imekataa, that is the end of it. Akitaka kuchagua Police Commissioner, lazima afuate criterea ambayo iko pale, lazima pia Wabunge waangalie huyo mtu, akisha kuchaguliwa kama ni Police Commissioner, amekuwa ni mtu aina gani, amekuwa mwizi? Anaweza kuwa na qualification, lakini ni mwizi, ama pengine ana fisadi mahali pengine. Kwa hivyo ninaonelea, vile Rais atakuwa anachaguwa, atakuwa na kile kitu kinaitwa approval. Parliament ndiyo itakuwa ina-approve, halafu inapitisha.

Lingine ni kuhusu Prime Minister, tunakubaliana na hiyo maneno, Prime Minister akuwe, atakuwa ni head of government. Yeye ndiye atakuwa anashughulika na mambo ya serikali. Sioni kama kuna tashuishi hapo kwa sababu tumeonelea, hata ingawaje atachaguliwa, Rais atamchagua, lakini atatoka from chama kilicho na Wabunge wengi, na tena Bunge litafanya nini, kama hata-kuwa na 51% majority 62 percent sijui, hatakuwa amepitishwa. Kwa hivyo nimeonelea atakuwa na uwezo amepewa. Atakuwa na uwezo amepewa na Wabunge, mimi naona atafanya kazi yake independently, kati ya.... Sema mama.

Interjection: (inaudible):

John Okech: Naonelea kazi yake itakuwa ni shwari kwa sababu atakuwa anafanya kazi ikuwa ni independent, atakuwa na majority ya Wabunge ndio wanam-back. Kwa hiyo atakuwa tu Prime Minister, pole pole namna hiyo. Halafu tukuwe na two Deputy Prime Ministers. Hiyo tunasema kwamba ni sharing of the powers, asanteni.

George Nakholi: Asante sana, mama anakuja. Lakini wewe mama tu jambo moja.

Pauline Kinyakuo: Kwa majina ninaaitwa Pauline Kinyakuo. Ni shukrani sana, unajua si vizuri kurudi kuongea yale maneno yaliongewa, tutaongea mpaka hata tukose kulala ikose ladha. Kwa hivyo mimi nimesema ni shukrani sana kwa Katiba ya wakati huu, tukiwa wana-Kenya tunashukuru sana Katiba ilioko wakati huu, ndio mmekuja kutupatia nafasi ya kujua haki yetu pahali tuko. Na kujua mabaya na mazuri. Kwa hivyo yule mtu atakuja kuvunja Parliament wakati huu ikiwa Katiba ndiyo imefikia wakati ambayo itakuja kumalizika, inaonekana yeye ni mnyanyasaji. Ili hangekubali kusema atavunja angenyamaza avumilie' kama ilikuwa na makosa aangalie mpaka makosa yatoke au uzuri utoke. Kwa hivyo tungependa kusema tukiwa wanakenya tunaambia nyinyi wa Katiba jaribuni na tunawaombea nyini Mungu tukiwa wana Kenya, wamama wote Kenya nzima tukisikia Katiba ya wakati huu ndio utatumika kupiga kura. Na tunawaambia yule ambaye alioko saa hii, ajihadhari sana asikuje kusumbua sisi wakati wa mwisho na wakati ambayo tumetumia pesa mingi sana. Kwa hivyo yeye amefanya kazi yake anaenda nyumbani, hata sisi wakati anaenda nyumbani, asitufanye tuje tugombane bure. Akae vizuri na hata sisi tufanye kazi yetu. Kwa hivyo nashukuru nyinyi mfanye kazi vizuri na tuko na imani na nyinyi, na tumeweka mkazo kwa Katiba na tumeambia nyinyi, tumewapa nguvu tukiwa wana Kenya.

Maurice Karia: Asante sana mama. Kwa kusema kweli, kama sio kwa sababu ya kuungwa mkono na wananchi, Katiba hii mnavyo-jua kwa sababu mnasoma magazeti na mnaona katika runinga, tumepita katika majoribu mengi, lakini kwa sababu ya kuungwa mkono na kwa sababu ya mapenzi yenu wananchi, hii Katiba ama Tume hii ya Kurekebisha Katiba imepata nguvu kwa sababu ya kuungwa mkono na wananchi. Kwa hivyo hatuwezi kuendelea, iwapo hatuna ile support kutoka kwenu. Kwa hivyo kama mnataka tumalize mkondo huu wa mwisho ambao ndio mgumu zaidi, bado tunahitaji mkono wenu.

Mercy Ongote: Kwa majina mimi naitwa Mercy Ongote. Pendekezo langu naweza kusema ya kwamba sijui kwa nini, ni kama nimejaribu kuangalia kulingana na vile nimekaa pale na nikajaribu ku-study kidogo nimeona ya kwamba ni kama wengi ambao wamekuja kusimama hapa wako very very biased kuhusu hii Katiba. Kwa sababu ni kama tu ile kutupa mawe kwa huyu mtu mmoja. Ningependa kupendekeza ya kwamba nimefanya research yangu mwenyewe kibinasi na nikaona ya kwamba, mimi ningeulizwa ningesema ya kwamba tuende kwa election na ile old Constituition kwa sababu ya yafuatayo. Kwa ukweli, maoni yangu, watu wengi sana wacheni niwaambie ukweli hata ukiwaliza Constituition ni nini, hata akina mama huko ndani hawajui. Wale watu tu saa hizi unaweza sema wanajua ni wale elite kidogo. Watu wengi sana huko ndani hawajui Constititon hata ukiwaliza ni nini, Hawajui.

Interjection:: Toa maoni yako tafadhali mama.

Mercy Ongote: Kwa hivyo pendekezo langu ni ya kwamba, sioni ubaya tukienda kwa elections na ile old Constituition . Wengi wamesimama hapa na kusema kwamba tumetumia pesa mingi sana. Hebu ni waulize, kwani wakati unapozaa mtoto,

anaamkatu na kuanza kutembea? Si ni mpaka kwanza crawl na mpaka asimame? Kwa hivyo mimi pendekazo langu ningesema ya kwamba hii haraka haraka ...

Interjection: Nakholi: Tumeiweka chini hiyo, maliza mama..

Mercy Ongote: Tuangalie isitupeleke vibaya. Kwa hivyo I don't see why we should not go to the elections with the old Constituion.

Maurice Karia: Asante sana. (Noise) Mercy anasema ya kwamba. Tafadhalini, mtu akitoa maoni yake ako na haki ya kusema hivyo kwa sababu tumesema Katiba hii inatokana na masikizano. Tulisema kwamba Katiba ni mkataba kwa masikizano. Na vile Mercy kama nimemuelewa vizuri amesema ya kwamba, kwa sababu bado Wekenya wengi katika hasa sehemu za mashambani hawaja elewa Katiba ni nini, yeze angeomba kuwe na muda kwa sababu bado wananchi hawajui. Kwa hivyo vile yeze ameomba ni kwa sababu wananchi bado hawajui Katiba ni nini, wapewe muda wa kuelewa mapendekezo ya Katiba mpya na kwamba yeze angependelea uchaguzi wa wakatu huu uweze kutumia Katiba ilioko hivi sasa, na hayo ni maoni yake na tutaangalia, tutaweka tutanakili, na hayo mambo pia yataweza kujadiliwa, asante.

Speaker: Yangu ni tofauti kabisa, ninaona tunafunga lakini nina maombi yangu especially kwa mambo ya United Nation ama intenational treaties, maoni yangu ni kwamba, Kenya kabla haija-sign any of those treaties, because huwa wana enda tu wana-sign, (inaudible). Before they sign those treaties, lazima wasome kwanza waelewe, halafu if there are some contentious parts they should sign those treaties with reservations. Because sometimes wanachukua tu wholesomely and there are some things as the coucilor has said which we do not agree with. Then my other contribution is that the state is obliged to protect us Kenyans. I am on the economic side. There are these things like Word Trade organizations, the COMESA and all that. You find that a poor farmer in Narok right now is affected by this issue of liberalization. I don't know, I didn't see it clearly in the Constituion but I recommend that the government should protect the people from exploitation or any negative effect from liberalization. Then I still want to recommend still on land, another issue that we are living in arid and semi arid land. That when we are subdividing our land like the people in suswa now, each person has 30 acres, yet that land is not for any activity other than pastoralism, isn't it? So I propose that there should be a policy, a good land policy enacted especially to guide on land subdivisions. Then finally the land policy and the----- (*In Masai dialect*)----- and then compensation. Asante.

Speaker: unannounced: (In Masai dialect)

George Nakholi: Tafadhali tufunge, hawa ma-delegates --- watabaki baada ya kufunga kabisa.

Ole Punuya: (*in Masai dialect*) Jina langu ni Ole punuya, nilikuwa nimetoa maoni hapo awali. hapa. Na mimi nitaongea upande wa President. Nilisikia wengine wakitoa maoni wakisema President anastahili atawale Kenya kama ana 45 years 50

years. Kwa maoni yangu ninajua kila mtu hapa atatoa maoni yake. Maoni yangu, miaka 35 hadi 80 au 75 sio shida. Kwa sababu hata kuna countries zingine ambazo unasilia President ana miaka 30 na anaweza kutawala vizuri kuliko mzee wa miaka 60 au miaka 70, kwa maana utawala wa mtu unalingana na tabia yake. Unaweza kuta mtu ambaye anatawala na ana miaka 75, na roho yake ni ya kufurughu. Na kuna mtu hata wa miaka 30 na roho yake ni ya kutawala. Unajua utawala kwanza unatokana na Mungu.

Ya pili kwa upande wa Katiba, ninasikia wengi wameongea hapa mambo wa haraka haraka Waswahili wanasema haraka haina baraka. Haya si mambo ya kesho, au mambo ya kesho kutwa. Haya ni maneno ambayo yanaundwa, yasimamie maisha ya wana-Kenya milele na milele. Na sisi Wamaasai, ukiangalia kabisa ndani ya kijiji chao au kwa manyatta yao Wamaasai hawajui kitu kinaitwa Katiba ni nini. Ni kitu ambacho unaweza kuelezewa, na mimi naomba wana Katiba ma-Commissioners, kwa haya mambo kuwa Wamaasai bado hawajaua maana yake ni nini. Nilijibu kijana ni mmoja ambaye aliongea habari ya Lancaster House. Kusema kweli serikali ya Uingereza ilikuwa imeunda Katiba ya Majimbo, Wamaasai, walikuwa wamesema majimbo. Kufika hapa anakuja kudanganya watu wote, na kuweka mambo ya kibinafsi. Hiyo ilikuwa ya majimbo, na hata sasa Wamaasai bado sasa wanadanganywa. Na mimi naomba ma-Commissioners waingie mpaka kwa kijiji, kila mtu ajue maana ya Katiba ni nini. Asanteni.

Maurice Karia: Asante sana. Jambo ambalo pengine mungependa kujuliza kuwa wakati wenu ni kwamba kwa sababu gani wa Kenya hawajui Katiba. Mnajua ya kwamba kumekuwa na Katiba ambayo imekuwa kwa nchi hii kutoka 1963, tuko na miaka 39, na pengine mungetaka kujuliza kwamba je, Wakenya wanajua hio Katiba? Na ni sababu gani Wa Kenya hawakufunzwa hiyo Katiba? Kwa sababu tunafikiria kwamba Katiba ya sasa angalao imejaribu kupanya kuliko Katiba ilioko kwa wakati huu.

Lorna Mbugua Tetu: Asante sana. Kwa majina naitwa Lorna Mbugua Tetu, I am one of the delegates, na niliamua sitafunga nyumba bila kusimama hapa. Most of the days tumekuwa tukikaa tukiwa delegates tukiwasikiza. Kuna msemo wa kusema kwamba two heads are better than one. At least leo tumekaa na tumepata maoni yenu----

Speaker: Tumeongea hapa mara ingine ndio hata bado tunaongea, at least we can say we are doing something today kwa sababu tunaona hii draft. Swali ni hili, je, will these things ever be implemented? Implementation ndio tunataka ili isiwe ya kwamba shida ya Wamaasai, maneno yote ambayo wamesema at least iwe imeandikwa kwa draft kama ile ama inaandikwa kabisa kwa sbabau kuna mambo mengi ambazo tumeshazungumzia juu yake na hata kwa hiyo draft hakuna. Ndio tumekuaj kurudia tena na tunataka iandikwe na iwe implemented, kwa hivyo tuko tayari wananchi kuenda kuwalishaa huko. (*Applause*)

George Nakholi: Mama asante sana na ningependa kuwaambia kwamba vita bado haijaisha na pengine mkondo wa mwisho

pengine ndio uko mgumu zaidi kwa hivyo what I can tell you I that as a delegate you make sure that you take this fight to the bitter end. Hiyo ni sawa?

Audience: Yes, ni sawa.

George Nakholi: Nikiongezea tu kwa mama ambaye ni delegate na delegates wengine nataka kuhakikishia ya kwamba mambo yote mlisema hapa Narok North wakati Commissioners walikuwa hapa yote imenakiliwa na ingawa huwezi kuiona hapo ukija huko kwa Constitution Review Commission na hata uki-press button tu namna hivi kwa Narok North, useme tu Narok North at the press of a button utapata mambo yote iko hapo, hakuna kitu kitapotea. Kwa hivyo mambo yote imechukuliwa na hizi tu ni summaries ambazo haziweziwe kuwa ni kila kitu. Sasa ukija huko wewe ujue mambo yote iko huko, ukija kwa NCC utakuwa ukisikiza mambo ambao imetoka huko kwa maoni na ya leo halafu msaidiane vile mko watatu muone mambo ya watu wa Narok yote iko namna gani. Asante.

Speaker: Okay, nataka kufunga. Ningependa kuchukua nafasi hii kwa ...

Maurice Kepoi Raria: Ningependa kwa sababu tunaelekea kumaliza na pia ingekuwa ni vizuri sana kama watu walikuwa wanaakilisha Tume ya Kurekebisha Katiba, ningependa kutoa shukrani zangu kwa wananchi wa Narok North ambao wamekaa kutoka asubuhi. Kama Pastor alikuwa hapa wakati tulilingia saa tatu hivi, tulimkuta Pastor ambaye alitoa hoja yake hapa na wananchi waliweza kuingia na tumestahimili mchana mzima hadi wakati huu kwa hivyo napenda kuwarudishia shukrani sana kwa uvumilivu wenu. Hasi ningependa kushukuru sana madiwani ambao wameweza kuchangia sana kwa hoja hizi. Katika sehemu zote ambazo tumewahi kuenda sehemu za Kajiado, tumeenda sehemu tatu, sehemu ya Narok, sehemu ya Narok South, sehemu ya Trans Mara. Hakuna kikao kimoja ambao tumewahi kuwa na madiwani wengine katika mkutano moja, kwa hivyo tunawashukuru sana Councillors wa Narok North kwa sababu ya bidii yenu. Kwa kusema kweli inaonekana kwamba mko na nia ya kuwasaida watu wa sehemu yenu na nashukuru sana kwa sababu kati ya hawa madiwani bado kuna wale wataenda katika kongamano ya taifa ya National Constitutional Conference.

Pia ningependa kuwashukuru akina mama ambao wametia hoja zoa, wamechangia kwa wingi. Mtakubaliana nami Bwana Nakholi kwamba akina mama katika hall wamefanya kazi nzuri sana kwa sababu hatujaona akina mama wakitoa hoja kali kali na ambao wako- well informed. Tumefurahia sana hoja zako, tunegfurahia kama ungeweza kuandika na kumpatia District Coordinator. Asante sana mama kwa sababu tangu asubuhi wewe umeridia hapa mara nyingi sana na umepunzika hapa, nyote watatu tunawashukuru sana akina mama kwa sababu ikiwa mnapenda haki za akina mama ziwekwe katika Katiba lakini nyinyi hamwezi kuja katika mkutano kama hizi basi itakuwa ni kazi ya bure. Kwa hivyo ni vizuri pia katika kazi kama hizi nanyi m jitokeze kwa wingi ili wenzeni wazee wawee kusema kwa kweli akina mama wanajaribu. Kwa sababu mambo ya affiliation Act hasa mambo ya affirmative action unakuta wazee wengine wako na tashwishi kwa sababu hawaoni akina mama wakijitokeza. Kwa hivyo muwe mukitokea katika kazi kama hizi.

Pia ningependa kurudishia shukrani na kuwapongeza wale delegates ambao wamechaguliwa katika sehemu hii kuenda kuakilisha Narok District katika kongamano la taifa la kurekebisha Katiba, tutakutana tena huko na hasa ningependa kushukuru kwa sababu nimemkuta Ole Kina ambaye tulikuwa naye chuo. Wakati mimi nikiingia kwa chuo Ole Kina ndio alikuwa anatoka, kwa hivyo nikimwona tena katika mkutano huu nafikiria kwamba ataenda National Conference na tutakutana naye huko, naona kwamba hatukupoteza wakati wetu wa shule kwa sababu tunatumia wakati huo ili kuweza kuwakilisha watu wetu.

Pia District Coordinator, asante sana kwa kazi umefanya, Tulipokuja hapa saa tatu tumekuta kwamba hall ilikuwa imetayarishwa na tunashukuru sana kwa sababu tulikuwa tunapaswa kuja hapa Jumatatu lakini ulituomba ya kwamba tuhairishe siku hiyo hadi leo kwa sababu watu walikuwa wameenda Nairobi kwa mashuguli zingine za kisiasa na tulikuheshimu tukabdalisha tarehe hiyo na ulituhakikishia ya kwamba tukikuja Alhamisi utakuwa umetangaza vizuri kwa hivyo tutakuta watu. Katika sehemu za asubuhi tulikuta kwamba viti hivi vyote vilikuwa vimejaa kwa hivyo tunakushukuru sana kwa kazi njema ambayo unafanya. Kwa hivyo kufika hapo nawashukuru nyote na Mungu awabariki. (*Applause*)

District Coordinator: Basi sina la kuongeza isipokuwa ni kusema tu asanteni sana watu wa Narok na Pasto Khol atuombee tufunge hichi kikao.

George Nakholi: Pastor kuja huku mbele uchukue

PRAYER

Pastor Khol: Baba Mungu muumba wetu tunakushukuru sana kwa ajili umesikia maombi yetu asubuhi ya kwamba utuongeze katika majadiliano haya. Tunakushukuru Mungu wetu kwa moani yote watoto wako wametoa kuhusu Katiba ya kuweza kutuongoza katika nchi hii. Tunaomba Mungu wetu ufungue njia zote ziweze kumalizika kwa njia safi na iweze kutekelezwa ili Mungu wetu makilio ya wananchi wa Kenya hii ziweze kutoseleshwa. Saidia Mungu wetu na uondoe pepo zote za muovu shetani ambaye analeta ya kuweza kuharibu Katiba hii, Mungu wetu tumekemea kwa jina la Yesu uweze kuondoa ili Baba wetu maoni hayo yote wananchi wametoa isiwe ya bure. Tunaombe ndugu zetu san ma-Commissioners ambao wamefanya kazi kubwa ya kuweza kufika pahali pote ya nchi hii na kuchukua maoni na kuandika na sasa tunaona ya kwamba sasa tuna draft ambayo Mungu wetu tutafuata. Tunaombe National Conference ili pia wakati wanajadili waweze kuwa wanaongozwa na wewe na yote ziweze kufikia masikilizano. Bariki watu wote wa nchi hii, viongozi na watu wote ili Baba wetu tukae na amani vile umetuwezesha kukaa namna hii na amani. Asante Mungu wetu.

Wote wale watasafiri kwa njia yoyote ya miguu, njia ya magari uwafikishe makwao salama salimini na Mungu wetu tunashukuru

kwa yote. Naomba kwa ajili ya Yesu Kristo Mwokozi wetu. Amin.

The meeting ended at 6.00 PM

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&